

# **Unajua Utambulisho Wako Wa Kweli?**

---

**Kitabu Cha Pili cha Masomo:**

***Kuishi Maisha yaliyobadilishwa katika  
Kristo***

# ***Bill Loveless Kristo ni huduma za uzima***

## **Hati miliki © 2011 na Bill Loveless**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiwezi kuigwa au kuchapishwa kwa faida ya kibiashara au faida. Matumizi ya nyenzo hii kwa ajili ya utafiti wa kibinafsi au wa kikundi inaruhusiwa.

Maandiko yamechukuliwa kutoka Biblia Takatifu, Toleo Jipya la kimataifa®, hati miliki ©1973, 1978, 1984, Jamii ya Kimataifa ya Biblia, imetumika kwa ruhusa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa.

Maandiko yamechukwulia kutoka Biblia Takatifu, Tafsiri Mpya ya Kuishi, hati miliki © 1996 na Uaminifu wa Usaidizi wa Tyndale. Kimetumika kwa ruhusa ya Wachapishaji wa Nyumba ya Tyndale.

Maandiko yamechukwulia kutoka Biblia ya New America Standard®, hati miliki ©1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972,1973, 1975, 1977, 1995 na Msingi wa Lockman. Kimetumika kwa ruhusa.

Maandiko yamechukwulia kutoka Toleo Jipya la Mfalme James, hati miliki © 1982 na Thomas Nelson, Inc. kimetumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.

Maswali ya maandiko yaliyowekwa (GNT) yanatoka kwenye Utafsiri wa Habari Njema katika Toleo la Leo la Kiingereza – Toleo la Pili, hati miliki ©1992 na Jamii la Kiamerika la Biblia. Kimetumika kwa ruhusa.



***Huduma za Kristo ni uzima***

**Tovuti: [www.christislifeministries.com](http://www.christislifeministries.com)**  
**Barua pepe: [bill@christislifeministries.com](mailto:bill@christislifeministries.com)**

### **Mpangilio wa utafiti huu**

Nataka kukushukuru kwa kuchagua kujifunza Unajua Utambulisho Wako Wa Kweli. Kabla uanze, naamini itakuwa na usaidizi kukupa wewe mpangilio wa utafiti. Utafiti unayo masomo sita, na kila somo lina masomo tano ya kila siku (Siku ya kwanza, siku ya pili n.k) ikiwa mnakutana kila wiki, hii itakupa wewe siku saba kukamilisha masomo tano ya kila siku. Kote katika kila somo kutakuwa na Maswali, Maandiko ya Kutafakari, na sehemu ya Kumhusisha Mungu.

#### **Maswali**

Maswali ni hasa yaliyoundwa kwa ajili yako kulinganisha kile unachoamini na ukweli ambao umeusoma. Hii ni muhimu kuonyesha imani yoyote ya uongo ambayo waweza kuwa nayo.

#### **Kutafakari kwa maandiko.**

Watu wengine hupambana na neon ‘Kutafakari’ kwa sababu ya maneno mapya ya umri. Hata hivyo, ni neon la Kibiblia ambalo hatuhitaji kuliogopa. Muhimu ni nini na nani ambaye tunatafakari juu yake. Lengo la kutafakari kwetu litakuwa juu ya Mungu ukweli wake. Naamini kwamba kutafakari juu ya neon la Mungu ni muhimu kwa sababu inaruhusu Roho Mtakatifu kuchukua ukweli wake na kufanya ufunuo kwako.

#### **Kumhusisha Mungu.**

Sehemu za kumhusisha Mungu katika kila somo ni sehemu muhimu zaidi za utafiti huu. Sehemu hii imeundwa kwa ajili yako kuomba Roho Mtakatifu kukupa ufunuo wa kibinafsi, uelewa na matumizi ya yale ambayo umesoma. Hii ni muhimu haswa unapofikia ukweli ambao unapingana na nini unachoamini. (Ikiwa hatutamtafuti Mungu kutufunulia ukweli wake, basi hatuwezi kamwe kuhamia zaidi ya imani ya uongo ambayo huenda tunaamini) kwa hivyo, kuwa na uhakika na uchukue muda kumhusisha Mungu unapopitia utafiti.

#### **Ufunuo**

Kwa vile nitakuwa nikitumia ufunuo kwa utafiti wote, nataka kufafanua nini ninacho maanisha ninapotumia neon hili. ‘Ufunuo unamaanisha tu Mungu huchukua kwa njia isiyo ya Kwaida ukweli wake na kuufanya wa kibinafsi kwako na hali zako za kimaisha. Ufunuo hukuondoa kutoka uelewa wa kiakili hadi uelewa wa Kiroho wa ukweli wa Mungu.

### **Ukweli Muhimu**

Tafadhali kumbuka ukweli muhimu unapopitia utafiti huu.

**Hautaishi zaidi ya kile unachoamini  
Ikiwa unachokiamini ni unongo basi hivyo ndivyo utakavyoishi.**

Hii ni muhimu kwa sababu kile unachoamini huathiri kile unachofikiri, tabia yako, na uchaguzi unayofanya. Kwa hivyo, moja ya malengo ya Mungu kupitia utafiti huu ni kuonyesha imani zako za uwongo, kufanya upya akili yako na kukuweka huru kulingana na Yohana 8:32. Kwa hivyo, ombi langu kwa ajili yako ni kwamba utamtafuta kupitia kwa utafiti huu wote kukuweka huru kutokana na imani zako za uwongo na athari mbovu ambazo imani hizo za uwongo zinajenga katika maisha yako.

## ***Jinsi kuelewa utambulisho wangu wa kweli unabadilisha maisha yangu.***

Kuna sababu sana ya kibinafsi kwa nini nafundisha ukweli wa utambulisho wetu upya katika Kristo. Sababu ni kwamba bila kujua na kuamini ukweli ambao hivi punde nitashiriki nawe, maisha yangu yangekuwa kwa wakati huu janga la jumla. Nililelewa nyumbani ambako baba yangu alikuwa na hasira, mwenye kudhibiti na mwenye matusi. Mama yangu alikuwa katika mfumo wa ulinzi wa kibinafsi ( kujilinda mwenyewe kutoka kwa baba yangu) wakati wangu ninapokua. Matamania yangu mapema katika maisha ilikuwa kufanya chochote kilichohitajika kwa wazazi wangu kunipenda na kunikubali. Tatizo ni kwamba kamwe sikufanya ya kutosha ‘kupata’ upendo wa wazazi wangu, kukubalika na thamani.

Hasira ya baba yangu na matusi yaliniongoza kuamini kwamba kamwe singeweza kufanya ya kutosha ili kupendwa na kukubaliwa. Matokeo ni kwamba nilianza kuunda imani kuhusu mimi mwenyewe. Baadhi ya imani ni kwamba nilikuwa sikubaliwi au sikubaliki kwa sababu nilihisi kukataliwa sana. Ni lazima nisiwe wakupendwa kwa sababu sikuweza kufanya ya kutosha kupendwa na wazazi wangu. Sikuwa na kutosha kwa sababu baba yangu alinifanya nihisi namna hiyo. Kwa umri wa 18, imani hizi zilikuwa na nguvu sana, na hatimaye zikawa ngome katika maisha yangu. Nilimwamini Kristo kwa wokovu wakati wa mwaka wangu mkuu katika shule ya sekondari. Hata hivyo, mtu alisahau kuniambia ukweli muhimu sana wakati nilipo okolewa. Ukweli huo ni kwamba mini ni uumbaji MPYA katika Kristo na matokeo yake ni kwamba ninao UTAMBULISHO MPYA.

Baada ya miaka thelathini ya kujaribu kuishi maisha ya Kikristo kwa juhudi zangu mwenyewe, imani zangu kuhusu mimi mwenyewe ya kukataliwa, kutokuwa na thamani, na kutokuwa na utoshelezi yalikuwa tu mbaya zaidi. Haikuwa hadi Oktoba 1998 ambapo niliambiwa ukweli mbili ambayo yalianza mabadiliko makubwa kwa maisha yangu. Ukweli wa kwanza ni ule nilishiriki *Kuishi Maisha Kutoka Chanzo Mpya* utafiti kwamba maisha ya Kikristo haikuwa kuhusu mimi kuishi kwa ajili ya Mungu. Badala yake, ilikuwa kuhusu Kristo kuishi maisha yake ndani yangu (Wagalatia 2:20). Hata hivyo, kama vile athari kama ukweli huo ulikuwa ni ukweli wa pili ambao nimejifunza ni kwamba wakati wa wokovu Mungu alinipa utambulisho mpya wa kuishi kutoka. Utambulisho huu mpya ni utambulisho wangu wa **kweli** kulingana na Wakorintho 5:17.

***‘Kwa hivyo, ikiwa mtu yeyote ako NDANI ya Kristo, yeye ni UUMBAJI MPYA; vitu vya zamani vilipita mbali; tazama, mambo mpya yamekuja. ‘ 2 Wakorintho 5:17***

Nilipoanza kujifunza kuhusu utambulisho wangu wa kweli katika Kristo, nilianza kumtafuta Mungu kufanya upya akili yangu kwa ukweli na kuniweka huru kwa imani hizi za uwongo. Nilipoanza kuchukua hatua za imani, Mungu alifanya kazi ya ndani sana ndani yangu kwa hatua ambapo siamini tena kwamaba nimekataliwa, bila thamani au kutosheleza. Naamini kweli katika nimekubaliwa, thamani na utoshelezi katika Kristo. Haikuwa mabadiliko ya usiku mmoja lakini ilikuwa mchakato usio wa kawaida ambao hatimaye ulifanyika. Kuwa mwaminifu na wewe, sikuwahi fikiri ningewahi kuweka huru na imani za uwongo na tabia ambazo zimesababishwa na imani hizo. Leo, hata hivyo, kama matokeo ya kazi

ya Mungu ndani yangu naweza kuthibitisha kile Paulo anasema katika Waefeso 3:20 anaposema “ Sasa kwa Yule anayeweza kufanya zaidi kwa wingi kuliko yote tunayoomba au kufikiria.”

Maombi yangu kwa ajili yako unapopitia utafiti huu ni kwamba Ataufanya upya akili yako na kukuweka huru kutoka kwa imani yote na yoyote ya uongo ambayo uko nayo kuhusu wewe mwenyewe.

## ***Jedwali La Yaliyomo***

**Somo La Kwanza - Je, unachoamini kuhusu wewe mwenyewe ni ukweli?.....5**

**Somo la Pili - Mungu alikamilisha nini kukupa Utambulisho Mpya.....21**

**Somo la Tatu -Ni nini Utambulisho Wako wa Kweli.....37**

**Somo La Nne -Mchakato wa Mungu wa Kukubadilisha kuishi kutokanana Utambulisho wako wa Kweli.....54**

**Somo la Tano - Upinzani kwa Mchakato wa Mungu Wa Kubadilisha Mstari na Utambulisho Wako wa Kweli.....66**

**somola Sita – Kupata Mitazamo Kama ya Kristo Kwa Nafsi Ukweli wa Mwisho Kuhusu Utambulisho Wetu wa Kweli .....77**

## **Somo La Kwanza**

***Je unachokiamini kuhusu wewe mwenyewe ni ukweli?***

### **SIKU YA KWANZA**

#### **Utangulizi**

Naamini kwamba kupitia kwa utafiti wa *Kuishi Maisha Kutoka Kwa Mchango Mpya*, Mungu amekupa uelewa wa ndani zaidi na matumizi ya nini ina maanisha kuishi kutoka kwa Mungu kama chanzo chetu. Baada ya kuelewa ukweli kuhusu kuishi maisha ya Kikristo, naamini kwamba ukweli wa pili wa muhimu zaidi kwa Wakristo kuelewa ni Utambulisho wao wa kweli katika Kristo. Natumai ulichukua muda kuusoma ushuhuda wangu na kuona jinsi ukweli katika utafiti huu ulibadilisha maisha yangu pakubwa. Hebu nianze kwanza kwa kufafanua neon ‘utambulisho’

#### **Tunafafanua Vipi Utambulisho?**

Huenda ukawa unauliza kwa hatua hii: una maanisha nini kwa ‘utambulisho?’

#### ***UTAMBULISHO WAKO***

***Jinsi unavyo HISI au nini unacho AMINI kuhusu wewe mwenyewe.***

Hii inaniongoza mimi kukuliza wewe maswali mawili:

- **Ni nini unaamini kuhusu wewe mwenyewe?**
- **Je, unacho amini ni ukweli?**

Unakumbuka nilichoshiriki mara kadhaa katika utafiti wa *Kuishi Maisha Kutoka Chanzo Mpya*?

#### ***Hautaishi Zaidi ya Kile unacho AMINI***

***na ikiwa unacho amini ni UWONGO basi hivyo ndivyo utakavyoishi.***

## **Inawezekana kwamba umevaa maski**



Nilitumia masks kwenye kifuniko cha mbele kama mtazamo wa jinsi ninavyoona Wakristo wengi wanavyoishi maisha yao. Najua kwa sababu nilivaa maski nyingi kwa miaka mingi sana kama Mkristo. Namaanisha nini na ‘masks?’ kama nilivyoshiriki katika ushuhuda wangu nilikuwa na imani za uwongo kunihusu kama vile sina utoshelezi, bila thamani, na mshindwa. Tatizo ni kwamba sikujua ukweli kuhusu utambulisho wangu katika Kristo. Kwa kuongezea, sikutaka wewe kuona mimi mwenyewe kama nilivyoona mimi hivyo nilijenga ‘nafsi mpya’.

Nilifanya hivi kwa kuvaa masks zakujitegemea, ujasiri wa nafsi na mafanikio.

Tatizo ni kwamba ‘nafsi mpya’ ilikuwa tu ‘nafsi ya uongo’ kwa sababu maski zilikuwa tu uongo kama kile nilichoamini kuhusu mimi mwenyewe. Kwa maneno mengine, nilikuwa nafunika ‘nafsi ya uongo’ na nafsi nyingine ya uongo.

Vipi kuhusu wewe? Kuna uwezekano kwamba unazo imani za uongo kuhusu wewe mwenyewe na umevaa mask au masks ili watu wengine wasikuone wewe kama unavyojiona wewe mwenyewe. Naamini hii ndio matokeo ya kutojua utambulisho wetu wa kweli.

***Ikiwa hujui utambulisho wako wa kweli, mazoea yatakuwa kuvaa masks kufunika nafsi yako ya uongo.***

Hoja muhimu ni kwamba ikiwa hujui ukweli utafunika imani zako za uongo na imani za uongo zaidi. Kwa hivyo, bila kujua na kuishi kutokana na utambulisho wetu wa kweli, hatuwezi kamwe kuwekwa huru kutoka kwa imani zetu za uongo. Kwa hivyo, hebu kwanza tuzuru jinsi imani zetu za uongo ziliundwa na kugundua imani zipi za uwongo waweza kuwa nazo kuhusu wewe mwenyewe.

### **Jinsi Imani zetu za UONGO Kuhusu Sisi Wenyewe Ziliundwa.**

***“Kama mtu anavyofikiri kwa moyo wake, ndivyo alivyo.”***

*Methali 23:7*

Kutoka kuzaliwa, ulianza kupokea ujumbe kuhusu wewe mwenyewe, Mungu, wengine, na kuishi maisha. Kwa ajili ya utafiti huu, tutazingatia juu ya jumbe ambazo huenda ulisikia kuhusu wewe mwenyewe. Jumbe kwa kawaida huja kwa mifumo miwili, jumbe chanya na hasi. Kwa mfano:

Jumbe **hasi** huenda ilikuwa **“Wewe ni mshindwa.” “huwezi kamwe kupima” “hii ndio bora zaidi ungeweza kufanya?” “Sikupendi.”**

Jumbe **chanya** huenda ilikuwa: **“Ninajivunia wewe.” “Unaweza ukaifanya” “Hakuna chochote ambacho huwezi kukamilisha.” “Wewe ni maalaum”**



**Zoezi :** Linganisha kwenye mchoro wa ukurasa 22 wa somo hili na umuombe Mungu kuleta akilini baadhi ya jumbe chanya au hasi ambazo umesikia kuhusu wewe mwenyewe kutoka kwa wazazi wako, wadogo wako, jamaa, marafiki, au walimu. Andika jumbe hizo chini ya vitalu juu ya ukurasa.

**Swali :** Ni kwa njia gani unaamini kwamba jumbe ambazo umeorodhesha yaliathiri kwa uzuri au vibaya namna unavyohisi au kuamini kuhusu wewe mwenyewe ?

---

---

---

**Tafakari :** Soma Methali 23:7 hapo juu na umuombe Bwana kukupa ufunuo jinsi kile unachoamini kuhusu wewe mwenyewe huathiri kila eneo la maisha yako.

### ***Ujumbe za Mara Kwa Mara Ulipelekea Imani kukuhusu Mwenyewe.***

Kama jumbe zilivyopokelewa na kurudiwa mara ya kutosha, ulianza kuunda imani kuhusu wewe mwenyewe karibu na jumbe hizo. Swali ni:

***Je unachoamini kukuhusu mwenyewe unafanana na UKWELI wa neno la Mungu?***

Hebu tuangalie katika imani mbili tofauti na tuone kama zinafanana na neno la Mungu:

**Imani :** “Mimi ni mshindwa.”

**Ukweli wa Mungu:** Katika Kristo, wewe ni zaidi ya mshindi. Warumi8:37

**Imani :** “Ninaweza kufanya chochote ambacho ninaweka mawazo yangu.”

**Ukweli wa Mungu:** Yesu anasema katika Yohana 15:5, “Mbali na mimi huwezi fanyachochote.”



Kama unavyoona, imani hizi mbili hazifanani na neon la Mungu. Naziita hizi imani za ‘uongo’ Kwa hivyo nafafanua imani ya uongo kama:

**IMANI YA UWONGO**  
***Imani yoyote kuhusu wewe mwenyewe ambayo haifanani au inapingana ukweli wa Mungu***

Katika sehemu hii inayofuata, tutachunguza baadhi ya imani zako za uongo.

### **Ni zipi baadhi ya Imani Zako Za Uongo?**

**Zoezi:** Kabla kwenda mbali katika utafiti, angalia kwenye orodha inayofuata na uchague sifa ambazo unahisi au unaamini ni kweli juu yako. (Ni muhimu kuwa mwaminifu na wewe mwenyewe unapopitia orodha hii.) unaweza kufikiria kuomba Roho Takatifu kukufunulia yale unayoamini kutoka kwenye orodha hii. Nenda kwenye mchoro kwenye ukurasa 22 na uandike chini imani zako ndani ya mviringo.

#### **Naamini au nahisi kuwa mimi ni:**

<b>Sistahili</b>	<b>Salama kwa kujitegemea</b>
<b>Sikubaliki</b>	<b>Kujiamini</b>
<b>Kukataliwa</b>	<b>Kujitosheleza</b>
<b>Mshindwa</b>	<b>Mfanikiwa kwa nafsi</b>
<b>Mwenye wasiwasi</b>	<b>Kujitegemea</b>
<b>Bila kutosheleza</b>	<b>Kujidhibiti</b>
<b>Dhaifu</b>	<b>Raslimali kwa nafsi</b>
<b>Nimeshindwa</b>	<b>wenye uwezo wa kujitegemea</b>
<b>Bila usalama</b>	<b>Bila hofu</b>
<b>Mwoga</b>	<b>nguvu kwa nafsi.</b>

Nahitaji kukujaza kwa hatua hii kwamba kila moja ya imani iliyo orodheshwa hapo juu ni imani za uongo. Safu katika upande wa kushoto naiita imani za uongo HASI, na safu upande wa kulia naiita imani za uongo CHANYA.

Imani za uwongo chanya zinaonekana kupendeza lakini tunajuaje ni imani za uongo. Neon muhimu ni ‘binafsi’. Chochote unachoamini juu yako mwenyewe ambayo ina binafsi kushikana nayo ni imani ya uwongo.

Ikiwa umechagua moja au zaidi ya imani hapo juu kama kuwa kweli kwako, basi bado unaamini imani za uongo juu yako mwenyewe. Hebu tuchunguze baadhi ya madhara mabaya ya kuamini uongo huu. lakini kabla ufanye, tafadhali fanya zoezi linalofuata.

**Zoezi :** njia moja ya kukusaidia wewe kuelewa kwamba safu mbili hapo juu ni imani za uongo ni kuongeza neno Mkristo baada ya kila moja.” Natumai kwamba inaonekana kama imani ya uongo wakati unapongeza neon la Kikristo kwa imani yako. Tutalinganisha imani zako na kile Mungu anasema katika Somo La Tatu.

### **Nini Kilichotokea Imani Zako Za Uongo Zikitiwa mkazo?**

“Kisha hatutakuwa tena kama watoto, daima kubadilisha akil zetu kuhusu nini tunachoamini kwa sababu mtu Fulani ametuambia kitu Fulani tofauti akwa sababu mtu Fulani amedanganya kwa werevu kwetu na kufanya uongo kuwa kama kweli.” Waefeso 4:14

Kwa kuongezea kwa kuunda imani za uongo, tatizo zaidi lilitokea. Uliendelea kuamini na kujenga imani hizi za uongo kwa muda mrefu unaotosha kwamba zimekuwa ukweli kwako. Mchoro hapo chini unaonyesha hoja hii.



Unapoendelea kuchukua umiliki wa imani zako za uongo, zinajijenga kwa hatua ambapo husababisha tatizo kubwa.

#### **Tatizo:**

***Baadhi ya imani zako za uongo zimekuwa za kweli sana kwako kwamba hata ukweli wa Mungu UNAPOONYESHA imani zako za uongo, bado unaamini UONGO wako.***

Unaenda kuona hoja hii kwa uwazi zaidi katika Somo La Tatu utakapojifundisha sifa za utambulisho wako wa kweli. Hoja muhimu ikiwa kwamba zaidi tunavyoendelea kuamini imani zetu za uongo ndivyo zaidi zinajengeka.

## **SIKU YA PILI**

### **Athari mbaya za Kuishi Kutokana na Imani Zako Za Uongo.**

Nilisema mapema katika utafiti huu kwamba hautaishi zaidi ya kile unachoamini. Ikiwa unachoamini ni uongo, basi hivyo ndivyo utakavyoishi. Hii inamaanisha kuwa kuna athari mbaya ya kuendelea kuishi kutokana na imani yako ya uongo ambayo inakuathiri vibaya,

uhusiano wako na Mungu, na uhusiano wako na wengine. Jina lingine la athari mbaya ya imani zetu za uongo linaitwa kuishi kutoka kwa **mwili**.

“Kwa maana tunajua kwamba sheria ni ya kiroho, lakini mimi ni wa **mwili** mnunuliwa kwa utumwa kutenda dhambi.” Warumi 7:14

**Maana ya Kibibilia ya neno “Mwili” ni tama ya mtu kuishi maisha na yeye MWENYEWE kama chanzo, KUJITEGEMEA au KANDO na Mungu kama chanzo.**

Tulizungumzia kuhusu mwili katika utafiti wa *Kuishi Maisha Kutoka Chanzo Mpya* lakini nataka kurudia tena kwa vile kwa vile inatumika kwa utambulisho wetu.

### **Kuishi Kutoka Kwa Imani ZAKO Za Uongo Hutoa Tabia za KIMWILI.**

#### **Mwili**

**Katika mazingira ya utafiti wetu ni MTAZAMO wa dhambi na TABIA zinazosababishwa na kuwa na imani ya UONGO kuhusu sisi wenyewe**

“Sasa tabia za kimwili ni dhahiri: uasherati, uovu, ibada ya sanamu, uchawi, chuki, ugomvi, wivu, ghadhabu, ugomvi, machafuko, vikundi, wivu, ulevi, utoto na mambo kama haya.”  
Wagalatia 5:19 – 21 a

Kuishi kutoka kwa imani zako za uongo kuhusu wewe mwenyewe kutaleta matokeo ya mitazamo ya kimwili au tabia za kimwili kama zile zilizoordheshwa katika Wagalatia 5:19 – 21 hapo juu. Tabia za kimwili na mitazamo huja kwa namna mbili, mwili chanya na mwili hasi. Hapo chini kuna mifano ya miili chanya na hasi.

#### **Mwili hasi:**

Mwili hasi ni rahisi sana kuona kwa sababu hutoa tabia mbaya za kimwili na mitazamo. Angalia katika mifano inayofuata kuelewa vizuri nini ninamaanisha.



**Mifano ya miili hasi:** hasira, utoshelezi, kutokusamehe, wivu, kudhibiti, uoga, hofu.

Ifuatayo ni mfano wa imani ya uongo na tabia hasi ya kimwili ambayo hutokea.

**Mfano:** - hebu tudhani kwamba moja ya tabia yako ya kimwili ni kwamba huna utoshelezi. Kile wasiostahili wanataka si kujihihisi hawatosheshezi. Kwa hivyo, huonyesha tabia za kimwili kama

vile kuwa wa umuhimu na kuhukumu wengine kufanya wenyewe kuhisi vizuri kuhusu wao wenyewe. Wanaweza wakawa watu wa kuridhisha watu kwa hatua ambapo watafanya chochote kinachohitajika ili kufikiriwa vizuri. Mwishowe, ikiwa hawawezi kutingisha hisia za kutotosheleza, wanaweza kukwepa hisia hizo kupitia tabia za kkama vile kuiga utaratibu wa kukabiliana na kazi zao, hulka, pombe, picha za ngono n.k.

### **Mwili Chanya.**

Mwili chanya ni ngumu zaidi kutambua kwa sababu huonekana ya kupendeza sana. Tatizo ni kwamba mwili chanya ni mwili ambayo huonekana nzuri lakini inawezekana kufanywa kwa kuzingatia mwenyewe au kufanywa bila kujitegemea na Mungu. Hebu nikuonyeshe mifano ya yote.



**1. Mifano ya miili chanya ambayo huzingatia juu ya NAFSI** kujiamini, kujitegemea, kuji tosheleza, ufanisi, haki ya kibinafsi.

Ifuatayo ni mfano wa imani ya uongo na tabia chanya ya kimwili ambayo hutokea.

**Mfano** : - hebu tudhani kwamba moja imani yako ya uongo ni kujiamini. Suala la kujitegemea kujiamini ni kufanya chochote kinachohitajika ili kuimarisha ujasiri huo. Baadhi ya tabia za kimwili ambazo hutiririka kutoka kwa kujiamini ni kujivunia na kusikia kama unayo majibu yote (unajua yote). Watu wenye kujiamini huwa na kiburi katika mafanikio yao na kuwadharau au kuchukua faida ya wale ambao hawafikii viwango vyao.

### **2. Mifano ya miili chanya ambayo hufanywa kwa KIJITEGEMEA NA MUNGU**

1. Kujaribu kufanya kazi yako kwa kujitegemea na Mungu.
2. Kujaribu kuwa mume wa kiungu, baba, mke au mama kwa kujitegemea na Mungu.
3. Kuhubiri kwa kujitegemea kwa Mungu.
4. Kuadhibu mtu mwingine kwa kujitegemea na Mungu.
5. Kuenda kanisani, kupeana kwa kanisa, kushiriki katika huduma ili kupata kitu kutoka kwa Mungu.

***Mwili chanya ni matokeo ya KUJARIBU kufanya mambo Fulani kwa kujitegemea na Mungu.  
Inaweza KUONEKANA ya kiroho sana au nzuri lakini ikiwa yanafanywa kwa kujitegemea na***

**Mfano wa kibinafsi wa mwili chanya kwa kujitegemea na Mungu:** Nilipoingia katika huduka miaka 12 iliyopita, nilipata mfumo wa mwili ambao sikuwa nayo kabla. Naiita mwili wa “huduma” .nini aina

nzuri sana ya mwili lakini bado ni mwili. Kwa mfano, kuna nyakati ambazo niliamka kuzungumza kwamba nilihisi nilikuwa na maelezo yangu kadhaa za nguvu kwenye komputa . Badala ya kumtegemea Mungu kuzungumza kupitia kwangu, nilifundisha kwa kujitegemea kwa nguvu zangu na uwezo wangu kwa kujitegemea na uhai wa Mungu na nguvu. Hata kama ukweli ulifundishwa, nilikuwa nafundisha na mtazamo wa kimwili kwa sababu nilifundisha ukweli kwa kujitegemea na Mungu.

Hebu tuangalie katika mitazamo zaidi ya kimwili na tabia zinazohusiana na imani yako hasi au chanya ya kimwili. Kutoka kwenye orodha mbili zinazofuata, tazama kama unaweza kutambua na tabia yoyote ya kimwili.

## **SIKU YA TATU**

### **Mifano ya Mitazamo Ya Kimwili na Tabia Inayohusiana Na Imani HASI Za Uongo**

Hapa chini pana orodha ya imani hasi ya uongo ambayo unaweza kukumbuka kutoka kwa zoezi ambayo umekamilisha kuhusu imani zako. Imani ya uongo imepigwa mstari. Inayofuata imani ya uongo ni baadhi ya mitzamo ya kimwili ambayo yanaweza kutokea kutoka kwa imani hiyo.

1. **Hastabili** - ukijihukumu zaidi, kujihukumu mwenyewe, kuwashawishi wengine kujijenga mwenyewe.
2. **Haukabaliki** – wivu, wivu, kuwa mridhisha watu.
3. **Mkataliwa** - hasira, kuwa kujihami, kataa wengine.
4. **Mshindwa** – hofu ya kufanya makosa, kuwa introspective, kuwa na wivu wa mafanikio ya wengine, kuwa peke yake.
5. **Hatoshelezi** – muhimu na kuhukumu wengine, kukataa, mridhisha watu, kuepuka kupitia mambo kama vile kazi yako, vitendo, pombe, ponografia, n.k
6. **Hofu** – kujitenga mwenyewe, ulinzi binafsi, kuepuka kushindwa kwa gharama zote.
7. **Bila usalama** – huzuni, endelea kudhibiti, kuzingatiwa na mafanikio.
8. **Kushindwa** – kujihurumia, tama, huzunika.

**Swali** : Je, yeyote kati ya tabia hizi za kimwili zinatambulika kwako?

## **Mifano ya Mitazamo Ya Kimwili na Tabia Inayohusiana Na Imani chanya ya Uwongo**

Hapo chini pana orodha ya imani chanya ya uongo na baadhi ya mitazamo ya kimwili ambayo inaweza kutokea kutoka kwa imani hizo:

1. **Salama kwa kujitegemea** – kuzingatia vitu vya kimwili, kuwa na kibri katika akili au mwonekano wako, kuwa na kuhukumu wengine.
2. **Kujiamini** – narcissistic, kujivunia, kujihudumia.
3. **Kujitosha** – kuendeshwa na utendaji, kudhibiti, kujivunia.
4. **Imefanikiwa kwa nafsi** – udikteta, kulazimisha, kuwatumikia wengine.
5. **Kujitegemea** – wa kukaa pekee, kulazimisha wengine,
6. **Kudhibi nafsi** – mkamilifu, si kuvumilia wengine, kufanya chochote kinachohitaka kubaki kwenye udhibiti.
7. **wenye uwezo** wa kujitegemea – mpenda kupingana, mkaidi, kutisha.
8. **nguvu kwa nafsi** – kudhibiti, kutawala, kidogo au hakuna uvumilivu kwa udhaifu.

**Swali** : Je, yeyote kati ya tabia hizi za kimwili zinatambulika kwako

### ***Hoja Muhimu:***

***Kuendelea kuishi kutoka kwa imani yako ya uongo kuhusu wewe mwenyewe kutakuweka katika UTUMWA kwa mitazamo yako ya kimwili na tabia.***

**Zoezi** : Tafadhali rejelea ukurasa 18 na 19 ya somo hili lenye kichwa “ Tabia ya Kimwili” na uandike hapo chini tabia tano za kimwili ambazo unataka kuwekwa hurur kutoka.

---

---

---

Chukua tabia zako za kimwili na uzitie katika nafasi iliyo hapo chini katika ukurasa wa 21, unapotazama mchoro iliyo katika ukurasa wa 21, unaweza kuona kwa uwazi jinsi ujumbe inavyounda imani ya uongo na tabia za kimwili zinazotokana na imani hizo

**Swali** andika jinsi tabia zako za kimwili zinaweza kukudhuru, mchumba wako, watoto wako, au wafanyi kazi wako.

---

---

---

## **SIKU YA NNE**

### **Nini Matokeo Ya Mitazamo Yako Ya Kimwili na Tabia?**

“kwa kuwa akili iliyowekwa kwa mwili ni kifo, lakini akili iliyowekwa kwa Roho ni uhai na amani.” Warumi 8:6

Ayah ii inasema kwamba kuendelea kuishi kutoka kwa mwili hupelekea kifo. Ni aina ipi ya kifo inazungumziwa katika Warumi 8:6? Sio kifo cha kiroho kwa sababu tunajua kama matokeo ya kuamini Kristo kwa wokovu, tunayo uzima wa milele katika Kristo na kamwe hatuwezi kufa tena kiroho.

***Kifo***  
***Kinachozungumziwa kinaelezwa katika***  
***Lexicon ya Nguvu kama***  
***“shida ya roho kama matokeo ya dhambi”***

Kwa maneno mengine, ikiwa tutaendelea kuishi kutoka kwa tabia za kimwili ambayo hutokea kwa imani zetu za kudanganya kuhusu sisi wenyewe, matokeo ya kuepukika yatakuwa **shida katika nafsi zetu**.

**Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya namna shida ya roho huonekana kama.**

Hukumu	Shida	Wasiwasi	Aibu	Kutokusamehe
Hasira	Hatia	Kiburi	Machungu	Ubinafsi
Kujihurumia	Kutostahili	Hofu	Wasiwasi	Kuchanganyikiwa
Bila thamani	Lawama	Kukataliwa	Bila usalama	Kutotosheka

**Zoezi:** kwenye orodha iliyoko hapo juu, chagua vitu vilivyo na tabia za kiroho unayopitia sasa kama matokeo ya tabia za kimwili.

---

---

---

**Swali:** Je, unataka kuwekwa huru kutokana na tabia yako ya kimwili?

**Kumbuka:** Kwamba ikiwa utaendelea kuishi kutoka kwa imani zako za uongo kuhusu wewe mwenyewe, basi wewe ni kama mtu katika 2 Petro 2:22:



*“Miongoni mwao methali ni kweli: **Mbwa hurudia matapishi yake’ na ‘saw ambayo imeoshwa hurudia kuogelea kwenye matope.**”*

Mbwa kurudia matapishi yake au nguruwe kurudia kuogelea kwenye matope ni picha kuu ya namna ilivyo kuendelea kuishi kutoka kwa tabia zako za kimwili ambayo hutokea kwenye imani zako za uongo. Ikiwa hivi ndivyo ilivyo, kwa nini tunazoea kuurudia mwili? Hapa tena, ni kile tulichokizoea. Mgonjwa kama inavyosikika, tuemjifundisha kuwa nyumbani na kuwa na furaha na huzuni ya mwili wetu.

Je, tabia yako ya kimwili inayotokana na imani yako ya uongo hufanya uhisi kama Paulo anaposema:

*“ Kwa kile ninachokifanya , sikielwi; **kwa kuwa sifanyi kile ningependa kufanya, lakini nafanya kitu hasa ninachokichukia.**”* Warumi 7:15.

Mapambano ya Paulo na tabia yake ya mwili yalikuwa makubwa sana kwa nusu ya pili ya Warumi 7:24:

***“Nani ataniweka huru kutoka kwa mwili wa hiki kifo?”***

Paulo yuko katika huzuni! Yuko katika huzuni kwamba kwamba anaonekana kuomba wakati anaomba kuwekwa huru. ‘mwili wa hiki kifo “inaashiria kwa mwili na huzuni inayohusiana mabayo iko ndani yake. Sio kuvutia kwamba Paulo hakuuliza mpango upi wa usaidizi wa kibinafsi au hatua zipi kumi zitaniweka huru?” Aliuliza,



## **“NANI ataniweka huru?”**

### **Hoja ya mwisho:**

**KUENDELEA kuishi kutoka kwa tabia yako ya kimwili kutakuweka kwenye UTUMWA wa imani zako za uongo kuhusu wewe mwenyewe. Hata hivyo, ahadi ya Mungu katika Yohana 8:32 ni kwamba “Utajua Ukweli, na ukweli utakuweka wew HURU.”**

**Mungu atakuweka huru wakati ukijua na kuishi kutoka kwa ukweli wa utambulisho wako wa kweli.**

**Maswali:** Je, unataka kuwekwa huru kutoka kwa imani amabzo unaamini kuhusu wewe mwenyewe? Unafikiri nini itakuwa matokeo ikiwa huwekwi huru? Unaamini vipi umewekwa huru kutoka kwa imani yako ya uwongo?

### **Mawazo ya Mwisho Kuhusu Mwili**

*“ kwamaana mwili huweka matamano yake dhidi ya Roho, na Roho dhidi ya mwili, kwa kuwa haya yako katika upinzani..., ili usiweze kufanya mambo unayotaka. ” Galatia 5:17*

**Hapa ni baadhi ya ukweli wa mwisho ambao tunahitaji kuelewa kuhusu mwili.**

- Mwili **hauendi mbali**. Utakuwa nasi maisha yetu yote
- Mwili **hauwezikubadilishwa** a **kuuimarishwa**. (inaweza kuwa mbaya zaidi!)
- Mtazamo wa maisha ya Mkristo **SIO** kwa wewe **kusimamia, kuondoa**, au **kushinda** mwili bila kujitegemea na Mungu.
- Nguvu yako sio ya kutosha kuwa na **ushindi thabiti** juu ya tabia yako ya kimwili.

Tutambana maisha yetu yote na mwili. Habari mbovu ni kwamba kurudia kwa maisha yetu ya kimwili, kujitegemea ni nafasi ya msingi kwa sisi sote. Kwa maneno mengine, ni rahisi kurudi kwa mwili kwa sababu hiyo ndio tumezoea kufanya. Hata hivyo, kwa vile sasa ni Wakristo, tunalo chaguo lingine. Kwa vile tunao ukamilifu wa nguvu za Mungu ndani yetu, tunaweza sasa kuchagua kutembea kwa kumtegemea nguvu za Mungu.(ambayo DAIMA hushinda mwili)

***Kwa sababu ya nguvu ya tabia za kimwili, zinaweza tu kushindwa***

***kwa kutembea kwa imani ndani ya nguvu za MUNGU.***

Ni muhimu kukumbuka kwamba nguvu zako mwenyewe na uwezo wako hayawezi kushinda tamaa yako ya mwili. Ni lazima uteke juu ya nguvu za Mungu kupitia kwa imani kusema ‘La’ kwa mwili wako.

**Maswali:** kulingana na Warumi 7:15, nini baadhi ya mambo ambayo ungependa kuwa ukifanya lakini hayafanyi au kinyume chake? Umejaribu kutofanya (au kufanya) vitu hivi ukitumia uwezo wako mwenyewe? Inafanya kazi?

---

---

---

***Ukweli muhimu kwa utafiti wetu***

***Mwili ni mtazamo na / au tabia. Sio UTAMBULISHO wako wa kweli.***

## **SIKU YA TANO**

### **Jinsi Kuishi Kutoka Kwa Imani Zako Za Uongo Huathiri Kila eneo la Maisha Yako.**

Nataka nikupe wewe baadhi ya mifano ya namna kuishi kutoka kwa imani yako ya uongo huathiri kwa kiasi kikubwa uhusiano wako, ndo yako, watoto wako, na mahalipako pa kazi.

#### **Mahusiano:**



Ikiwa rafiki amekukataa, unaweza pata hasira, machungu au kuto kusamehe. Ikiwa akili yako haija fanywa upya kwa ukweli wa utambulisho wako wa kweli, tabia hizi za kimwili zitasababisha huzuni kwa moyo wako kwa maisha yako yaliyosalia.

Ikiwa umesumbuliwa na dhulma (maneno, hisia, ngono, au kimwili) kutoka kwa mzazi, huenda umeachwa ukiamini kuwa huna thamani au “chini ya”. Ikiwa haujabadilishwa kutembea kwa ukweli, imani hizi za uongo zinaweza kukuelekeza wewe kuoja mtukanaji, au kuwa mtukanaji wewe mwenyewe. Au, zinaweza kukuzuia wewe usiwe na uhuru unaokuja kutokana na kuishi kutoka kwa utambulisho wako wa kweli.

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akupe ufunuo jinsi imani zako za uongo na/ au tabia za kimwili zinaathiri pakubwa maisha yako na maisha ya wengine.

## Dunia



Shetani, kiungu cha dunia hii, anataka kukuweka wewe kutilia maanani kwa kujaribu kupata usalama wako, utambulisho, na furaha katika vitu vya dunia. Ikiwa utaanguka kwenye mtego wake, unaweza kujaribu kutafuta usalama wako, utambulisho, furaha kwenye akaunti yako ya banki, kwa gari unayoendesha, au mahali ambapo unaishi. Tatizo ni kwamba Mungu amekataa kwa kuwa hutaweza kupata usalama, utambulisho wako wa kweli, au furaha katika nje ya maisha. Kwa kuongezea, matukio yanaweza kutokea ambayo yanaweza kuondoa vitu hivi hivyo basi kukufanya uhisi bila usalama, bila furaha, na kuhisi hasara ya utambulisho.

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akuonyeshe maeneo katika maisha yako ambako unajaribu kutafuta usalama, utambulisho, na furaha katika vitu vya dunia.

## Ndoa

Kwenye ndoa, tunazoea kukataa wenzi wetu kwa nyakati tofauti tofauti. Mazoea ni kwamba mwenzi mmoja anapokataliwa, mwili wao huleta kichwa chake kibaya na kusema, ‘nina haki ya kukataa nyuma’. Hii itajenga kile ninachoiita ‘mzunguko wa kukataa’ ambayo hatimaye itasababisha kushuka kwa kasi katika ndoa yako.

Wewe kama mwenzi unaweza kuhitaji uthibitisho mwingi. Wakati mke wako asipokupa, inaweza kulisha imani yako ya uongo kuwa huwezi. Unaweza kuitikia kwa kupata hasira au kuondoka. Ikiwa hii itaendelea, itaunda migogoro inayoendelea kwa ndoa yako.

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akupe ufunuo wa maeneo ya ndoa yako ambayo imani yako ya uongo na/au tabia ya kimwili inaunda mgogoro kwa ndoa yako.

## Watoto

Ukiwa mzazi kutokana na imani zako za uongo, tabia ya kimwili inayotoka kwa imani hizo za uongo itakuwa na athari mbaya kwa watoto wako. Kwa mfano, hasira yako inaweza kuharibu hisia zao za thamani au thamani au kuimarisha tabia ya hasira katika kujibu.

Ikiwa unapambana na kutostahili, unaweza kujitunza au kuwahudumia watoto wako ili waweze kukuhakikishia au ili uweze kujisikia vizuri kuhusu wewe mwenyewe kama mzazi.

**Kumhusisha Mungu.** Muombe Mungu akufunulie jinsi imani zako za uongo na tabia zinaathiri vibaya watoto wako.

### **Mahali pa Kazi**

Ikiwa unajaribu kupata utambulisho wako kazini kwako, kutakuwa na kupotea kwa utambulisho ikiwa utapoteza kazi. Ikiwa hujui ukweli wa utambulisho wako katika Kristo, unaweza kuwa unajaribu kutafuta thamani yako au thamani kwa kazi yako. Hii inaweza kupelekea kufanya kazi masaa marefu, ambayo inaweza kuleta matokeo ya kuwa workaholic. Ikiwa umeolewa na familia, hii inaweza kuchukua mzigo mkubwa katika kazi na familia.

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akupe ufunuo jinsi unavyojaribu kutafuta utambulisho wako , thamani yako, au usalama wako katika mahali pa kazi.

### **Muhtasari**

Natumai kwamba somo hili halija kupa tu ufunuo wa imani yako ya uongo lakini pia imedhihirisha tabia ya kimwili inayotokana na imani hizo za uongo. Najua kwamba inaweza kukatisha tamaa ikiwa utaendelea kuishi kutoka kwa imani hizo za uwongo. Naomba kwamba kama matokeo ya Mungu kuonyesha athari ambayo tabia yako ya mwili inayo katika kila eneo la maisha yako, itaunda tamaa ya sio kujifundisha tu ukweli bali pia kuwekwa huru na ukweli. Habari njema ni kwamba Mungu alijua kwamba tulihitaji utambulisho mpya kuondoa ile ya zamani. Katika somo linalofuata, tutaangalia katika nini kilitendeka kwenye msalaba na kwa ukombozi kukupa wewe utambulisho mpya.

## **Tabia za Kimwili**

### **Kuwa mtu anayejijali**

Najihurumia  
Kuwa na huzuni  
Kujidanganya  
Kuwa mwadhiriwa  
Lenga katika kuteseka  
kwangu kupata kusikika na  
kuhurumiwa Kuwa na wivu  
kwa kufaulu kwa mwingine  
na furaha yake.

### **Kujitoe pale (kujitenga)**

Jiondoe mwenyewe  
Nijiweke mbali na wengine  
kujiondoa nao Jifiche  
kinamna  
Kuwangumukufikiwa  
Wanyamazie Kataakuwasilian  
a

**Toroka** (uchungu au  
shinikizo) kwakutumia:  
Mapenzi, dawa za kulevya na  
pombe, Kuongea, Kufanya  
kitu kila wakati, Kufanya  
ulipendalo au michezo,  
shuleni, Kusoma, tarakilishi,  
raha, televisheni, sinema,  
picha za uchi, kulala, kula  
kupit akiasi, dini, kazi, ngono

**Kuwa na wasiwasi** (ingiwa  
na woga, hofu)  
Kosa amani na pumziko,  
pooza, pata tuhuma, kosa  
kuona mazuri, dhania mabaya

### **Tafuta ushauri kutoka:**

Unajimu/nyota, kuambiwa  
mifumo na uchawa

### **Kuwa mtu wa kujitegemea**

Chukua msingi wa kujikubali  
na kukubaliwa na wengine  
kwa utendaji Jione mkamilifu  
Jaribu sana usikosee, Ogopa  
kufanya makosa Kuwa  
wakisheria, Ishi “kulingana  
na kitabu” Jihisi kutengwa  
,kuwa mgumu kwako na kwa  
wengine, weka viwango  
zisizowezezana kwako na  
kwa wengine

### **Jazwa na mambo kama:**

Ufanikishaji,  
kutambulika/hadhi, kujipatia  
vitu za dhamana, vile  
wengine hunifikiria,  
ninavyofanana, afya yangu,  
siku za nyuma (hasa  
yaliyokuuma au ulikofeli),  
kujitoe kwa mjengo, amri na  
udhibiti

### **Kuja kutawala**

Kuwa dikteta (mwenye  
kusema) Kuwa mwenye  
kudai Kuwa Jabari  
(ukidhibiti) Watishe wengine  
Kataa kukubali

### **Kaa kwa udhibiti** kwa:

Kusaliti (kutia vitisho)  
Simamia (tumia hatia,  
huruma, ukinya, ujeuri, n.k  
Kuingilia (vitisho) Kuapa,  
Batili (kuonyesha unyonge)  
Kutokula

### **Kosa huruma au upole**

Kuelewa, wema, upendo,  
jihami

### **Kuwa wa kujihesabia haki**

(kujihalalishia)  
Peana visababu (boresha)  
Funikia makosa  
Dhibitisha fikra yako  
Dhania wewe sio tatizo  
Zuia kuchukua majukumu  
Kwa kufeli au kwa shida  
Kuwa na ugumu kwa:  
kuomba msamaha, kuomba  
msaada, ama kutoshukuru,  
kuwa na mtazamo mkali  
unaosema “Najuamiminani”  
“Njia yangu ndiyo ya kweli”

### **Kuwa na mkali** (waku hukumu)

Pata kosa kwa wengine,  
binafsi na chochote  
kinachokuzunguka,  
kuyapelekea mambo kwa  
kifo, chuki (sio vumilivu),  
lalamika sana (hakuna  
chochote kizuri hata)

### **Kuwa na uhakika**

Naweza jitegemea badalaya kut  
egemea Mungunawengine,  
kuwanakiburi, kuwanahisabu,  
patamaringo,  
kuwawakujisifu, kujivuna

**Kuja kuwa asiye jali,**  
asiyelianawengine, tofauti au  
asiyeshughulika

**Kuwa mtu aliye ridhika na  
yote:** sema mambo kama,  
“nisawa” ama “haidhuru”

**Kaa ukimakinika**

Pata ugumu wa kujiburudisha

**Pata tama** (mbaya)

Kosa uhakika na matumaini, pata wasiwasi, kosa kuamini wengine, wewe, Mungu, kanisa nahata serikali, Tarajia mabaya, kutoridhika kivyako au na wengine, kukosa kutosheka

**Kuwa na uhasama**

Bila rafiki, pata dhihaka, kuwa na dharau, kuwa na chuki, kuwa mkatili, kuwa na hasira ya haraka, kuipa hasira yangu pengo, kuwa wa kutusi, midomo yenye matusi, vunja vitu

**Kuwa na uhasama** (kata tamaa)

,nuna, machungu, asiyesamehe, weka kadri ya ulikokosewa, jaribu kulipiza kisasi, unataka wengine kufeli ama kuudhiwa, kujiadhibu au kuadhibu wengine

**Pigana bila haki**

Pata kashfa

Wakilisha hali visivyo, sengenya, husika katika tabia za kuudhisha: tumia ucheshi kuficha hisia za kweli, sahau mambo, kataa kuwasiliana, chelewa, kuacha.

**Kuwa wa kujishusha chini**

Dhania mimi ndiye shida kila wakati Kuwa mgumu Kwakukiri Kuwa mgumu Sana kwangu, asiye na kufaulu kukifaa Kuwa na ugumu na kuchukua upendo,

maoni, kusamehe, kutoweza kujisamehe

**Wape wengine changamoto**

Kataa na mamlaka

Kuwa asiye shirikiana, kuwa asiye guzika, letaupinzani, kuwawakuwakerawengine, kuwa mwenye kujadili, kuwa msumbufu (asiye na mazao), kuwa asiye leta umaana

**Kataaukweli**

Puuza shida na utarajie itaenda, Kataa yote ni mabaya Kuwa na lengo Jidanganye na wengine pia Yachukulie mambo kwa uzito, Leta mchezo kuyaficha mambo.

**Tanguliza**

Fichakile ninachofikiria kujifanya, jaribu kuwafurahisha wengine au kuwavutia, jaribu kuiga kwa usichokijua, kuwa wajuujuu (usitake yeyote awe mwepesi kwako)

**Kuwambatili** (kosaari)

Kata tama kiurahisi Usichukue nafasi Ngoja mtu wa kukuambia utakachofikiria na utakachokifanya Tangatanga Zuia kufeli kabisa Ahirisha mambo Kuwa asiye wajibika Kuwa mvivu Kosa pumziko Kosa subira Kuwa wa kuchukizwa kwa urahisi

**Kulinda hisia zako**

Zuia urafiki wa kimapenzi Pata ugumu kueleza hisia na maoni.

**Ishi kwa hisia zangu**

Amini kuwa ukweli ndiyo nahisi, niwe makini sana kwa kukashifiwa, niwe mmakinifu zaidi, niwe mchokozi, mwenye kuongozwa na woga, shaka na kutokuwa salama huelekeza kwa kukataliwa

**Kuwawakufarahisha**

Jaribu kuweka kila mtu na furaha

Zuia migogoro ama weka amani, niseme ninachofikiria watu wanataka, kuwa mwenye kutii zaidi, niko na ugumu kusema “la”, siwezi jipigania, naogopa kuwasikitisha wengine, najipeane kwawengine kwa urahisi

**Kuwa mwenye Kulinda**

(mkombozi)

Kuwa umelindwa zaidi Kuwa umewajibika zaidi Kuwa wa kuhusikana mambo ya wengine Kuwa mwenye ameekezwa Ongea sana nausikize kidogo Fanyia wengine maamuzi

**Chukulia mambo kwa**

**uzito** (mkali) Hutaweza kufurahia kosa furaha na maisha

**UJUMBE KUHUSU MIMI MWENYEWWE NILIOPOKEA:**

--	--	--	--

***Imenifanya kuhisi na kufikiri  
namna hii kuhusu mimi mwenyewe:***

**IMANI ZA UONGO**  
**NAHISI au NAAMINI**  
**MIMI NI:**

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_



**TABIA ZA KIMWILI ZINAZOLETA IMANI YA UWONGO**

---

---

---

## Somo La Pili

### Nini Mungu alikamilisha kukupa Wewe Utambulisho Mpaya?

#### **SIKU YA KWANZA**

##### **Utangulizi**

Natumai kwamba ulijifundisha katika somo la mwisho baadhi ya imani ya uongo kuhusu wewe mwenyewe na tabia za kimwili zinazotokea kutoka kwa imani hizo za uongo. Naamini kwamba matamano yako ni kwamba unataka kuwekwa huru kutoka kwa imani yako ya uongo na tabia za kimwili. Katika somo hili, tutaona nini Mungu alikamilisha kwa wokovu kukuweka wewe huru. Nitakuwa nikitumia nambari ya michoro kuonyesha baadhi ya kweli muhimu. Siwezi kukuhimiza ya kutosha kuomba kupitia somo hili badala ya kujaribu kusoma kweli hizi kwa kutumia akili. Muombe Roho kukupa ufunuo ya kile ambacho utasoma hivi karibuni. Hebu tuanze kwa kuelewa mpango wa Mungu wa mwanadamu.

##### **Mpango wa Mungu wa Mwanadamu**

1 Wathesalonia 5:23 inatufunulia kwetu mpango wa Mungu wa mwanadamu:

*“Sasa Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; na **Roho**yako na **Moyona mwili**wako uhifadhiwe...”*

Aya hii inatuonyesha kuwa mtu ni sehemu tatu. Tumeundwa kwamwili, moyo, na roho ya mwanadamu. Hebu zaidi katika maana ya mwili, moyo na roho ya mwanadamu.

**Mwili** – mwili unawakilisha mwili wa **kimwili** au sehemu yako ambayo inaonekana. Hapa ndipo unahusiana na ulimwengu wa kimwili. Hapa ni mahali pa hisia zako tano. Hapa ndipo makao ya sehemu mbili zifuatazo za kuwa kwako, moyo na roho ya binadamu. Vinaweza kuwa vigumu kiasi kuelewa kwa sababu **havionekani**. Mwili utapita, lakini moyo na roho ni milele.

**Moyo** – moyo ni utu wa **pekee** au sehemu ya kisaikolojia ambayo unahusiana na watu na hali za maisha. Nafsi imeundwa na **akili** yako, (Methali 23:7), **mapenzi** ( 1 Korintho 7:37a), na **hisia** (Luka 10:33)

**Roho ya mwanadamu** – seshemu ya tatu ya kuwa kwako ni roho ya mwanadamu. Roho yako ya mwanadamu haifai kuchanganyikiwa na roho takatifu. Roho yako ya mwili ni ile sehemu ya kuwa kwako toka kuzaliwa. Hata hivyo, hukupokea Roho Mtakatifu mpaka hatua ambapo ulimwamini Kristo kwa imani kwa wokovu.

Wakati Mungu alisema katika Mwanzo 1:26 kwamba aliumba mwanadamu kwa mfanano wake, alimaanisha kwamba aliunda mwanadamu kwanza kabisa kama ‘**kiumbe roho**. Yohana 4:24 inatufunulia kwamba sisi, kama viumbe roho, twaweza kumwabudu Mungu:

*“Mungu ni **Roho**, na wale wanaomwabudu lazima waabudu katika **Roho** na ukweli.”*


Kwa kuongezea kwa kumwabudu Mungu kutoka kwa roho yetu ya mwanadamu, ni pia kutoka kwa roho yetu ya mwanadamu ambapo tunajifundisha kutoka (Jobu 32:8), mkutano na (Zaburi



51:12), pokea ufunuo na hekima kutoka (Waefeso 1:17), na muhimu zaidi kuwa na uhusiano wa ukaribu na Mungu (Warumi 8:16)

***Hoja muhimu ya utafiti huu ni kwamba roho ya mwanadamu ni mahali pa UTAMBULISHO wako.***

Mchoro unaofuata unasaidia kuonyesha mwili, moyo, na roho ya mwanadamu:



Ukweli ni kwamba hatuwezi tukajiweka chini katikati na kuona sehemu hizi tatu. Hata hivyo, naamini kwamba mchoro huu utakupa wazo nzuri zaidi wa sehemu tatu za mwanadamu. Tutaona kwenye mchoro inayokuja kwa nini ni muhimu zaidi kuelewa kwamba moyo na roho ya mwanadamu ni tofauti kabisa.

### **Hoja Muhimu Zaidi Ya Kukumbuka.**

Wakati mwingine watu huchanganyikiwa moyo na mwili wa mwanadamu kama ilivyo thibitishwa na jinsi wanaweza kuzitumia kwa kugeuza. Hata hivyo, neno la Mungu inaifanya wazi kabisa katika Waibrania 4:12 kwamba kuna tofauti kati ya mbili:

*“Kwa maana neno la Mungu ni kuishi na hai na kali zaidi kuliko upanga wowote wa kuwili, na kupiga mbali mpaka mgawanyiko wa moyo na roho.”*

Hili ni andiko muhimu sana kiasi kwamba inaeleza kwa uwazi (kama vile Wathesalonia 5:23 ifanyavyo) kwamba moyo na roho ni tofauti kipekee. Utaelewa utofuti vizuri tunapoendelea kwenye utafiti. Inatosha kusema kwa sasa kuwa tofauti ni kwamba moyo ni mahali pa uelewa wa kibinafsi wakati roho ya mwanadamu ni mahali pa ufahamu wa Mungu.

***Fikiria kuhusu hili***

***Mungu hukuona wewe kwanza kabisa kama kiumbe cha ROHO kuwa na uzoefu wa kibinadamu badala ya Mwanadamu kuwa na uzoefu wa kiroho.***

**Maswali** : je, umefikiri kuhusu wewe mwenyewe kuwa kwanza kabisa kiumbe roho? Inaweza kuathiri vipi namna unavyojiona na wengine ikiwa ulijiona wewe mwenyewe kama kiumbe roho kuwa na uzoefu wa kibinadamu badala ya kiumbe mwanadamu kuwa na uzoefu wa kiroho?

---

**Tafakari**: juu ya ukweli kwamba moyo wako ni tofauti na roho yako ya mwanadamu kama ilivyo andikwa katika Thesalonia 5:23 na Waibrania 4:12.

**Kumhusisha Mungu**: Muombe Bwana akupe uelewa wa ndani zaidi juu ya ukweli kwamba yeye hukuona kimsingi kama kiumbe roho imefungwa ndani ya mwili wa kibinadamu.

## **SIKU YA PILI**

### **Hali Ya Mwili, Moyo, na Roho Ya Adamu Na Hawa**

Sasa kwa vile unaelewa tofauti kati ya mwili, moyo, na roho ya mwanadamu, nataka kuangalia katika hali ya mwili, moyo na roho ya Adamu na Hawa kabla kuanguka. Hii ni muhimu kwa sababu tutaona namna zilivyobadilika baada ya kuanguka.

**MWILI** – ilikuwa MILELE. (Mwanzo 1:27)


**MOYO** – ilikuwa MKAMILIFU. (Mwanzo 1:26)

1. Akili zao zilikuwa za kuamini UKWELI.
2. Hisia zao zilikuwa katika UMOJA KAMILI na Mungu na kwa kila mmoja.
3. Mapenzi yao yalikuwa mara kwa mara kuchagua kutembea kwa wakati na wakati KUMTEGEMEA juu ya Mungu.

## **ROHO YA MWANADAMU** – (Warumi 6:11)

1. Ilikuwa HAI kwa Mungu.
2. Ilikuwa MFU kwa dhambi.

Kwenye ukurasa unaofuata ni mchoro kuonyesha hali za Adamu na Hawa kabla kuanguka.



### **Wakati Adamu na Hawa Walitenda Dhambi, Mambo Yalibadilika.**

Mpango wa Mungu kutoka mwanzo ulikuwa kwamba Adamu na Hawa watapata maisha mengi na ya milele. Hata hivyo, ili mwandamau aendelee kupata maisha haya ya milele na mengi, Mungu alimpa mwanadamu mapenzi huru kufanya uchaguzi. Chaguo hilo lilikuwa kuendelea kuishi wakati kwa wakati kwa utegemezi juu ya Mungu kama chanzo chao au kufanya uchaguzi wa kidhambi na wa kuto tii wa kuishi kwa kujitegemea bila Mungu.

Tunajua kutoka Mwanzo 3 kwamba walijaribiwa na Shetani, hawakumtii Mungu, na kula kutoka kwenye mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Kwa wakati huo, hali zao zilibadilika pakubwa. Hebu tuone nini Bibilia inatuambia kuhusu nini kilibadilika kuhusu kilicho badilika.

**Kwa hatua ambapo Adamu na Hawa walitenda dhambi, hali zao zilibadilika:**

- Roho zao za kibinadamu zili KUFUFA kwa sababu ya dhambi. (yaani kifo cha kiroho). Hali ya roho ya mwanadamu ilibadilika. Kwa sasa ni MFU kwa Mungu na HAI kwa dhambi.

*“kwa hivyo, kama vile dhambi imeingia ulimwenguni kupitia mtu mmoja na kifo kupitia dhambi, na namna hii kifo kikawajia watu wote, kwa sababu wote walitenda dhambi.” Warumi 5:12*


- Walikuwa Wakitengwa na Mungu MWENYEWE.

*“Lakini uovu wenu umefanya utengano kati yakona Mungu wako, na dhambi zako zimeficha uso wake kutoka kwako, ili asisikie.” Isaya 59:2*

- Walikuwa wakitengwa kutoka kwa UHAI wa Mungu na Nguvu.

*“Kuwa giza katika ufahamu wao, walijitenga na maisha ya Mungu...” Waefeso 4:18*

Mchoro hapo chini unaonyesha hali ya Adamu na Hawa baada ya kuanguka. Angalia kwamba roho ya mwanadamu haiishi tena kiroho.



## **UKWELI MUHIMU**

***Kabla kuanguka, roho ya Adamu na Hawa ilikuwa HAI kwa Mungu na MFU kwa dhambi. Hata hivyo, baada ya kuanguka roho ya mwanadamu ikawa MFU kwa Mungu na HAI kwa dhambi.***

### **Vipi Uamuzi wa Adamu na Hawa Ulikuathiri Wewe?**

*“Kwa hivyo kama vile kupitia **mtu mmoja dhambi** iliingia duniani, na **kifo kupitiadhambi** na hivyo kifo **kilienea kwa watu wote**, kwa sababu wote walitenda dhambi.” Warumi 5:12*


Tatizo ni kwamba sisi sote tumetoka kwa Adamu na Hawa. Kama matokeo, ulipozaliwa kimwili, ulirithi uharibifu wa kiroho kutoka kwa Adamu na Hawa. Kwa maneno mengine, ulirithi hali yao ya kiroho baada ya kuanguka

**Wakati wa kuzaliwa kimwili, ulirithi hali ya Adamu na Hawa:**

- **Ulizaliwa MFU KIROHO** kwa Mungu – Warumi 5:12
- **ULITENGANISHWA** kutoka kwa Mungu – Isaya 59:2
- **ULITENGANISHWA** kutoka kwa MAISHA na NGUVU za Mungu – Waefeso 4:18

Mchoro unaofuata unaonyesha hali yako ya kiroho wakati wa kuzaliwa (Tambua kwamba roho ya mwanadamu ni mfu kwa Mungu lakini hai kwa dhambi).

## Ulirithi hali ya Roho wa Adamu na Hawa ulipozaliwa kimwili




### **SIKU YA TATU.**

#### **Matumizi Kwa Sehemu Mbili Za Msalaba**

Nataka kutumia michoro ya miviringo kwa pande mbili za msalaba tulizungumzia juu yake katika Kitabu Cha Kwanza Kuishi Maisha Kutoka Chanzo Mpya. Kumbuka kwamba kulikuwa na pande mbili za msalaba: Upande wa DHAMBI na upande wa MAISHA ya msalaba. Kama ukumbusho, hebu tuangalie katika pande mbili za msalaba kwenye mchoro ufuatao.

## Sehemu MBILI ya Msalaba




Kabla tuangalie kwa pande mbili za msalaba tukitumia michoro ya mviringo, utaona kwenye upande wa MAISHA wa msalaba nimeongeza kwamba ‘Mungu alisulubisha nafsi yako ya zamani na utambulisho wako wa zamani na kuibadilisha kwa roho mpya ya mwanadamu na utambulisho mpya.’ kwa hivyo, hebu tuanze na upande wa dhambi wa msalaba.

### **Sehemu ya Kwanza – Upande wa DHAMBI kwa Msalaba**

Kumbuka kwamba kile Kristo alikamilisha katika kufa na kutukomboa kutoka kwa dhambi zetu.

Upande wa DHAMBI wa msalaba.

## *The SIN Side of the Cross*



### **Suluhisho La Mungu Kwa Upande Wa Dhambi Wa Msalaba – Kristo alikufa KWA AJILI Ya Dhambi Zako.**


“Ndani yake, tunao ukombozi kupitia damu Yake, msamaha wa makosa yetu, kulingana na utajiri wa neema yake ambayo alitupa.” Waefeso 1:7

“Lakini Mungu huonyesha Upendo wake mwenyewe kwetu kwa wakati tulikuwa bado wenye dhambi, Kristo ali tufia.” Warumi 5:8

Sisis, kama waumini, tunajua kwamba ikiwa Kristu hakwenda msalabani ili kutoa msamaha wa dhambi, hakungekuwa na wokovu au upatanisho na Mungu. Bado tungekuwa tumetengwa milele kutoka kwake na kuwa na lengo la kuzimu. Hata hivyo, Mungu, kwa neema na upendo wake kwa ajili yako, alimtuma mwanawe Yesu kufa kwa ajili ya dhambi zako ili kwa kumpokea Yeye kwa imani kama mwokozi wako, utapata milele naye. Kwa hivyo, sehemu ya kwanza ya suluhu ya Mungu ilikuwa kwa Yesu kufa kwa dhambi zako. Tunaona kwenye mchoro mviringo unaofuata kwamba dhambi zetu zilifutwa kupitia kifo cha Kristo msalabani.



# Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu



***Hata hivyo, ingawa dhambi zilishughulikiwa, kulikuwa na ZAIDI ambayo ilihitajika kufanywa kwa wokovu***

Hebu tuvunje kila ukweli wa upande wa MAISHA wa msalaba.

## **Upande Wa MAISHA Msalabani.**

Kwa kuongezea kwa kuondoa dhambi zetu, Mungu bado alihitaji kushughulika na roho yetu ya mwanadamu ambayo ilikuwa mfu kwa Mungu na hai kwa dhambi. Bado tulikuwa na utambulisho wetu wa zamani na bado tulikuwa tumetenganishwa na Mungu. Hivyo basi, hebu tuangalie kile Mungu alifanya kuponya masuala haya. Kumbuka kuwa tulisoma kwamba nini Mungu alikamilisha kwa kuongezea kuondoa dhambi zetu inaitwa upande wa MAISHA wa msalaba. Mchoro kwenye ukurasa unaofuata unafupisha Upande wa MAISHA wa msalaba.


## **SIKU YA NNE**

### **1. Mungu Aliweka UKAMILIFU wake ndani Ya Mwanadamu.**

Kwa sababu mwanadamu alitenganishwa kutoka kwa Mungu kama chanzo chake cha kuishi maisha, kitu cha kwanza Mungu alifanya ni kujiingiza tena ndani ya mwanadamu. Kama matokeo ya kuokolewa, sasa tuko katika Kristo, na matokeo kwamba ukamilifu wote wa uungu unaishi ndani yetu. Tunaona hili katika Wakolosai 2:9, 10.

*“Kwa maana ndani ya Kristo ukamilifu wote wa Uungu unaishi katika muundo wa mwili, na umepewa ukamilifu ndani ya Kristo, ambaye ni kichwa juu ya kila nguvu na mamlaka.”*  
Wakolosai 2:9, 10

Sasa unao Baba, Yesu, na Roho Mtakatifu. Angalia kwenye mchoro kwenye ukurasa unaofuata ambao unaonyesha ukweli huu.



#### **UKWELI MUHIMU**

***Mungu aliweka UKAMILIFU Wake Mwenyewe ndani ya mwanadamu ili mwanadamu SIO lazima awe chanzo cha kuishi maisha.***

**2. Mungu aliweka UHAI wake na NGUVU ndani ya Mwanadamu.**  
**MAISHA ya Kristo.**

*“...Kristo ambaye ni maisha yako...”* Wakolosai 3:4

*“Mimi ndimi....maisha.”* Yohana 14:6

***Kristo aliweka UKAMILIFU wa MAISHA yake ndani yako uwe maisha YAKO na kukidhi mahitaji yako.***


**NGUVU za Mungu.**

Kwa kuongezea kwa maisha ya Kristo, sasa unao nguvu zote za Mungu. Paulo anatujuza kuhusu hili katika 2 Wakorintho 4:7

*‘Lakini tuna hazina hii katika mitungi ya udongo ili kuonyesha kwamba hizi nguvu zote zenyenguvu zinatoka kwa Mungu na sio kwetu.’*

***Mungu aliweka NGUVU yake ndani yako KUKUBADILISHA wewe kufikiri, kuamini, kuchagua, na tabia kulingana na ukweli wa utambulisho wako wa kweli.***

Mchoro unaofuata unaonyesha hili.



**3a. Mungu Alisulubisha NAFSI YAKO Ya kale na UTAMBULISHO WAKO WA KALE.**

Ukweli muhimu ambao tunastahili kuanza nao ni huu:


***Imani zako chanya na hasi kuhusu wewe mwenyewe KABLA Ya wokovu uliunda UTAMBULISHO WAKO WA KALE.***

***Roho yako ya mwanadamu ndio pahali pa UTAMBULISHO WAKO WA KALE.***

kumbuka kutoka kwenye mchoro wa mviringo wa kwanza kwamba utambulisho wako unapatikana katika roho yako ya kibinadamu. Kile ulichoamini kuhusu wewe mwenyewe kabla hujaokolewa ni utambulisho wako wa zamani. Kwa hivyo, utambulisho wako wa kale ulipatikana kwenye roho yako ya kibinadamu. Hapo chini ni mchoro unaoonyesha ukweli huu.

# Roho yako kabla ya kuokoka inayo utambulisho wako wa awali

Mungu  
Maisha  
Nguvu



**UKWELI MUHIMU** : Kumbuka kwamba kile ulicho amini kabla ya kuokolewa ni nani kweli WEWE.

**Swali:** Je, unafikiri kwa nini nilitumua wakati uliopita ‘ULI’ katika sentensi hapo juu?

***Kwa sababu ya hali yako ya kiroho Kabla Wokovu, haukuwa na uchaguzi bali  
KUAMINI Imani za***


***uongo za utambulisho wako wa zamani na KUISHI KUTOKA kwa tabia ya kimwili ya  
utambulisho wako wa zamani.***

Roho yako ya mwanadamu ambayo ilikuwa mfu kwa Mungu na hai kwa dhambi inaitwa katika Biblia ‘ubinafsi wako wa kale’ (Tazama Warumi 6:6 hapo chini) kwa vile utambulisho wako unapatikana katika roho yako ya mwanadamu , utambulisho wako wa kale ni sehemu ya ‘nafsi yako ya kale. Kabla Mungu kukupa roho mpya ya mwanadamu na utambulisho mpya, alipaswa kushughulika na nafsi yako ya kale na utambulisho wako wa kale. Kwa hivyo,

**alisulubisha** na nafsi yako ya zamani na utambulisho wako wa kale (na Imani zako zote za uongo) **pamoja na Kristo** kwenye msalaba. Tunaona kweli hizi katika aya zifuatazo.


*“Mimi (roho ya mwanadamu aliyekufa na utambulisho wa zamani) ulisulubiwa na Kristo na mimi (roho ya mwanadamu aliyekufa na utambulisho wa zamani) haiishi ten..”* Wagalatia 2:20a (mgodi wa msala)

Mchoro ufuatao unaonyesha utambulisho wako wa zamani ukisulubiwa na Kristo kwenye msalaba.



**Nukuu:** Huenda ukawa unauliza, “ Je, ni vipi nafsi yangu ya zamani na utambulisho wa kale unaweza kusulubiwa na Kristo tangu kusulubiwa kwa Kristo kulifanyika zaidi ya miaka 2000 iliyopita? “ jawabu kwa hilo ni kwamba katika ulimwengu wa milele na Mungu hakuna wakati. Kila kitu kiko pamoja na Mungu ili iwe bila kujali wakati unapookolewa, Mungu anaona nafsi yako ya kale na utambulisho wa zamani ukisulubiwa na Kristo msalabani. Hii ni kweli zaidi ya ufahamu wa mwanadamu. Kama maandiko yote, hapa ni pahali ambapo tunapaswa kuamini kwa imani.

**Zoezi:** Andika kwenye mduara wa kati chini ya jina “Utambulisho wa kale” imani zako za uongo kutoka kwenye mchoro kwenye ukurasa 22.



**Swali** :kulingana na kile tulichojifunza tu, nini kilichotendeka kwa imani yako ya uongo kwa wokovu kulingana na Warumi 6:6 na Galatia 2:20?

**Kutafakari** : juu ya Warumi 6:6 na Wagalatia 2:20 na umuombe Mungu akupe wewe ufunuo na uelewa wa ndani zaidi wa umuhimu kwamba roho yako ya mwanadamu ya kale na utambulisho wa zamani vilisulubiwa pamoja na Kristo.

**Kumhusisha Mungu** : Muombe Mungu akupe ufunuo wa ndani zaidi juu ya ukweli kwamba imani za uongo ambazo bado unazo kuhusu wewe mwenyewe vilisulubiwa msalabani.

**SWALI MUHIMU**

*Ikiwa imani zako za uongo ni sehemu ya utambulisho wako wa zamani ambao ulisulubishwa msalabani , basi unahitaji kuendelea kuamini imani zako za uongo tena?*

## SIKU YA TANO

### 3b. Mungu ALIBADILISHA nafsi yako ya kale na utambulisho wako wa zamani kwa roho MPYA ya binadamu na Utambulisho MPYA.


“kwa hivyo ikiwa mtu yeyote yuko **katika Kristo**, yeye ni **uumbaji mpya**; mambo ya zamani yamepita; tazama, **mambo mapya** yamekuja.” 2 Korintho 5:17

Ayahii inasema wakati ambapo ulimwamini Kristo kwa wokovu, ulikua uumbaji mpya. Kuwa uumbaji mpya kuna maanisha kwamba sasa unayo roho mpya wa mwanadamu na utambulisho mpya katika Kristo. Mambo ya kale katika 2 Korintho 5:17 (akiashiria roho yako ya mwanadamu ya kufa na utambulisho wako wa zamani) vilisulubiwa (vilipita). Na ‘mambo’ mapya (roho yako mpya ya mwanadamu na utambulisho mpya) ulipewa na Mungu kwa wokovu. Kwa maneno mengine, kwa wokovu, Mungu alibadilisha utambulisho wako wa kale na utambulisho mpya.

Ezekia 36:26-27 anaeleza ubadilishaji wa utambulisho wako wa zamani kwa upya:

“.....nita...vaa **roho mpya**( **roho mpya ya kibinadamu na utambulisho mpya**) ndani yako, na nitaondoa **moyo wa jiwe** (**roho ya mwanadamu iliyokufa na ya kale**) kutoka kwa mwili wako....” (mgodi wa msala)

Mchoro unaofuata unaonyesha jinsi Mungu ALIBADILISHA nafsi yako ya kale na utambulisho wa zamani kwa roho mpya na utambulisho mpya





**Maswali:** Ikiwa Mungu amekupa wewe utambulisho mpya, je unastahili kuendelea kyuishi kutoka kwa utambulisho wako wa kale? Itabadilishaje jinsi unavyoishi ikiwa huishi tena kutoka kwa imani zako za uwongo?

**Kutafakari :** Juu ya 2 Korintho 5:17 na Ezekiel 36:26-27 na umwombe Mungu akufunulie wewe ukweli kwamba alibadilisha utambulisho wako wa kale kwa utambulisho mpya.

#### **4. Mungu Amejiweka Katika UMOJA Na Wewe.**


Sasa kwa vile wewe ni uumbaji mpya, Mungu alikamilisha kitu moja zaidi kwa wokovu. Alijiweka mwenyewe katika UMOJA na wewe. Kwa maneno mengine, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu waliungana kwa roho mpya ya kibinadamu ya haki ( utambulisho mpya). Mungu anafunua ukweli huu katika aya inayofuata:

*“ Lakini huyo ( Muumini) anayejiunga mwenyewe kwa Bwanani rohomoja(katika umoja na) nayeve.” 1 Korintho 6:17 (mgodi wa msala)*

Huna tena Mungu ambaye ametenganishwa nawe. Mungu wako sasa yuko katika umoja wakaribu, wa milele na usioweza kutenganishwa nawe. Soma Yohana 14:20 kwa uthibitisho zaidi wa uhusiano wako wa muungano.

*“Katika Siku hiyo utajua kwamba Niko ndani ya Baba Yangu, nawe ndani yangu, na mimi ndani yako.”*

Mchoro kwenye ukurasa unaofuata unaonyesha utambulisho wako mpya katika UMOJA na Mungu.



**Maswali** : Kwa kuwa Mungu yuko katika muungano usioweza kutenganishwa nawe, je anaweza kukuacha au kukuacha ( Waibrania 13:5)? Ikiwa Mungu yuko katika Muungano usioweza kutenganishwa na wewe, unaweza kupoteza wokovu wako?

**Kutafakari** : Juu ya Korintho 6:17 na Yohana 14:20 na ufikiri kuhusu ukweli kwamba Mungu yuko katika muungano na wewe.

**Kumhusisha Mungu** : Muombe Mungu akufunulie kwa njia ya ndani zaidi nini inamaanisha kwa wewe kuwa katika muungano na yeye. Ikiwa kwa namna Fulani unaamini kwamba unaweza kupoteza wokovu wako, mwombe Mungu akushawishi kwamba haiwezekani kwa sababu ya umoja wake usioweza kutenganishwa na wewe.

**Swali** : ikiwa unashuku upendo wa Mungu kwa ajili yako, kuna uwezekano kwamba kupitia yote ambayo alifanya kwa ajili yako kwa wokovu unaweza kushawishika kwa njia ya ndani zaidi kwamba kwa kweli anakupenda?

**Tafakari** : juu ya yote ambayo Mungu alikufanyia kwa msalaba na kwa wokovu kusamehe dhambi zako, kukupa wewe uhai wake, na kukupa wewe utambulisho mpya. Je, kutafakari juu ya kweli hizi unakupa moyo mkuu wa shukrani?

**Kumhusisha Mungu**: ikiwa unashuku upendo wa Mungu kwa ajili yako, Muombe yeye atumie yote ambayo umesoma kwa somo hili kukushawishi wewe juu ya upendo wake kwako.


### **Hebu tupitie Pande Mbili za Msalaba**

Kufanya muhtasari wa sura hii, angalia kwenye upande wa DHAMBI na MAISHA wa msalaba mara moja tena.

# SEHEMU MBILI ZA MSALABA

**DHAMB**

**ISHA**



Kristo alikufa ili usamehewe  
dhambi zako Waefeso 1:7

Mungu alijiweka KIKAMILIFU kwako  
Wakolosai 2:9,10

Mungu aliweka NGUVU zake na MAISHA  
kwako Wakolosai 3:4;Waefeso 1:19,20

Mungu ALISULUBISHA mwili wako wa  
awali na utambulisho wako na  
KUIBADILISHA kuwa Roho mpya wa  
mwanadamu na utambulisho mpya  
Warumi 6:6;2Wakorintho 2:17

Mungu alijiweka PAMOJA nawe Yohana  
14:20

## **Muhtasari**

Ninaamini kwamba unahimizwa na yote ambayo Mungu alikamilisha kwa msalaba kurejesha roho yako ya kibinadamu kwa hali sawa na ile ya Adamu na Hawa kabla kuanguka. Habari njema ni kwamba huhitaji kuamini imani za uongo ambazo unazo kuhusu wewe mwenyewe. Yote haya yalifanywa kama matokeo ya upendo wa Mungu na tamaa ya kukuteka wewe katika uhusiano wa karibu na yeye mwenyewe. Katika somo linalofuata, utatambua utambulisho wako mpya katika Kristo.

**Somo la Tatu**  
***Ni nini utambulisho wako wa kweli?***  
**SIKU YA KWANZA**

**Utangulizi**

Ninaamini kwamba kama matokeo ya kile ulichosoma katika somo la mwisho kwamba una ufahamu bora Zaidi wa kile Mungu alifanya kwa wokovu kukupa wewe utambulisho mpya. Nataka kuanza somo hili kwa kukupa wewe njia nyingine ya kuelewa nini Mungu alifanya ndani yako kwa wokovu. Baada ya mjadala huu, tutaona utambulisho wako mpya katika Kristo.

**Njia nyingine ya kuelewa nini Mungu alifanya kwa wokovu**


**“NDANI” YA ADAMU**

Nataka kukupa wewe njia nyingine kuona nini Mungu alikamilisha kwa kuondoa utambulisho wetu wa zamani na kutupa moja mpya. Kama tulivyotaja kabla, tulirithi hali ya Adamu ya kiroho. Njia nyingine ya kusema hili ni kwamba kwa kuwa sote tumekuja kutoka kwenye jeni la Adamu, sisi sote tumezaliwa katika Adamu.

Kama matokeo, sehemu ya utambulisho wetu wa zamani NDANI ya Adamu inamaanisha kwamba kabla wokovu, tulitambulikana na Adamu katika:

- Kifo cha kiroho – 1 Korintho 15:22
- Utenganisho kutoka kwa Mungu na Uhai wake na nguvu – Efeso 4:18, Isaya 59:2
- Kuhukumiwa – Warumi 5:18
- Utambulisho wa zamani – (yaliyoundwa na Imani zako za uongo) – Methali 23:7

Tunaona katika mchoro unaofuata muonyesho wa nini inaonekana kuzaliwa KATIKA Adamu.




## **“KATIKA” KRISTO**

Hata hivyo, kama matokeo ya kumwamini Kristo kwa wokovu, hautambulik tena na Adamu katika kifo chake cha kiroho, utenganisho, kuhukumiwa na utambulisho wa zamani. Wakati wa wokovu, Mungu alikuondoa nje ya kuwa ndani ya Adamu na kukuweka wewe ndani ya Kristo na matokeo kwamba wewe sasa unatambulika na Kristo

Mchoro unaofuata unaonyesha nini Mungu alifanya wakati wa wokovu katika kukuchukua wewe kutoka kwa kuwa KATIKA Adamu na kukuweka katika Kristo.

Mungu alikuchukua kutoka kwa kuwa KATIKA Adamu na  
Kukuweka KATIKA Kristo.



*Ulikuwa na utambulisho wa zamani katika Adamu kabla ya wokovu.*

*Hata hivyo, kwa vile sasa uko ndani ya Kristo, unao utambulisho MPYA.*

### **Ni ipi hali yako mpya kwa vile sasa uko katika Kristo?**

#### **1. Uko HAI kiroho**

Mungu alikuleta wewe kutoka kifo hadi kwa uhai. Tunaona hii katika Korintho 15:22: “kwa maana katika Adamu wote wanakufa, kwa hivyo **katika** Kristo wote watafanywa **hai.**” 1 Wakorintho 15:22

## 2. Sasa uko katika umoja na Mungu.

Hautenganishwi tena kutoka kwa Mungu. Tumeona hili hapo nyuma katika Yohana 14:20

*“Katika siku hiyo utajua kwamba niko katika baba yangu, nawe ndani yangu, nami ndani yako.*

## 3. Wewe sasa ni mwenye haki

Kuna njia nyingine muhimu ambayo ulikua kutambulika na Kristo. Mungu aliposulubisha utambulisho wako wa zamani usio na haki ndani yako, aliibadilisha na utambulisho mpya wenye haki. Hauko tena chini ya hukumu. Mungu alikufanya wewe mwenye haki katika utambulisho wako mpya. Onyo: unaweza kuwa na mapambao na ukweli huu lakini angalia kwa neno la Mungu kuhusu uhaki wako.

*“kwa maana kwa moyo **mtu huamini** ikisababisha uhaki..” Warumi 8:10*

*‘kwa hiyo tu kama matokeo ya kosa moja (dhambi) ilikuwa hukumu ya kila mtu, hivyo pia matokeo ya tendo moja ya uhaki ilikuwa haki ambayo huleta uhai kwa watu wote. Kwa vile vile kwa njia ya kutotii kwa mtu mmoja (Adamu wengi walifanywa watenda dhambi, hivyo pia kupitia kwa **kutii kwa mtummoja** (Yesu) wengi watafanywa wenye **haki**.’ Warumi 5:18-19*

*“Mungu alimfanya yeye (Yesu) ambaye alikuwa hana dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, **ili katika yeye tunawezakuwa uhaki wa Mungu.**” 2 Wakorintho 5:21  
(msisitizo wangu)*

*“mkiwa mmejazwa na matunda ya haki ambayo huja kupitia kwa Yesu Kristo, kwa utukufu na kumtukua Mungu.” Wafilipi 1:11*

*“na labda kupatikana ndani yake, bila kuwa na haki yangu mwenyewe inayotokana na sheria, lakini ile ambayo inapitia kwa Imani katika Kristo, **uhaki** unaokuja **kutoka kwa Mungu** kwa **msingi wa imani.**” Wafilipi 3:9*

### **Tafadhali soma hili:**

Je, umeamini uongo kwamba unafaa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu ili kuwa mwenye haki? Je, umefikiri kwamba ilikuwa juu yako kufanya (au kutofanya) kitu fulani kupata uhaki wa Mungu? Aya hizi tatu (na mengine mengi) zinatuaambia kwamba tulikuwa wenye haki wakati ambapo tuliokolewa. Kwa maneno mengine, uhaki sio kitu ambacho unapata. Ni kitu ambacho unapokea wakati wa wokovu kwa sababu Mungu alikupa wewe utambulisho mpya wa haki.

***UHAKI wako katika Kristo hauna chochote cha kufanya na kile unachofanya au haufanyi. Ni matokeo ya kile Mungu alifanya NDANI yako wakati wa wokovu.***

**Maswali :** Je, umeamini hadi kwa hatua hii kwamba ulipaswa kufanya ( au kutofanya) kitu fulani kupata uhaki wa Mungu? Itaweza kufanya tofuti gani katika maisha yako ikiwa huhitaji kufanya kazi au kujitahidi kuwa mwenye haki?

---

---

**Tafakari :** Juu ya Warumi 5:18 – 19, 2 Korintho 5:21 na Filipi 3:9 na umwombe Mungu akushawishi kwamba wewe ni mwenye haki kwa kuzingatia nini alifanya kwa wokovu.

**Kumhusisha Mungu :** ikiwa unapambana na ukweli wa uhaki wako, muombe Roho Mtakatifu Kukushawishi kwamba uhaki sio kitu ambacho unapata. Badala, ni sehemu ya kazi iliyokamilishwa ambayo Yesu alikamilisha msalabani.

Ni muhimu pia kujua kwamba kwa vile sasa wewe ni mwenye haki katika Kristo, hakuna tena hukumu kutoka kwa Mungu. Hatawahi tena kukuhukumu tena kwa dhambi zako. Zaidi, huhitaji tena kujihukumu. Paulo anathibitisha hii katika Warumi 8:1:

*“kwa hivyo, **hakuna sasa hukumu** kwa wale walio katika **Kristo Yesu.**”*

***Kwa vile sasa wewe ni mwenye haki katika Kristo,  
Mungu HAKUHUKUMU tena, na hihitajitena kujihukumu.***

**Swali:** ikiwa hakuna hukumu na wewe ni mwenye haki, je, unastahili kuendelea kuamini kwamba Mungu atakuhukumu wewe au unapaswa kujihukumu?

**Kumhusisha Mungu:** ikiwa unapambana na hukumu ya kibinafsi, (haswa unapotenda dhambi) muombe Mungu afanye upya akili yako katika Warumi 8:1 na kukuweka wewe huru kutoka kwa hukumu ya kibinafsi.

## **SIKU YA PILI**

### **1. Unao UTAMBULISHO MPYA ( Wewe ni mshiriki wa uumbaji wa Mungu.)**

*“Hivyo basi, ikiwa mtu yeyote yuko katika Kristo, ni **uumbaji mpya**; mambo ya **kale**(utambulisho wa zamani) yalipita; tazama **mambo mapya**( **utambulisho mpya**) yamekuja.” 2 Wakorintho 5:17 (mgodi wa msala)*

***Kuwa na utambulisho mpya ina maanisha kwamba wewe ni MSIRIKI wa uumbaji wa Mungu***

*“kwa maana kwa haya ametupatia ahadi zake za thamani na za ajabu, ili kwa hayo, unaweza kuwa washirika wa uumbaji wa uumbaji wa Mungu...” 2 Petro 1:4*

Mungu alikufanya mshirika wa uumbaji wake kipindi ambapo uliokolewa. ‘mshirika’ katika Ugiriki ina maanisha ‘yule anaye shiriki’. Kwa hivyo, kama matokeo ya umoja wako na Mungu katika roho yako ya mwanadamu, unashiriki sehemu ya asili ya Mungu. Namna nyingine ya kuisema ni kwamba kuna baadhi ya ‘sifa za uungu’ ambayo Mungu anashiriki nawe. Hii haimaanishi kwamba unakuwa na uungu. Ina maanisha kwamba kuna sehemu ya uungu wa Mungu ambayo anashiriki nawe au anakupa wewe.

**Mshiriki wa Divai ki halisi anashiriki na Mungu tabia za Kiungu anayoweka ndani yako kama sehemu ya utambulisho wako mpya.**

### **Utambulisho wako wa kweli katika Kristo.**

***“Kwa maana sisi ni KAZI ya Mungu.....” Waefeso 2:10***

Tunaenda sasa kuangalia kwa baadhi ya sifa za uungu ambayo inaunda utambulisho wako wa kweli katika Kristo. Sijui majibu yako yatakuwa vipi unapopitia orodha ifuatayo. Jawabu langu la kwanza lilikuwa kwamba hii ni nzuri Zaidi kuamini. Ikiwa unahisi namna sawa, tambua kwamba kila kitu kilichoorodheshwa hapa chini ni ukweli ambao wewe ni katika Kristo. Kwa hivyo, ningependa kwa wewe kusoma kupitia somo hili polepole na uache ukweli wa utambulisho wako wa kweli uingie ndani. Unaposoma kupitia orodha hii kumbuka kwamba ‘katika Kristo’ ina maana kwamba wewe ni nani katika utambulisho wako wa kweli. Kwa mfano, unaweza soma kila sifa hivi: ‘Katika utambulisho wangu wa kweli katika Kristo, Mimi ni mshindi.

### **Baadhi ya sifa za utambulisho wako wa Kweli ‘KATIKA’ Kristo**

Warumi 8:35, 38-39	Katika Kristo, napendwa bila ya masharti.
1 Wakorintho 15:57	Katika Kristo, Mimi ni mshindi.
Zaburi 71:5	Katika Kristo, Mimi ni mwenye ujasiri.
Zaburi 56:4	Katika Kristo, Mimi ni bila uoga.
2 Wakorintho 9:8	Katika Kristo, Mimi ni mwenye
Zaburi 139:14	Katika Kristo, Mimi nina thamani.
2 Wakorintho 3:5	Katika Kristo, mimi ni
Warumi 8:37	Katika Kristo, Mimi ni Zaidi ya mshindi.
Waefeso 6:10	Katika Kristo, Nina nguvu.
Zaburi 71:5	Katika Kristo, najiamini.
Warumi 15:7	Katika Kristo, nakubaliwa na mwenye kukubalika.
Waefeso 4:24	Katika Kristo, mimi ni mwenye haki na mtakatifu.
Wakolosai 3:13	Katika Kristo, mimi ni mtu wa kusamehe.
Wakolosai 2:10	Katika Kristo, mimi ni mkamilifu ndani yake.
Wagalatia 5:1	Katika Kristo, niko huru.
Wakolosai 3:12	Katika Kristo, nina huruma, mnyenyekevu, mwema, subira.
Zaburi 139:5	Katika Kristo, nina usalama.



Waefeso 1:1	Katika Kristo, mimi ni mtakatifu. (Ona 1Wakorintho. 1:2; Wafil. 1:1; Wakol.1:2)
Yohana 15:13	Katika Kristo, mimi ni dhabihu.
Wafilipi 2:3	Katika Kristo, mimi ndio wengine wanazingatia.
Wagalatia 5:22, 23	Katika Kristo, ni mwenye furaha, amani, mstahimilivu, mwema, mzuri, mwaminifu, mpole
Warumi 8:17	Katika Kristo, mimi ni mrithi pamoja na Kristo.
Yohana 1:12	Katika Kristo, mimi ni mwana wa Mungu (sehemu ya familia yake)
1 Wakorintho 2:16	Katika Kristo, niko katika umiliki wa akili ya Kristo.
Wagalatia 3:26, 28	Katika Kristo, mimi ni mwana wa Mungu.
Yohana 15:15	Katika Kristo, mimi ni rafiki wa Kristo.
Wakolosai 3:12	Katika Kristo, ni mchaguliwa wa Mungu, mtakatifu, na kupendwa kwa dhiti.
Waibrania 3:14	Katika Kristo, mimi ni mshirika wa Kristo.
1 Petro 2:9, 10	Katika Kristo, mimi ni aina iliyochaguliwa, ukhani wa Kifalme.

**Swali** : Ni zipi baadhi ya sifa zilizoordheshwa hapo juu ambayo hauhisi au kuamini ni kweli yako?

---



---



---

Zoezi: Soma kila ya sifa ya utambulisho wako kwa sauti. Kutoka kwenye orodha hiyo, chagua tano kati ya sifa ambazo ungependa Zaidi kuwa na uzoefu. Angalia aya kwa kila ya sifa hizo.

---



---



---


**Tafakari**: juu ya sifa hizi za utambulisho wako wa kweli.

Kumhusisha Mungu: Anza kumuomba Mungu kufanya upya akili yako kwa ukweli wa nani wewe katika utambulisho wako wa kweli. Hasa muulize akushawishi juu ya ukweli wa andiko wa sifa hizo tano ambazo ungependa Zaidi kupata.

### **Utambulisho Wako wa Kweli na Michoro ya Mviringo**


Kumbuka mchoro hapo chini ambao tulisoma katika somo la pili. Inaonyesha utambulisho wako wa kweli ukiwa umewekwa katika roho yako ya mwanadamu.

## Utambulisho wako wa kweli katika Roho ya mwanadamu



Katika mchoro unaofuata, nimepanua roho ya mwanadamu kuonyesha baadhi ya sifa za utambulisho wako wa kweli kutoka kwenye orodha kwenye ukurasa uliopita.

## Tabia zingine za utambulisho wako mpya katika Kristo



**HOJA MUHIMU YA KUKUMBUKA:**

***Jinsi unavyo HISI au nini wewe UNAAMINI kuhusu ukweli wa utambulisho wako haibadilishi ukweli kwamba ukweli wa Mungu ni UKWELI***

**SIKU YA TATU**

**Kupanua juu ya baadhi ya sifa za Utambulisho wako mpya.**

Kukupa wewe akili bora ya nini utambulisho wako mpya unafanana, hebu tuangalie kwa ukaribu katika sifa chache za utambulisho wako mpya.

**Katika Kristo, UMEKAMILIKA.**

Wakolosai 2:9 – ‘Kwa maana **ndani** yake wa, **ukamilifu Uungu** huishi katika muundo wa mwili’’

Wakolosai 2:10 – ‘**nandaniyake** umefanywa kuwa **mkamilifu**’’

Kabla wokovu sote tulikuwa hatujakamilika. Hata hivyo, kwa wokovu Mungu alitufanya sisi wakamilifu katika Kristo. Yote ya ukamilifu wa Mungu huishi katika Yesu, na Yesu huishi ndani yetu na matokeo kwamba sisi ni Wakamilifu ndani yake. Kwa maneno mengine, hakuna chochote ambacho tunahitaji kuongezea kwa ukamilifu wetu katika Kristo.

**Swali:** Ikiwa unahisi au kuamini kwamba wewe sio mkamilifu, je, hiyo inabadilisha ukweli kwamba wewe ni mkamilifu katika Kristo?

**Katika Kristo umekubaliwa KABISA NA UNAKUBALIKA**

Warumi 15:7 – ‘Kubalianeni, basi, kama vile Kristo alikukubali wewe...’’



Sababu kwa nini Mungu mtakatifu anaweza kutukubali sisi kabisa kwa sababu Ametufanya sisi kukubalika. Unaweza kuhisi au kupata kukataliwa ikija kutoka kwa wengine, lakini hiyo haibadilishi ukweli kwamba unakubaliwa na Mungu bila masharti! Hii in maanisha kwamba hakuna tabia ya kidhambi kubwa Zaidi kusababisha Mungu kukukataa wewe. ( Mungu haukubali tabia ya dhambi, lakini Hakukatai kwa sababu ya tabia yako ya dhambi. Kama matokeo, huhitaji tena kupata (au fanya kwa ajili ya) kukubaliwa na Mungu na kuwa huru

kutokana na kukataliwa na wengine. Kuamini kwamba umekubalika katika Kristo kutakupata wewe uhuru wa kukubali wengine bila ya masharti.

**Maswali** : Kwa vile Mungu anakukubali bila ya masharti, je anaweza kukukataa? Ikiwa kweli unaamini kwamba unakubaliwa katika Kristo, je unastahili kuchukua umiliki wa kukataliwa kokote unaolekezwa kwako na wengine (au na wewe mwenyewe)?

**Kumhusisha Mungu:** ikiwa unapambana na kukataliwa, muombe Roho Mtakatifu kukupa ushawishi kwamba wewe unakubalika kabisa na kwamba huhitaji tena kuchukua umiliki wa kukataliwa kwako kwa mtu mwingine.

### **Katika Kristo uko SALAMA Kabisa.**

*Zaburi 91:14 – ‘Kwa sababu amenipenda mimi; kwa hivyo, nitamtoa, nitamweka salama juu kwa sababu amelijua jina langu.’*

*Ezekieli 24:38 – ‘hawatakuwa tena mawindo kwa mataifa, na wanyama wa dunia hawatawaangamiza; lakini wataishi kwa **usalama**, na hakuna atakaye waogofya.*

Unahisi nini bila usalama kuhusu? Je, ni kazi yako?, ndoa yako, au zile tu hisia za bila usalama ambazo unazo kukuhusu mwenyewe? Huhitaji tena kuhisi namna hiyo kwa sababu katika Kristo uko na usalama kabisa. Je, unajaribu kupata usalama katika kitu au mtu mwingine kando na Mungu? Ukweli ni kwamba ukweli wetu pekee wa kweli uko katika Kristo. Kwa kuwa yeye ni mkuu na ndiye pekee ambaye yuko katika udhibitikweli, tunaweza kuishi kutoka kwa usalama wetu ndani yake.

**Maswali** : Ni matukio gani au mahusiano katika maisha yako zinakufanya uhisi bila usalama? Itafanya tofauti gani katika hali hizo ikiwa kweli unaamini uko na usalama katika Kristo?

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akupe ufunuo nini au nani unaweka usalama wako ndani yake badala ya Mungu. Mtafute yeye kufanya upya akili yako kwa ukweli kwamba usalama wako uko tu ndani Yake.

(Mungu wakati mwingine ataruhusu vitu tunavyoweka usalama wetu ndani yake kuondolewa ili tuweze kutambua kwamba usalama wetu tu uko ndani yake)

### **Katika Kristo wewe ni mwenye NGUVU**

*Waefeso 5:10 – ‘Hatimaye, kuwa mwenye nguvu katika Bwanana katika nguvu ya uwezowake.’*

Sisi sote tuna nguvu za ndani, nguvu ya kimwili, na nguvu ya kiakili. Tunazoea kutumia nguvu zetu kusuluhisha au kushughulikia maswala ya maisha. Hata hivyo, matukio, hali, na mahusiano hutuibia hizo nguvu za kibinadamu. Mungu huruhusu matukio katika maisha yetu kutupa ufunuo kwamba nguvu zetu za kibinadamu hazilinganishwi na nguvu ya dhambi, mwili, au shetani. Anatumkumbusha sisi kupitia kwa matukio haya kwamba nguvu isiyo ya kawaida anatupea sisi katika utambulisho wetu wa kweli haiwezi kamwe kushindwa au kushinda. Paulo alikuja kutambua kwamba nguvu zake za kibinadamu zilikuwa tu udhaifu katika 2 Korintho 12:8 – 10.

**Maswali** : ni baadhi ya vitu gani ambavyo vinaweza kukuibia wewe nguvu yako ya kimwili, kiakili, nay a ndani? Je, unafikiri itaonekana vipi katika maisha yako kuishi kutokana na nguvu ya Kristo?

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akufunulie wewe jinsi unajaribu kutumia nguvu yako mwenyewe ya ndani au kiakili kukabiliana na mapambano au maswala katika maisha yako ambayo yanaweza kushughulikiwa kikweli katika nguvu za Mungu. Mtafute yeye akupe ufunuo wa ndani Zaidi na tamaa ya kuacha kuamini nguvu zako mwenyewe na uishi kutoka kwa nguvu zake.

### **Katika Kristo wewe ni wa KUTOSHA kabisa.**

2 Korintho 3:5 – ‘sio kwamba hatuna uwezo wa kuzingatia kitu chochote kinachokuja kutoka kwetu, lakini ufanisi wetu ni kutoka kwa Mungu.

Waumini wengi huhisi au kuamini kwamba hawana thamani na/ au hawatoshi. Tunajiangalia, na hatuwezi kufikia viwango vya dunia vya utoshelezi/ thamani. Tunaweza kutafuta kutosha kwetu na thamani katika mahusiano, kazi, au katika ‘vitu’ hata hivyo, hii kamwe haitatuletea utoshelezi au thamani ambao tunaweza tu kupata tu katika Kristo. Hii hapa habari njema. Kuamini na kuishi kutoka kwa kutosha kwako katika Kristo hukuondolea wewe shinikizo la kujaribu kutafuta kutosha kwako katika mtu au kitu kingine.

**Maswali:** Hata kama unahisi au unaamini kwamba wewe sio wa kutosha, je, hiyo inabadilisha ukweli kwamba wewe ni wa kutosha kabisa katika Kristo? Unaamini itabadilisha vipi tabia yako ikiwa kweli utaamini kwamba unatosha katika Kristo?

Kumhusisha Mungu: ikiwa unapambana na utoshelezi, anza kuaminisha kutotosha kwako kwa Mungu na chukua hatua ya Imani kwa yeye kufanya upya akili yako kwa ukweli kwamba unatosha kabisa katika utambulisho wako mpya.

### **Katika Kristo unapendwa bila MASHARTI.**

**1 Yohana 4:16-** “na tumekuja kujua na tumeamini upendo ambao Mungu ako nao kwa ajili yetu. **Mungu ni Upendo..**”

1 Yohana 3:1 – “tazama **jinsi mkuu upendo ambao baba ametupa, kwamba tutaitwa watoto wa Mungu.**

Warumi 8:38, 39 – “kwa maana nina hakika kwamba hakuna kifo, wala uzima, wala malaika, wala mamlaka, wala vitu vilivyopo, wala vitu vijavyo, wala nguvu, wala urefu, wala kina, wala kitu chochote kilichoumbwa **kitaweza kututenganisha na upendo wa Mungu, ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.**”

Huhitaji tena kuamini kwamba wewe hupendwi kwa sababu Mungu anakupenda bila kipimo, milele, na bila masharti. Ni kiini chake cha kufanya hivyo! Hana tamaa kubwa Zaidi ya kukupenda wewe kwa sababu ya yeye nani. Kwa kuongezea, Warumi 8:38 – 39 inaonyesha dhahiri kuwa hakuna chochote kinachoweza kuwatenganisha na upendo wake. Hakuna chochote ambacho wewe unaweza kufanya ambacho kitabadilisha mtiririko wa upendo wa kuendelea wa Mungu kwa ajili yenu.

Upendo wa Mungu hautegemei wewe ni nani au juu ya kile ulichofanya au hukufanya. Inazingatia tu juu ya yeye ni nani. Kwa vile Mungu ni upendo, na yuko ndani yako, basi unamilki upendo wote wa Mungu. Huwezi tu kupokea upendo wa Mungu usio na masharti pekee, lakini pia unaweza kuruhusu upendo wa Mungu kupitia kwako hadi kwa wengine.

**Maswali :** Ikiwa hauhisi au kupata upendo wa Mungu usio na masharti, je, hiyo inabadili ukweli yeye anakupenda? Itabadilishaje mtazamo wako kwa Mungu ikiwa unaamini kwa kweli kwamba hakuna chochote ambacho unaweza kufanya (au kutofanya) kubadilisha upendo wake kwa ajili yako?

**Tafakari** : juu ya aya ya sifa zako nne za utambulisho wako mpya katika sehemu hii.

Kumhusisha Mungu: ikiwa unapambana kwa kiwango Fulani kuhusu upendo wa Mungu, mtafute kupitia hatua za Imani kuondoa Imani zako za uongo kwa ukweli kwamba anakupenda milele, bila kipimo, na bila masharti.

## **SIKU YA NNE**

### **Katika Kristo wewe ni MSHINDI Na Zaidi Ya Mshindi.**

1 Korintho 15:57 – “lakini shukrani iwe kwa Mungu, ambaye hutupa ushindi kupitia ..Kristo.”

Warumi 8:37 – “Lakini katika vitu vyote hivi sisi hushinda kupitia Yeye aliyetupenda.”



Unaweza kujiona mwenyewe kama mshindwa, lakini katika Kristo wewe ni mshindi na mshindi. Hakuna tatizo, mgogoro, au shida ambazo Kristo hawezi kushinda kupitia kwako. kwenye mkono mwingine, unaweza kujiona mwenyewe kama “Kujitoshia mwenyewe”, mshindi au mshindi katika maisha kando na Kristo. Kwa kuwa ukweli ni kwamba mbali na Mungu huwezi kufanya **chochote**( Yohana 15:5) Mungu anakupenda wewe ya kutosha kwamba ataleta hali zisizowezekana (au mahusiano) katika maisha yako kukufunulia kutokuwa na uwezo kwako kushinda hali hizo. Kutambua udhaifu wako na kutokuwa na uwezo wa kutatua hali utakugeza kwenye utegemezi juu ya Mungu na kumruhusu kuwa mshindi kupitia kwako. kwa hivyo, anza kuishi kutoka kwa ushindi katika Kristo katika utambulisho wako wa kweli.

**Maswali** : ikiwa unahisi kama mshindwa, je, hiyo inabadilisha ukweli kwamba katika Kristo wewe ni Zaidi ya mshindi? Ikiwa katika Kristo wewe ni mshindi, je unahitaji kujitahidi kuwa mshindi?

**Kumhusisha Mungu** : Angalia katika maeneo ambapo unafikiri kwamba unashindwa katika maisha. Katika maeneo hayo, muombe Mungu akupe ufunuo wa jinsi inavyoonekana kutembea kwa ushindi katika maeneo hayo.

### **Katika Kristo uko HURU**

Wagalatia 5:1 “ni kwa ajili ya uhuru kwamba **Kristo ametuweka sisi huru**. Simameni imara, basi, na msiache nafsi zenu kuwa na mzigo tena kwa jukumu la utumwa.”

Warumi 8:2– “ kwa maana nguvu ya roho ya kupeana maisha **imekuachilia huru kupitia Yesu Kristo** kutoka kwa nguvu ya dhambi ambayo huongoza kwa kifo.

Chukua mtazamo wa ukaribu kwa Galatia 5:1 inasema kwamba umewekwa huru. Ni wakati uliopita. Ni tendo lililokamilika. Uhuru wako ulipata ushindi kwenye msalaba. Kama matokeo, katika Kristo uko huru kutoka kwa nguvu ya dhambi, tabia yako ya kimwili, kutoka kwa uhalali, na kutoka kwa ngome zako za dhambi zisizoshindwa. Pia uko huru kutoka kwa mshiko wa dunia na nguvu ya shetani. Kwa maneno mengine, huhitaji kuishi tena kana kwamba bado uko kwa utumwa kwa vitu hivyo kwa sababu ukweli ni kwamba umewekwa huru kutokana nazo.

**Swali:** hata kama huenda hauhisi uhuru katika eneo Fulani ya maisha yako, je inabadilisha ukweli kwamba umewekwa huru?

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akushawishi kwamba hata kama huenda usihisi huru kutoka kwa nguvu ya dhambi, tabia ya kimwili, mfumo wa dhambi usioshindwa, n.k kwamba umewekwa huru.

**Kumhusisha Mungu:** muombe Mungu akuongoze hata ingawa haujisikii huru kutoka kwa nguvu ya dhambi, tabia za kimwili, mbinu ya kushinda dhambi. Kwamba umewekwa huru.

### **Katika Kristo, uko na AKILI YA KRISTO.**

1 Korintho 2:16 b – “...tunayo akili ya Kristo.”

Inamaanisha nini kwamba uko na akili ya Kristo? Ina maana kwamba huhitaji tena kutegemea hekima yako ndogo na kamilifu, ufahamu, ufahamu kujaribu na kutambua maisha. Kwa kila hali ambayo unakabiliana nayo, unaweza kuteka juu ya ujuzi wa Kristo usio kamilika, hekima, kuelewa, na kufahamu.

**Swali:** Inaweza kuwa kwamba Mungu huruhusu hali ngumu katika maisha yako ili uweze kuona uhitaji wako kuteka kwake kama chanzo chako kwa hekima, ufahamu na uelewa? Ni nini hali ambazo unakabiliana nazo leo ambazo unahitaji akili ya Kristo?

**Kumhusisha Mungu:** katika hali hizo, muombe Mungu akuzuie kuendelea kuteka juu ya hekima yako ndogo, ufahamu au ufahamu na kuanza kuteka juu ya yake.

### **Katika Kristo wewe ni MTAKATIFU**

Wakolosai 1:12 – “*kupeana shukrani kwa Baba, ambaye amekustahili kushiriki katika urithi wa watakatifu katika ufalme wa nuru.*”

Waumini wengi ninao wajua hujitambulisha wewe kama watenda dhambi. Kwa nini? Kwa sababu wanaamini tabia yao ya kidhambi huamua utambulisho wao wa kweli. Hata hivyo, kwa vile wewe u mtakatifu, huhitaji tena kujitambua kama mtenda dhambi. Kwa nini? Mungu anasema mara kwa mara katika neno lake kwamba wewe ni mtakatifu. Hii Haimaanishi kwamba kamwe hutatenda dhambi tena. Inamaanisha kwamba katika macho ya Mungu utambulisho wako hauamuliwi tena na tabia yako ya kidhambi. Unaweza kuisema kwa njia hii: katika utambulisho wako wa kweli, wewe si mtenda dhambi tena. Badala, wewe ni mtakatifu ambaye wakati mwingine hutenda dhambi. Kwa vile dhambi yako yote imeondolewa

na Mungu hakumbuki dhambi yako tena (Isaya 43:25), basi jua kwa ujasiri kwamba Mungu hakuoni tena kama mtenda dhambi.

**Swali:** itabadilisha vipi jinsi unavyofikiri ikiwa utajiona kama mtakatifu ambaye wakati mwingine hutenda dhambi badala ya mtenda dhambi?

**Kumhusisha Mungu:** muombe Mungu aanze kukushawishi kwamba utambulisho wako sio tena kwamba wewe ni mtenda dhambi. Mtafute yeye akufunulie kwamba wewe ni mtakatifu hata kama tabia yako huenda isiwe daima ya “kitakatifu”

### **Katika Kristo wewe ni mtu wa KUSAMEHE.**

Efeso 4:32 – “kuweni na wema kwa kila mmoja, mioyo laini, **kusameheana**, kama vile tu Mungu katika Kristo amewasamehe nyinyi.”



Huenda ukawa umekosewa na mtu mwengine, na hauhisi kwamba unapaswa kumsamehe (au unaamini kwamba una haki ya kutokusamehe). Ukweli ni kwamba hauna kisingizio cha kuto samehe wengine. Kwa nini? Ni kwa sababu katika utambulisho wako wa kweli wewe ni mtu wa kusamehe. Iwe wajisikia au la, si shida. Unaweza **kuchagua** kusamehe kwa sababu huo ni utambulisho wako wa kweli katika Kristo. Ikiwa hutaki kusamehe, muombe Mungu aongoze moyo wako kuwa tayari kusamehe.

**Maswali:** Je, kuna mtu katika maisha yako ambaye huhisi kama kumsamehe? Kwa kuwa wewe ni mtu wa kusamehe katika Kristo, je, bado una haki kutomsamehe mtu huyo?

**Kumhusisha Mungu :** ikiwa unapambana na kusamehe mtu Fulani, anza kuaminisha kutosamehe kwako kwa Mungu na kumtafuta kwa bidii kuimarisha akili yako kwa kweli kwamba wewe ni mtu mwenye kusamehe na kukuweka huru kutokana na mtazamo wako usio wa kusamehe.

## **SIKU YA TANO**

### **Kutofautisha Kuishi Kutoka Sifa za Kibinadamu Dhidi ya Kuishi Kutokana na Utambulisho Wako Mpya Katika Kristo**

Nahisi kwamba inaweza kuwa na usaidizi kwa hatua hii ya utafiti kuchora tofauti kati ya kuishi kutokana na sifa za kibinadamu dhidi ya kuishi kutoka kwa sifa za Mungu za utambulisho wetu mpya katika Kristo.

**Nguvu za binadamu** – ni nguvu ya mwanadamu ya sifa iliyo na changamoto na udhaifu.

**Nguvu ya Kristo** – haina changamoto au udhaifu



**Kujiamin kwa binadamu** – ina changamoto kiasi kwamba kuna watu au hali zinazoweza kuibia mtu kujiamini kwa binadamu

**Kujiamini kwa Kristo** – haina changamoto na haiwezi kuathiriwa na hali au watu.

**Kutohofu kwa binadamu** – ni udanganyifu kwa sababu kila mtu ana kitu kimoja au vitu Zaidi ambazo wanahofia.

**Kutohofu kwa Kristo** – ina maanisha kwamba hupaswi kuwa na hofu katika hali yoyote.

**Udhibiti wa mwanadamu** – pia ni udanganyifu. Mwanadamu ana udhibiti mdogo sana juu ya hali, uhusiano, na hata maisha yake mwenyewe.

**Udhibiti wa Kristo** – hukuweka mbali na kutenda dhambi na kukuweka kwenye kupumzika kwa kujua kwamba Mungu yuko katika udhibiti.

**Kukubalika kwa mwanadamu** – inazingatia juu ya nini wengine wanafikiri kukuhusu wewe. Unaweza kukataliwa na wengine.

**Kukubaliwa kwa Kristo** – ina maanisha kwamba hauchukui umiliki wa kukataliwa na wengine kwa sababu ya kukubalika kwako bila masharti katika Kristo.

**Tafakari** : Muombe Mungu kufafanua kwa akili yako tofauti kati ya sifa za kuwa mwanadamu dhidi ya kuwa mwanadamu anayeishi kutoka kwa utambulisho wake mpya katika Kristo.

**Kumhusisha Mungu**: Muombe Mungu akuonyeshe pale unapoishi kutoka kwa sifa zako za kibinadamu dhidi ya utambulisho wako wa kweli katika Kristo. Muombe akuondoe kutoka kuishi kwa sifa zako za mwanadamu hadi kuishi kutoka kwa utambulisho wako wa kweli.

## **Vitu Viwili Muhimu Kukumbuka Kuhusu Utambulisho Wako Wa Kweli.**

### **#1 – TABIA Yako Haiamui Utambulisho Wako Katika Kristo.**

Hii ni swali ambalo unaweza kuwa wauliza. “Hata kama ukweli wa Mungu unasema kwamba mimi ni mwenye haki, kukubaliwa, mwenye kusamehe, nk, mitazamo yangu na/au tabia yaweza tu kuniambia kinyume. Ipi ni kweli, kile tabia yangu inaniambia, au kile Mungu ananiambia ni kweli juu yangu?”

Hata kama tabia yako huenda isiwe daima kwenye safu na kile Mungu anasema ni kweli kukuhusu, je inabadilisha ukweli wa utambulisho wako katika Kristo? Jawabu ni LA! Kama waumini, Mungu amewapa, katika roho zenu za binadamu, utambulisho mpya ambayo iko kando nambali na tabia yako ya kutenda dhambi. Kabla ya wokovu, kile ulichoamini na tabia yako ilifunua utambulisho wako.

Hata hivyo, sasa kwa vile utambulisho wako mpya ni sehemu ya asili ya Mungu ndani yako, tabia yako ya kutenda dhambi ya kimwili haiamui tena wewe hasa ni NANI. Haifanyi tofauti yoyote ikiwa mimi ni Loveless mzuri au Loveless mbaya; tabia yangu haibadilishi utambulisho wangu kama Loveless. Katika njia sawa, utambulisho wako katika Kristo hubaki bila kubadilika kwa tabia yako.

Hebu tuangalie kwenye baadhi ya mifano:

**Mfano #1:** - Hata kama huenda ukachagua tabia ya kimwili na kutenda tendo lisilo la haki la kuwa wa umuhimu na kuhukumu, haibadilishi ukweli katika utambulisho wako ndani ya Kristo wewe ni mwenye haki

**Mfano #2:** - tabia yako ya kutenda dhambi inaweza kukuongoza kwa mtazamo wa kutosamehe kwa mwenzi wako ambaye amekukosea. Hii haibadilishi ukweli kwamba kwa vile wewe nit u mwenye kusamehe katika Kristo, unaweza kusamehe.

Je, ukweli kwamba tabia yako ya kimwili hai amui utambulisho wako unakupa leseni ya kuishi kutoka kwa tabia yako ya kimwili? Bila shaka hapana. Mungu kamwe haridhishwi na dhambi yako katika muundo wowote. Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kwamba kwa sababu ya kile Mungu amefanya katika kukupa wewe utambulisho mpya, uko na uchaguzi wa kutoishi tena kutoka kwa tabia yako ya kutenda dhambi.

**Maswali:** Ni zipi baadhi ya mitazamo/tabia ya kidhambi ambayo inapinga utambulisho wako katika Kristo? Ni vipi tabia hizo za kutenda dhambi zinaathiri nini unafikiri kuhusu wewe mwenyewe? Unafikiri itaweza kukuathiri vipi ikiwa utaamini ukweli wa Mungu kuhusu utambulisho wako mpya juu ya tabia yako ya kutenda dhambi?

---

---

---

**Kutafakari:** Juu ya ukweli kwamba tabia yako haiamui utambulisho wako.

**Kumhusisha Mungu:** ikiwa unapambana na ukweli kwamba utambulisho wako unazingatia tabia yako, basi mwombe Mungu afanye upya akili yako kwa ukweli kwamba tabia yako ya dhambi haiamui utambulisho wako.

***Kama Mkristo, tabia yako ya dhambi, kimwili  
Haiamui utambulisho wako katika Kristo.  
Kile MUNGU ANASEMA juu yako huamua utambulisho wako.***

## **#2- Imani zako za UONGO Na Hisia Haiamui Utambulisho Wako Katika Kristo**

Hata kama Mungu amekupa utambulisho mpya katika roho yako ya mwanadamu, utakuwa na imani za uongo na hisia hasi kuhusu wewe mwenyewe. Ni muhimu kuelewa kwamba imani zako za uongo au hisia hasi kuhusu wewe mwenyewe haibadilishi ukweli wa wewe ni nani katika Kristo. Kwa maneno mengine, Imani za uongo ambazo unaamini au hisia hasi ambazo unahisi haibadilishi ukweli wa utambulisho wako mpya katika Kristo.

Hebu tuangalie kwenye baadhi ya mifano:

**Imani ya Uongo Au Hisia**

**Ukweli Wa Utambulisho Wako Mpya Katika Kristo**

Unahisi/ kuamini umekataliwa

Umekubaliwa na unakubalika katika Kristo.

(Warumi 15:7)

Unaamini kwamba unajitoshia

Kutosha kwako kunaweza tu kupatikana katika Kristo.

(2 Wakorintho 9:8)

Huhisi kama kusamehe

Wewe ni mtu wa kusamehe katika Kristo.

(Waefeso 4:32)

Huhisi kupendwa bila masharti na

Mungu anakupenda bila masharti (1 Yohana 4:16)

---

***Imani zako za uongo na / au hisia zako hasi***

***HAIAMUI utambulisho wako wa kweli.***

***Kile Mungu anasema ni kweli kukuhusu ni utambulisho wako wa KWELI***

Labda hadi sasa Imani zako za uongo na hisia hasi imekuwa ndio ukweli kwako. Hata hivyo, kwa vile sasa unaelewa kwa kiakili kwamba Mungu amekupa wewe utambulisho mpya, anataka wewe kuamini ukweli wake kinyume na nini hisia zako hasi na Imani za uongo zinakuambia.

Tafakari : Juu ya ukweli kwamba Imani zako za uongo na hisia hasi haiamui utambulisho wako wa kweli.

Kumhusisha Mungu: Anza kuchukua hatua za Imani ili Mungu akushawishi wewe juu ya utambulisho wako wa kweli hata kama unazo Imani za uongo na/au hisia kuhusu wewe mwenyewe.

**Muhtasari.**

Naamini kwamba Mungu ametumia kweli katika utafiti huu kukupa wewe ufahamu wa ndani Zaidi katika kuunda utambulisho wako na kwamba utamruhusu yeye kukushawishi juu ya utambulisho wako wa KWELI katika Kristo. Maswali mawili ambayo huenda ukawa wauliza kwa hatua hii ni “ Najua kwamba niko na utambulisho mpya, lakini mbona bado nachagua kuishi kutoka kwa Imani zangu za uongo?” na “ ni vipi nitaondoka kutoka kuishi kutoka kwa ukweli wa Mungu dhidi ya Imani zangu za uongo?” Tutazuru majibu kwa maswali hayo katika somo linalofuata.

## Somo La Nne

### **Mchakato Wa Mungu Wa Kukubadilisha Wewe Kuishi Kutoka Kwa Utambulisho Wako Wa Kweli**

#### **SIKU YA KWANZA**

##### Utangulizi

Natumai kwamba ulitiwa moyo uliposoma katika somo lilipita kuhusu utambulisho wako wa kweli. Kwa hatua hii katika utafiti, watu kawaida huniuliza maswali yafuatayo:

- Sasa najua kwamba nina utambulisho mpya, lakini kwa nini bado nachagua kuishi kutoka kwa Imani yangu ya uongo?”
- Ninapata vipi na kuishi kutoka kwa utambulisho wangu wa kweli?

Haya ni maswali mawili ambayo tutakuwa tunayajibu katika somo hili. Hebu tuanze kwa kujibu swali la kwanza. za U

#### **Kwa Nini Bado Nachagua Kuishi Kutokana Na Imani Zangu Za Uongo?**




Hii ni swali muhimu kwa sababu jawabu kwa swali hili hufunua kwa njia ya undani kwa nini tunapaswa kutofautisha moyo kutoka kwa roho ya mwaanadamu. Kumbuka kutoka somo la pili kwamba Mungu aliondo roho yako ya mwanadamu ya zamani na utambulisho wako wa zamani na kukupa wewe roho mpya kabisa ya mwanadamu na utambulisho mpya. Tatizo ni kwamba hata kama unamiliki utambulisho mpya katika roho mpya ya mwanadamu, moyo wako unahitaji kubadilishwa kwa mahali ambapo unapata uzoefu na kuishi kutoka kwa sifa za utambulisho wako mpya dhidi ya kuishi kutoka kwa Imani zako za uongo. Hebu nifafanue.

Kumbuka muundo wa moyo wako. Imeundwa kwa akili yako, hisia, na mapenzi. Hebu tuangalie katika hali ya akili, hisia, na mapenzi kabla ya kubadilishwa.

- **AKILI** – bado ina Imani za uongo kuhusu wewe mwenyewe.
- **HISIA** – zimefungwa kwa Imani zako za uongo kuhusu wewe mwenyewe zinakuwa hisia zilizoharibiwa.
- **MAPENZI** – inachagua kuishi kutoka kwa Imani zako za uongo.
- **TABIA ZA KIMWILI** – ni matokeo ya kuchagua kuishi kutoka kwa Imani zako za uongo.


Mchoro kwenye ukurasa ufuatao unatofautisha tofauti kati ya hali ya moyo na hali ya roho ya mwanadamu.



**Hata kama unao utambulisho MPYA katika utambulisho wako MPYA katika ROHO YAKO YA MWANADAMU, MOYO wako ni ile sehemu yako ambayo bado inahitaji KUBADILISHWA**

Hebu tueleze Zaidi katika hali ya akili, hisia na mapenzi kabla ya kubadilishwa.

## **Akili yako inayo imani za uwongo kukuhusu**



### **AKILI – ina Imani za uwongo kuhusu wewe mwenyewe.**

*“Usifanane na dunia hii, lakini badilishwa kwa kufanywa upya AKILI yako...”*

Je, unakubaliana na kauli hii? Kile unafikiri kuhusu wewe mwenyewe ndicho unacho amini kuhusu wewe mwenyewe? Kwa mfano, ikiwa unafikiri kwamba hauna usalama na kutosha, je unaamini kwamba wewe huna usalama na utoshelezi? Hoja ni kwamba kufikiri na kuamini huenda pamoja. Kwa sababu kufikiria kwako na Imani ziko katika akili

yako, basi kile Mungu anataka kufanya na Imani zako za uwongo ni kufanya upya akili yako ili kufikiria kwako na Imani ziambatane na ukweli wa utambulisho wako wa kweli.

Tukitumia mfano wetu hapo juu, Mungu anataka kufanya upya akili yako kwa ukweli kwamba katika utambulisho wako wa kweli una usalama kabisa na unatosha. Anapofanya upya akili yako kwa kweli hizi basi utanza kufikiri na kuamini ukweli kinyume na Imani ya uwongo. Fikiria kuhusu kauli inayofuata:

***Kile UNAFIKIRI na KUAMINI kuhusu wewe mwenyewe ni kweli KWAKO hata kama huenda isiambatane na ukweli wa utambulisho wako.***

Hivyo basi, kile Mungu anataka kufanya ni kutumia Ukweli wake kufanya upya akili yako nia kukuachilia huru kutoka kwa Imani yako ya uwongo. Kumbuka kile tumejadili kabla ni kwamba **kujua** ukweli na **kuamini** ukweli ni maswala mawili tofauti. Sasa unajua uko na utambulisho mpya. Swali ni, Je , kweli unaamini? Unapotafuta Roho kufanya upya akili yako, atakuchukua kutoka kujua ukweli hadi kuamini ukweli kwamba uko na utambulisho mpya.

***Mungu anataka KUUPYA akili yako kwa ukweli wa utambulisho wako mpya ili IMANI zako kuhusu wewe mwenyewe zitaambatana na utambulisho wako wa kweli.***

Ushuhuda wa kibinafsi : kumbuka kwamba nilishiriki kwamba nilikuwa na ngome za hofu na kukataliwa. Zilikuwa kweli halisi zenye nguvu kwangu kwamba katika mwanzo niliposoma kwa neno la Mungu kwamba katika utambulisho wangu wa kweli mimi sina hofu na kukubalika. Sikuamini kuwa vitu hivyo vilikuwa kweli yangu. Hata hivyo, ukweli kwamba sikuamini ukweli wa Mungu kwa wakati huo

haukubadilisha ukweli kwamaba ilikuwa ukweli. Mungu alipoanza kufanya upya akili yangu kwa ukweli wake, nilianza kuamini kwamba mimi sina hofu na ninakubalika.

**Zoezi:** rudi nyuma katika orodha ya sifa za utambulisho wako wa kwelikatika somo la Tatu na tia alama katika sifa hizo ambazo unajua ni kweli lakini ambazo kweli huamini ni kweli juu yako. Kasha jiulize swali hili. Je, kutoamini kwako kuhusu utambulisho wako wa kweli unabadilisha ukweli kwamba kile Mungu anasema ni kweli juu yako hasa ni ukweli?

**Tafakari:** juu ya Warumi 12:2

**Kumhusisha Mungu:** Anza kuaminisha Imani zako za uongo kwa Mungu na muombe afanye upya akili yako kwa ukweli Wake.

Mfano : “Bwana, naaminisha Imani ya uongo kwamba mimi sio mtu wa kutosha na kukuomba wewe ku upya akili yangu kwa ukweli kwamba mimi ni wa kutosha kabisa katika utambulisho wangu wa kweli.”

Mfano : “ Bwana, naamini kwamba mimi ni mtu wa kujiamni. Fanya upya akili yako kwa ukweli kwamba mimi ni Mjasiri katika Kristo, sio mtu mwenye kujiamini’

## **SIKU YA PILI**

### **HISIA – Zina haribika wakati zinapofungwa kwa imani zako za uongo.**

Hisia ni sehemu ya muundo wetu wa mwanadamu. Hisia huwa chanya au hasi. Hata hivyo, hisia/hisia yaweza ‘kuharibika’ zinapo ambatana na kuimarisha imani zako za uongo kuhusu wewe mwenyewe.

***Hisia zinazofUNGWA kwa imani yako ya uongo hukuwa kile ninachoita hisia***

***“ZILIZOHARIBIKA”***

Kama mawazo, hisia zaweza kuwa sehemu muhimu ya kuunda imani yako. Mapema katika maisha tulianza kuhisi namna Fulani kuhusu sisi wenyewe. (yaani kutotosha, bila usalama, kujiamini, n.k) ikiwa hisia hizi zitaendelea na kuanza kujishikisha kwa imani zetu za kutotosha, bila usalama, au kujiamini basi hisia zetu zitaanza kuimarisha imani zetu za uongo. Wakati hii inatokea basi “nahisi’ huwa ‘mimi’”. Wakati hisia zako zinaimarisha imani zako za uongo zinakuwa ‘zimeharibiak’



Kwa mfano, hebu tufhani kwamba uko na hisia za kuendelea za kutokuwa na usalama. Hebu tudhani pia uko na imani ya uongo kuwa wewe ni mtu asiye na usalama. Hisia hizi zinapoendelea, kasha zinaanza kuimarisha imani yako ya uongo hadi kwa hatua ambapo ‘nahisi kutokuwa na usalama’ ni sawa na kusema ‘mimi sina usalama.’ Kutoka hapo kuendelea, kila wakati ukiwa na hisia za kutokuwa na usalama zinaendelea kuimarisha imani ya uongo kwamba huna usalama. Kwa maneno mengine, ‘nahisi’ huja kuwa kitu sawa kama ‘mimi’

*Hisia za KUHARIBIKA hutokea wakati*

*‘NAHISI’ huimarisha imani zetu za uongo kwamba “MIMI NI.”*

## **Uponyaji wa hisia zako za kuharibika**

*“Yeye huponya waliovunjika mioyo na kufunga majeraha yao.” Zaburi 147:3*

Mungu anaahidi kuponya hisia zako zilizo haribika kulingana na Zaburi 147:3. Mungu anapofanya upya akili yako kwa ukweli wa utambulisho wako wa kweli, italeta matokeo ya uponyaji wa hisia zako zilizo haribika. Hii inafanya kazi vipi? Mungu anapoondoa imani zako za uongo kwa ukweli wa utambulisho wako wa kweli, basi hizo hisia zilizoharibika zinazohusiana na imani zako za uongo haziwezi tena kujiimarisha kwenye imani ya uongo kwa sababu sasa unaamini ukweli. Hii haimanishi kwamba hutakuwa na hisia hizo zikija kutoka wakati kwa wakati. Hata hivyo, tofauti itakuwa kwamba hisia hizo zilizo haribika hazitakuchukua tena moja kwa moja kutoka ‘nahisi’ hadi ‘mimi’



Kwa hatua Fulani katika mchakato wa mabadiliko, hisia hizo zilizo haribika hzitakuwa tena mshiko kwa moyo wako kwa sababu ukweli wa utambulisho wako wa kweli utakuwa ukweli mkubwa kuliko hisia zako. Njia nyingine ya kuisema wakati hisia hizo zikitokea ni ‘kwa sababu naamini ukweli wa utambulisho wangu wa kweli nachagua kutoruhusu hisia hizo kuamua utambulisho wangu tena.”

Kwa mfano unaweza kuwa na imani ya uongo kwamba wewe ni mtu mwenye kujitoshia. Kila wakati unapohisi kutosha inaimarisha imani yako



ya uongo kwamba wewe ni wa kujitosha. Unapomtafuta Mungu ku upya akili yako kwa ukweli kwamba

Utoshelezi wako unaweza tu kupatikana katika Kristo. (2 Korintho 9:8), basi wakati hisia hizo za kujitosha zikitokezautajikuta mwenyewe hauchukui tena umiliki wa hisia hizo. (Kumbuka : mapema katika mchakato huu wa kubadilishwa utachukua umiliki wa hisia hizo mara nyingi) hata hivyo, baada ya muda, unapoanza kuamini unajitosha katika Kristo, basi hisia zako za utoshelezi katika Kristo zitazidi hisia zako za kujitosha. Hisia zako za kujitosha hazitawahi kuondoka kabisa lakini unapobadilishwa hazitawahi kukuchukua kukota ‘nahisi’ hadi ‘mimi’

Nahisi uhitaji kusisitiza mara moja Zaidi kwamba uponyaji wa hisia zetu zilizoharibika ni MCHAKATO. Uponyaji utakuja kwa muongezeko unapoendelea kutafuta Roho kubadilisha uongo kwa ukweli. Hoja moja ya mwisho. Uponyaji wa baadhi ya hisia zako zilizo haribika utachukua muda Zaidi ya zingine kwa sababu ya kiwango cha nguvu ambayo zinazo kwako.

***HISIA ambazo uko nazo kuhusu wewe mwenyewe ambazo zinapinzana kwa ukweli wa utambulisho wako mpya itabadilishwa unapoamini ukweli.***

**Zoezi** : andika chini baadhi ya hisia zako zilizo haribika ambazo uko nazo ambazo zimefungika kwa imani yako ya uongo. Kwa mfano, ‘nahisi kutokusamehe’ kumefungika kwa imani kwamba ‘mimi ni mtu mwenye kutosamehe’. Unaweza kutaka kurejelea kwenye mchoro katika ukurasa 19.

---

**Tafakari**: juu ya Zaburi 147:3

Kumhusisha Mungu: Ukitumia kile ulichoandika chini hapo juu, anza kumwomba Mungu kuponya hisia zako zilizoharibika.

## **SIKU YA TATU**

**MAPENZI – ni kufanya uchaguzi kwa kuzingatia imani zako za uongo.**

Kama tulivyojadili kabla, kutoka kwa mapenzi yako unafanya uchaguzi wako. Inakuja kwa utambulisho wako, mapenzi yana machaguzi mawili. Unachagua kuishi kutoka kwa utambulisho wako wa kweli au unachagua kuishi kutoka kwa imani zako za uongo. Chaguo lipi unafanya itaamua ikiwa unakaa katika utumwa kwa uongo au kuwekwa huru kutoka kwa ukweli.

Kwa kuongezea, tunahitaji kuelewa mapenzi yamefungwa kwa kile unachoamini na jinsi unavyohisi. Kuhusu utambulisho wako, angalia ukweli huu muhimu.

**MAPENZI yako hufanya UCHAGUZI kwa kuzingatia nini UNAAMINI  
au jinsi UNAHISI kuhusu wewe mwenyewe.**

Mchoro unaofuata unaonyesha ukweli huu:



Ikiwa humtafuti Mungu kufanya upya akili yako na kuponya hisia zako zilizo haribika, basi utaendelea kuchagua kuishi kutoka kwa imani hizo na hisia. Kila wakati mapenzi yako hufanya uchaguzi huo, unaimarisha imani yako ya uongo. (Kumbuka: Kwamba inaweza kuwa ni uchaguzi Zaidi wa kutofahamu kuliko moja ya kufahamu) kuendelea kuimarisha imani yako ya uongo, itafanya tu iwe ngumu Zaidi kuwekwa huru kutoka kwa imani hizo kwa sababu zinakuwa imara Zaidi. Kwa kuongezea, kuna tatizo lingine.

***UKICHAGUA kuishi kutoka kwa imani zako za uongo na hisia zilizo haribika, matokeo yatakuwa TABIA ZA KIMWILI.***

Kumbuka kutoka somo la kwanza tulizungumza kuhusu kuishi kutoka kwa “mwili” ni matokeo ya kuishi kutoka kwa imani zetu za uongo. Pia ni matokeo tunapoishi kutoka kwa hisia zetu zilizo haribika. Kutoka kwa mwili hutokea tabia za kimwili. Nadhani ni muhimu kusisitiza tena hoja hii kuelewa kwa nini ni muhimu kwamba tunaruhusu kubadilisha akili zetu na hisia. Ikiwa hatufanyi hivyo basi tunaendelea kuishi “kifo” cha tabia zetu za kimwili.

Napenda kushiriki mfano wa kibinafsi kufanya hoja hii. Nilikuwa na imani ya uongo kwamba nilikuwa bila utoshelezi imejaa na hisia zilizoharibika zinazoendelea za kutotosha. Matokeo ya kuchagua kuishi kutoka kwa imani yangu ya uongo ilitokea kwa tabia za kimwili ya kuwa na

umuhimu, kuhukumu, na uhaki nafsi. Yalikuwa tu mtiririko wa kuishi kutoka imani zangu za uongo. Zaidi nilivyoishi kutoka kwa imani hii ya uongo na hisia zilizoharibika, ndivyo Zaidi imani na tabia za kimwili zilikuja.

Kwa hivyo, hebu tuzungumze kuhusu mapenzi ya Mungu ya kubadilisha.

### **Mbadiliko ya Mungu ya mapenzi yako.**

*“Kwa maana akili iliyowekwa kwa mwili ni kifo, lakini akili iliyowekwa kwa Roho ni uzima na Amani” Warumi 8:6*

Natumai sasa unaweza kuona hata kwa uwazi Zaidi kwa nini akili zetu na hisia zinahitaji kubadilishwa. Ikiwa la, tunakuwa ‘kugwama’ katika kuishi kwa tabia zetu za mwili. Kwa hivyo:

***Tunapomtafuta Mungu KUUPYA akili zetu kwa ukweli na KUPONYA hisia zetu zilizoharibika, basi tutaanza kuchagua kuishi kutoka kwa UKWELI wa utambulisho wetu wa kweli badala ya imani zetu za uongo***

Je, mchakato huu wa mabadiliko hufanya kazi kwa namna gani? Kuonyesha, hebu turudi nyuma kwa mfano hapo juu kuhusu kutotosha kwangu. Mara nilipoanza kusoma utambulisho wangu wa kweli, basi nilianza kumtafuta Mungu ku upya akili yangu kwa ukweli wa kutosha kwangu katika Kristo. Mungu alipoanza ku upya akili yangu kwa ukweli, alianza kuponya hisia yangu iliyo haribika ya kutotosha.



Kile ambacho hii ilionekana kama ni kwamba kama matokeo yaku upya akili yangu kwa ukweli na kuponya hisia zangu, mapenzi yangu yalianza kusema, ‘la’ kwa mawazo na hisia za kutotosha. Katika maneno mengine, sikuwa nachukua tena umiliki wa mawazo hayo na hisia. Kwa muda, nilipoanza kuamini ukweli Bwana alianza kuniweka huru kutoka kwa tabia zangu za kimwili. Kile uhuru kilionekana kama ni kwamba nilijikuta nikirudia tabia yangu ya kimwili ya kuwa na umuhimu na kuhukumu na mwenye haki nafsi kwa uchache na uchache. Kwa kuongezea, Mungu alianza kubadili tabia hizi za kimwili na tabia za kiungu kama vile upendo, kukubalika, na ustahimilivu. Ilikuwa mchakato usio wa kawaida ambayo ilitokea kwa kipindi cha muda lakini kuongeza uhuru kutoka tabia hizi za kimwili ulikuja.

**Hapa ni baadhi ya hoja muhimu ya kukumbukwa katika mchakato wa Mungu wa kubadilisha:**

1. Kufanya upya akili yako kwa utambulisho wako wa kweli unaweza kuchukua muda Zaidi katika maeneo Fulani Zaidi yam engine kwa sababu baadhi ya imani zako za uongo zina NGUVU kuliko zingine kwa sababu umeziadini kwa muda mrefu.
2. Kwa hivyo, inaweza kuchukua kutembea kwa imani kwa MUDA FULANI kabla upate mabadilko yoyote ya maana katika kufikiria kwako, hisia au tabia.
3. Wakati wa nyakati hizo ambazo huhisi kwamba Roho anatembea haraka ya kutosha kukubadilisha, muombe Kristo AWE subira yako na ustahamilivu.
4. Mapema, chaguo lako la KIMSINGI itakuwa kuenda kwa tabia zako za kimwili, hata hivyo, unapokuwa unabadilishwa kwa muda, utapata tabia yako ya kimwili ikibadilishwa katika tabia ya kiungu.
5. Mtafute Mungu akufunulie wazo, chaguo, au tabia ambayo inabadilika unapomtafuta ku upya akili yako.

**Kumhusisha Mungu:** Mtafute Mungu aanze kubadili tabia yako ya kimwili na tabia ya kiungu.

### **Nini Matokeo Ya Moyo Uliyobadiliswa?**

*“Utaujua ukweli na ukweli utakuweka HURU.” Warumi 8:32.*


*Mungu anataka KUBADILISHA moyo wako ili akili yako, hisia, na mapenzi YATAAMBATANA na utambulisho wako wa kweli katika roho yako ya mwanadamu.*

Hebu tufanye muhtasari wa sehemu hii kwa kuangalia kwa matokeo ni nini ukimruhusu Mungu kubadilisha moyo wako:

1. Akili yako itaanza kufikiri na kuamini ukweli wa utambulisho wako wa kweli.
2. Hisia zako zitaanza kuambatana na ukweli wa utambulisho wako wa kweli.
3. Ikiwa akili yako ina amini ukweli na hisia zako zinaambatana na ukweli basi unaweza kuchagua kuishi kutoka kwa ukweli dhidi ya imani za uongo.
4. Matokeo yatakuwa kwamba Mungu **atabadilisha** tabia yako ya kimwili katika tabia ya **kiungu**.

Mchoro hapo chini unaonyesha nini matokeo Mungu anapobadilisha moyo wetu ili akili yetu , hisia , mapenzi na tabia zinaambatana na ukweli wa utambulisho wetu wa kweli.

# Mabadiliko ya Moyo



## UKWELI MUHIMU

*Kumbuka kwamba mabadiliko ni mchakato wa MAISHA YA MUDA MREFU.  
Moyo wetu unabadilishwa kwa kuendelea ili kuamini ukweli*

## SIKU YA NNE

### Nini hatua ya imani inaonekana kama Kuhusu Utambulisho

#### Wako



#### Hatua Za Imani Kuhusu Imani Zako Za Uongo

**Kumhusisha Mungu:** Chukua moja ya imani yako ya uongo kutoka Somo La Kwanza na uanze kuchukua hatua za imani ili Mungu kufanya upya akili yako kwa ukweli. Baadhi ya mifano ya hatua ya imani yaweza kuwa:

**Mfano #1:** “Bwana, ninaamini uongo kwamba sina utoshelezi. Neno lako linasema katika 2 Korintho 3:5 kwamba nina utoshelezi kabisa ndani yako. Nakuamini wewe kufanya upya akili yangu kwa ukweli.”

**Hoja muhimu:** Naamini kwamba ni muhimu kutumia na kuthibitisha ukweli wa Mungu unapochukua hatua za imani.

**Mfano #2:**“ Naamini uongo kwamba mimi ni wa kujitoshwa mwenyewe kwa sababu ya IQ yangu au uwezo. Nishawishi kwamba utoshelezi wangu unaweza tu kuwa ndani yako na sio mimi mwenyewe ninapotembea katika utambulisho wangu wa kweli”

### **Hatua za imani kuhusu Kuishi Kutoka Kwa Utambulisho Wako wa Kweli**

**Kumhusisha Mungu:** Nenda kwenye Somo La Tatu ambayo inao orodhesha sifa za utambulisho wako wa kweli. Chagua sifa moja au Zaidi ambazo unataka kupata Zaidi na uanze kuchukua hatua za imani ili Mungu kufanya upya kwa ukweli.

**Mfano #1 :**“Bwana ukweli ni kwamba nin utoshelezi kabisa katika wewe na kwa sababu ya hilo hakuna kitu chochote au mtu yeyote anaweza kuniibia usalama huo. Nakuomba wewe kunishawishi juu ya ukweli.”

**Mfano #2:**“ Bwana, ukweli ni kwamba nguvu zangu zinaweza tu kupatikana ndani yako. Nipe ufunuo jinsi nguvu zangu na uwezo hauna nguvu dhidi ya mwili wangu, nguvu ya dhambi, na shetani.

### **Hatua za imani ili kubadilisha Tabia ya Mwili**

**Zoezi:** Angalia katika tabia za kimwili mwishoni mwa Somo la Kwanza zinazotoka kwenye imani zako za uongo. Anza kuchukua hatua za imani kumhusisha Mungu kubadilisha maisha yako katika maeneo hayo.

**Mfano #1:** “Bwana, najua kwamba imani yangu ya uongo ya kutokuwa wa kutosha inanisababisha kuwa mtu wa kuridhisha watu na mwenye kudhibiti. Nakuamini wewe kufanya upya akili yangu kwa ukweli kwamba ninatosha kabisa katika utambulisho wangu wa kweli. Nakuomba wewe kunondoa mbali na tabia yangu ya kimwili ya kuridhisha watu na kudhibiti.”

**Mfano #2:** “Bwana, nataka kujilinda au kujiondoa kwenye hofu zangu. Fanya upya akili yangu kwa ukweli kwamba katika utambulisho wangu wa kweli sina hofu. Ondoa tamaa hiyo ya kimwili kujilinda au.....mwenyewe”

**Kumbuka:** Tabia yako haiamui utambulisho wako. Ikiwa unapambana katika eneo hili, chukua hatua za imani ili Mungu akushawishi juu ya ukweli huu. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya nini hiyo inaweza kuonekana kama.

**Hatua ya imani:**“ Bwana, hata kama tabia yangu inaniambia uongo kwamba sikubaliki au mtu asiye kubalika, nakuamini wewe kubadilisha maisha yangu ili niamini kwa imani kwamba katika wewe nakubalika kabisa na kukubalika.

**Hatua ya imani:** “Bwana nahisi sana hatia na aibu juu ya kile nilichofanya zamani. Napambana na kuamini kwamba mimi ni mwenye haki katika Kristo. Nishawishi kwamba ulishughulika na hatia hiyo na aibu kwenye msalaba na kwamba mimi ni mwenye haki kulingana na ukweli wako.”

### **Hatua za imani na Utambulisho Kuhusu Ndoa Yako**

**Ukweli muhimu:** Ikiwa mwenzi wako ni Mkristo, kumbuka kwamba wana utambulisho mpya pia. Kama matokeo, Mungu hakutaki tu wewe kujiona kama uumbaji mpya, lakini

pia anataka wewe kuona mwenzi wako kama uumbaji pia. Hivyo basi, huwezi tu kujiombea katika eneo hili, lakini pia unaweza kumwombea mwenzi wako pia. Hapa ni baadhi ya hatua za imani kuhusu utambulisho katika ndoa:

**Hatua ya imani:** “Bwana, nipe mimi na mwenzi wangu macho ya kiroho tujione kama uumbaji mpya.”

( Ikiwa mwenzi wako yuko radhi kushiriki imani zake za uongo na wewe, uko na fursa nzuri ya kumsihi kwa ajili yake katika maombi.)



**Hatua ya imani :** Mwenzi wangu anaamini uwongo kwamba yeye ni \_\_\_\_\_ Nakuomba wewe kubadilisha uwongo wake na ukweli yeye ni \_\_\_\_\_ katika Kristo.

**Ukweli muhimu :** Kuhisi kukataliwa na mwenzi ni moja kati ya mapambano makuu katika ndoa. Tunaweza kusema mambo kwa wenzi wetu ambayo huwafanya kuhisi kukataliwa. Habari njema ni kwamba kujua kuwa unakubalika kabisa katika Kristo na huhitaji kuchukua umiliki wa kukataliwa kwako na mwenzi wako. Je, itabadilishaje ndoa yako kwa kuishi kutoka kwa ukweli huo? Ifuatayo ni mfano wa jinsi hatua ya imani inaweza kuonekana katika sehemu hii.

**Hatua ya imani:**“ Nahisi kukataliwa na mwenzi wangu. Nishawishi kwamba nakubalika kabisa katika wewe na sistahili kuchukua umiliki wa kukataliwa huko. Unapofanya hivyo, nipeleke mbali na tamaa ya mwili kukataa pia.

## **SIKU YA TANO**

### **Hatua za imani na utambulisho katika mahali pa kazi**

**Ukweli muhimu :** Wakristu wengi (sana wanaume) wanajaribu kupata kutosha kwao, thamani, na utambulisho katika mahali pa kazi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya hatua za imani kwa Mungu kukubadilisha katika eneo hili.

**Hatua ya imani:**“ Ninajaribu kupata utambulisho wangu na hisia ya thamani kati mahali pangu pa kazi. Nakuamini wewe kubadilisha kufikiria kwangu ili nipate utambulisho wangu na thamani ndani yako.”

**Hatua ya imani:** “Bwana, sihisi kwamba nafikia kiwango kazini kwangu. Nahisi sana bila utoshelezi. Nakuamini wewe kufanya upya akili yangu ili kazi yangu isiamue utoshelezi wangu. Nishawishi juu ya ukweli kwamba utoshelezi wangu unazingatia juu ya mimi ni nani katika Kristo.”



**Kumhusisha Mungu:** Anza kuchukua hatua za imani katika moja au Zaidi ya maeneo haya kuhusu utambulisho wako wa kweli.

**Ukweli muhimu ya kukumbuka wakati wa kutembea kwako kwa imani**

Tulisoma kweli hizi katika *Kuishi Maisha Kutoka Chanzo Mpya* lakini nahisi ni muhimu kukukumbusha wewe kuzihusu kabla tuende hata Zaidi katika utafiti.

1. Ni muhimu sana kuelewa kwamba kubadilishwa kuishi kutoka kwa utambulisho wako wa kweli ni MCHAKATO. Ni safari na sio sprint.
2. Huenda USIHISI au KUPATA nguvu za Mungu kutiririka ndani yako unapoanza kuchukua hatua za imani lakini jua kwa imani kwamba Mungu ananya kazi.
3. Mungu hakwambii jinsi anavyofanya kazi. Tunaamini kwa imani kwamba anatubadilisha tunapotembea kwa imani.
4. Kutakuwa na upinzani katika kutembea kwetu kwa imani na mwili, nguvu ya dhambi, shetani na kwa akili yetu.
5. Huenda ukahitajika kuchukua hatua KADHAA za imani kabla upate mabadiliko yoyote katika namna unavyofikiria au kuhisi kujihusu.
6. Ikiwa utatembea kwa muda mrefu wa KUTOSHA kwa imani, mabadiliko YATATOKEA.

***Ukweli muhimu:***

***Hata kama akili yako inafanywa upya kwa ukweli, bado unapaswa kufanya UCHAGUZI kutembea ndani na kuishi kutoka kwa ukweli wakati kwa wakati.***

**Tunajua vipi kwamba mabadiliko yanatokea?**

Ahadi ni kwamba hatimaye utapata mabadiliko ambayo Mungu anafanya kwa mawazo yako, hisia, uchaguzi na tabia. Hebu tuchukue mtazamo wa ukaribu juu ya nini waweza kutarajia.



1. Unaanza kuwa na mawazo yanatoombatana na ukwelidhidi ya imani zako za uongo.
2. Akili yako inapo fanywa upya, hisia zako zitaanza kuambatana na kufikiria kwako.
3. Hii haimaanishi kwamba hutakuwa na hisia zilizofungika kwa imani zako za uongo lakini utajikuta haujibu mara kwa mara.
4. Akili yako inapofanywa upya na hisia zako kuambatana na ukweli, utajikuta kufanya uchaguzi unaozingatia ukweli.
5. Unapokuwa unabadilishwa, Mungu atabadilisha tabia yako ya kimwili kwa tabia ya kiungu.

## **Inaonekana Vipi Kuishi Kutokana na Ukweli Wa Utambulisho wako Mpya?**

Kuishi kutokana na **nguvu** ya Kristo ina maanisha kwamba hauhitaji tena kuishi kutoka kwa udanganyifu wa nguvu zako mwenyewe.

Kuishi kutoka kwa **ujasiri** wa Kristo inamaanisha kwamba hautegemei tena kwa ujasiri wako mwenyewe.

Kuishi kutoka kwa **usalama** wa Kristo una maanisha kwamba usalama wakohautegemei kwa kile dunia inatoa kama usalama.

Kuishi kutoka kwa **ushindi** wa Kristo ina maanisha kwamba unaishi kutoka kwa ushindi badala ya kujitahidi kupata ushindi.

Kuishi kutoka kwa **upendo** wa Kristo usio na masharti inamaanisha kwamba huhitaji kujaribu kupata uhitaji wako wa **upendo** usio masharti kutoka kwa wengine.

Kuishi kutoka kwa **kukubalika** kwa Kristo ina maanisha kwamba huwezi tena kukataliwa.

Kuishi kutoka kwa **msamaha** wa Kristo ina maanisha kwamba huna kisingizio cha kutosamehe wengine.

Kuishi kutoka kwa **uhuru** wa Kristo ina maanisha kwamba hauko tena katika utumwa kufanya dhambi.

Kuishi kutoka kwa **nguvu** ya Kristo ina maana kwamba uko na nguvu yake juu ya dhambi, mwili, shetani, na dunia

Kuishi kutoka kwa **utoshelezi** wa Kristo hauhitaji tena kuamini au kuhisi bila utoshelezi.

Kuishi kutoka kwa **hekima** na ufahamu wa Kristo ina maanisha kwamba hautegemei tena kwa yako.

Kuishi kutoka kwa **ufalme** wa Kristo ina maanisha kwamba huhitaji tena kujaribu kuwa katika udhibiti.

Kuishi kutoka kwa **usambazaji** wa Kristo inamaanisha kwamba huhitaji kujaribu kupata mahitaji yako kukidhiwa mahali pengine.

### **Muhtasari**

Hii ni hatua ya mageuzi katika utafiti ndani kwamba Mungu anataka wewe kushirikiana naye kwa imani ili yeye afanye upya akili yako na kubadilisha maisha yako ili usiamini tena uongo na kutoishi tena kutoka kwa tabia za uongo zinazotoka kwa uongo huo.

***Nini itakuwa matokeo usipochukua***

***hatua za imani kuhusu utambulisho wako wa kweli?***

## Somo La Tano

***Upinzani Kwa Mchakato wa Mungu wa Kubadilisha  
“mstari” Na Utambulisho Wako Wa Kweli.***

### **SIKU YA KWANZA**

#### **Utangulizi**


Katika somo liliopita, tuliangalia kwa kile inavyoonekana kuchukua hatua za imani kufanya upya akili zetu kwa utambulisho wetu wa kweli. Kama unavyojua kutoka Kitabu cha Kwanza, tunapochukua hatua za imani tutakutana na upinzani kwa mchakato wa Mungu wa kubadilisha. Kwa hivyo, tutaangalia katika namna ya kumhusisha Mungu ili kushinda upinzani.

#### **UPINZANI kwa mchakato wa Mungu.**

Sababu tatu za upinzani ni sehemu ya ‘utatu usio mtakatifu’ tuliozungumzia katika Kitabu ca Kwanza:


- Mwili
- Nguvu ya dhambi
- Shetani/mapepo

#### **Utatu Usio Takatifu**



Hata hivyo, kuna sababu zingine mbili zinazosababisha upinzani katika kutembea kwetu kwa imani. Moja ni hali na nyingine ni watu. Hapo chini inaonyesha kwamba tuna upinzani wa ndani kutoka kwa mwili na nguvu ya dhambi na upinzani wan je kutoka kwa shetani/mapepo, hali, na watu.-

## UKIUKAJI KWA MATEMBEZI YAKO YA IMANI



*Kutakuwa na upinzani USIOKOMA kwa mchakato wa Mungu wa kubadilisha kutoka kwa mwili wako, nguvu ya dhambi, shetani/mapepo, hali, na watu.*

Kwa hivyo, hebu tuanze kwa kuangalia jinsi mwili wetu hupinga mchakato wa Mungu wa kubadilisha.

## **1. Kupinga kwa mwili**



Mwanzo kabisa, kwa vile umekuwa ukiishi na imani yako ya uongo na tabia za kimwili, basi tamaa yoyote kubadilika itajenga upinzani kwa sababu tabia zako za kimwili zimeimarika sana. Hivyo basi, watu au hali .....imani hizo za uongo basi tabia za kimwili zinazohusiana na imani hizo za uongo moja kwa moja ‘zinapiga’ ndani. Zinakuwa tabia zako za ‘kimsingi’. Kile kilichofungika kwa tabia hizi za kimwili ndicho ninachoita ‘haki za kimwili’.

Hebu nikupe mfano kuonyesha hoja hii. Hebu tudhani kwamba wewe ndiye boshi wa kampuni yako mwenyewe na kwamba uko na imani ya uongo kujiamini. Hebu pia tudhani kwamba tabia za kimwili zinazotoka kwa imani hiyo ya uongo ni kwamba unakuwa wa umuhimu kwa wengine. Unapona kwamba mmoja wa wafanyakazi wako hawafikii kiwango chako unayohitaji, basi mwili wako utasema ‘niko na haki ya kuhitisha kile ninachohitaji kutoka kwake kwa wakati huwa inafikia hapo unapona mtu afikishi kiwango kile unayohitaji.

**ni nini Ukweli?**

**Ukweli ni kwamba hauna haki za kimwili**

Ukweli ni kwamba Mungu anataka akili yako upya ili ukweli wako uweze tu kupatikana katika Kristo (Wafilipi 1:60)

**Hivyo Mungu anatumia mbinu gani katika harakati ya kuondoa ukiukaji ya kimwili:**



- Kwanza, Mungu anataka nife ili (au kusonga mbali na )haki zangu za kimwili. – 2 Wakorintho 4:11
- Mungu anafanya hivyo kwa kuonyesha “kifo changu kwamba matendo yangu ya kimwili yanafanya mimi na wengine – Warumi 8:6.

- Mara moja nikitambua kifo cha matendo yangu ya haki yangu ya Kimwili, Ni lazima nimuita Mungu kufanya akili yangu upya kutumia ukweli .Mathayo 7:7
- Kama Mungu anavyoifanya upya akili yangu, atanifanya huru kwa kunipeleka katika sehemu ambayo sitaweza kutamanai kufanya mazoezi yoyote kuhusu haki ya kimwili. Yohana 8:32

Hebu tuyaweke haya maneno manne katika mifano yetu iliyo hapo juu, Kwanza Roho mtakatifu ananitaka nife kwa haki zangu za kimwili ya kuhititisha katika hali mbaya. Anafanya hivi kwa kunifunulia “kifo” (kusumbuka kwa Moyo) kwamba tabia zangu za kuhititisha zinanifanya mimi na wafanyi kazi wangu mara tu ninapoiona hiyo kifo. Ninaanza kuchukua hatua za imani hivi.

Mungu sasa nimeona dhahiri kifo kinachotokana na tabia zangu na haki zangu za kimwili inavyowaangamiza wafanyi kazi wangu. Ninakuamini uifanye upya akili yangu na ukweli na unifanye niwe huru kutotana na haki za kimwili.”

Baada ya kuomba kuufanya akili yako upya, hautawahi kuwa na tamaa ya kufanya haki za kimwili. Kwa kuongeza, utajipata tabia yako ikibadilika hadi utakuwa mpole na kuwaelewa zaidi wafanyi kazi wako.

**Kumuhusisha Mungu:** Umuombe Mungu akufunulie haki zingine za kimwili? muombe Mungu akufunulie kifo inayosababishwa na haki zangu za kimwili na kunifanya huru kwayo.

## **SIKU YA PILI**

### **2. JINSI NGUVU YA DHAMBI HUZUIA HATUA YAKO YA IMANI**

Kumbuka kwamba nguvu ya dhambi ndiyo inachangia katika tabia za kimwili kama vile muhudumu katika hoteli anaweza kukuletea sinia ya chakula, awali katika hatua yako ya imani nguvu ya dhambi inayo sehemu kubwa katika imani yako ya uwongo. Lakini ukimuruhusu Mungu kuufanya upya akili yako kwa utambulisho wa kweli, utapata kuwa nguvu ya dhambi hautakuwa na nguvu tena katika sehemu hiyo kwako.

**Mfano:** hebu tufanye kuwa unayo imani iliyo na nguvu sana kugusa au kuamini kuwa umetengwa. Hebu tufanye kuwa nguvu ya dhambi inachangia tabia zako za hasira, kujikinga, au tama ya kumkataa wenzako wakati mtu au kitu kimekusukuma kwa imani zako. Tuseme unaanza kumuomba Mungu aifanye akili yako upya kwa ukweli kwamba ukubalike nawe ukubaliwe.

Awali katika hatua ya mabadiliko haya (sababu nguvu ya dhambi imekuwa hivyo kwako) utachukua umiliki wa kuitika na mmoja au zaidi ya tabia hizi. Lakini kama Mungu anavyoanza kuufanya akili yako upya kwa ukweli, nguvu ya dhambi itajaribu kukukumbusha kuhusu zile tabia za kimwili lakini utajipata ukizikataa sababu umechukuwa umiliki kwa nini?

**Kuzoea Ukweli = NGUVU**



Ninamaanisha nini? kwa imani katika ukweli inazidi kuwa na nguvu zaidi, utajipata ukizoea nguvu za Mungu. Nguvu hii ni ya kiroho ambayo kwa muda itaanza kuuzidi nguvu ya dhambi. Ifikirie hivi hebu tuseme mtu aliyejijenga mwili hiyo inasimamia nguvu ya dhambi akiweka mkono wake akipimana nguvu na kijana mdogo.. Basi mkono wa mwenye nguvu ambaye ni nguvu ya dhambi atashinda. Lakini unavyozidi kuchukua hatua ya imani na (kuifanyia zoezi) kutakuwa na wakati ambao Mungu ameutoa nguvu yako yakiroho ya kujitakia hadi sehemu ambayo utakuwa ukisema hapana kwa nguvu ya dhambi na usichukue umiliki wa tabia za kimwili inayosababishwa na nguvu za dhambi.

**Kumuhusisha Mungu:** Mtafute Mungu kwa ukweli dhahiri ya utambulisho wako na umuombe akuzidishie nguvu yako ya kiroho ya kusema HAPANA kwa nguvu ya dhambi inapokuletea tabia za kimwili.

### **3. Shetani / Upinzani wa Kishetani kwa matembezi Yako ya Imani**

Tumeiongelea awali lakini kitu cha mwisho ambayo shetani na nguvu zake za mapepo hawataki ni wewe kuwekwa huru, unaona Shetani na mapepo wanatambua ukweli wa utambulisho wako. Wanajua uhuru na mabadiliko yatakayofanyika ukianza kutembea katika ukweli. hivyo mpango wao ni kukuweka mateka katika imani zako za uwongo.

**Kukamilisha hii, watajaribu kukuzuia kujua ukweli wa utambulisho wako**

Hata hivyo kama shetani na mapepo hawawezi kukuzuia kujua ukweli, watafanya kile waweza kukudidimisha katika matembezi yako ya imani unapo muomba Mungu kufanya akili yako mpya kwa ukweli. Wao hufanya hivi kupitia akili yako.

Hizi hapa ni baadhi ya mifano ya jinsi shetani / mapepo huunda ukiukaji akilini mwetu kwa mchakato wa mabadiliko kwa Mungu.

1. Kuingiza mawazo ya kukuhukumu unaporudi katika tabia zako za kimwili.
  - a. Jione umeshindwa tena
  - b. “Lazima uwe unafanya makosa sababu hakuna mabadiliko”.



2. Kujaribu kuleta shaka katika akili zako kwa kukutia mawazo kama:
  - a. “Hatawahi wekwa huru”
  - b. “Hii safari ya imani haifanyi kazi”
  - c. “Waweza pia kata tamaa”
3. Kutia shaka akilini mwako kuhusu uwezo au mapenzi ya Mungu kuyafanya upya mawazo yako
  - a. “Kama Mungu anaweza yafanya upya mawazo yako, mbona hajafanya hivyo hadi sasa?”
  - b. “Imani hii ya uwongo ina uzito sana hata kwa Mungu mwenyewe kubadilisha”

Awalii katika mabadiliko haya, utajipata kwa mawazo ya shaka na ya kulaani. Hata hivyo, utahitaji kujitambua na kumtafuta Mungu akuonyeshe chanzo cha mawazo yako.



Unapoendelea kukua kiroho, hali ya kuyajua mambo ndani yako itakua kiasi cha kwamba utakuja kujua hayo mawazo hayakutokana nawe.

Acha nikupe mfano wangu binafsi. Nakumbuka mapema nilipokuwa naanza kuyafunza haya mafunzo ya ukweli mtupu. Nilikuwa kwa kiwango changa sana kujua kwamba kwa hakika niko ndani ya Kristo. Imani yangu ya upungufu ilikuwa na nguvu sana. Sitawahi sahai kongamano la kwanza langu kufunza. Nilipomaliza, nilisikia haya: “Hawakupata uliyoyasema. Umewasilisha ujumbe wa hadhi ya chini sana. Kamwe hautawahi funza kama walimu walio na uzoefu.”

Ninapoangalia nyuma nyakati zile, ni wazi kwangu kwamba shetani au maroho zake walikuwa wanajaribu kunivuta nisifunze huu ukweli. Hata hivyo, Mungu alipoyageuza mawazo yangu kwa ukweli ya kwamba ukamilifu uko ndani yake, nikawa nataka sana kujua chanzo cha mawazo hayo.

**Mambo muhimu ya kukumbuka:** Shetani/mapepo sio wa kulaumiwa kitu kwa kudanganya kwetu, kulaani, au mawazo yenye shaka. Akili zetu zaweza zalisha mawazo hayo pia. La muhimu hapa ni ya kwamba tunapokua kwa njia zetu za imani, utambuzi wetu wa mambo utakua kiasi cha kwamba hatutamiliki hayo mawazo.

**Kumhusisha Mungu:** Unapokabiliana na undanganyifu, kulaumiana, au mawazo ya shaka kuhusiana na kujitambua kwako, anzisha “tabia takatifu” ya kumuuliza Mungu chanzo cha mawazo hayo.

## **SIKU YA TATU**

### **4. Jinsi Hali Tofauti Huleta Upinzani**

Hali tofauti zaweza leta upinzani kwa Mungu kuleta mageuzi na njia ya kukwamilia kwa imani za uongo, hisia potovu, na matendo ya kimwili. Tazama mfano huu:

Tuseme uko na imani ya uwongo ya kwamba wewe ni mtu mwoga. Uende kazini upate kuna kupunguzwa kwa watu kazini. Unapopata zile habari, woga unakuingia. Wakati huo, unamiliki huo woga, unao kupa hakikisho la imani yako ya uongo, na kuharibu fikira na nafsi yako.

**Kumhusisha Mungu:** Ni hali gani zinajirudiarudia na zinazokuzuia kuwa na uhuru kwa imani ya uongo? Mtafute Mungu akafunulie ndio akaitumie hiyo hali kuifanya wazi kwako hitaji lako kwake na akuongoze kumtegemea yeye kwa undani akakubadilishie kwa hiyo nafasi.

## **5.Watu Waweza Leta Upinzani**



Watu waweza leta upinzani hasa kamauko kwa urafiki au katika ndoa. Maneno ya kinyume ama ya kulaumiana kutoka kwa uhusiano huu waweza changia imani za uongo kukuhusu. Njia nyingine husiano hizi zinaweza leta upingamizi kwa kazi ya Mungu maishani mwetu ni kwa kutosameheana. Ukiwa umekosewa au kukataliwa na mwingine jambo naambalo linakupa hakikisho kwa imani yakoya uongo kuwa umekataliwa, hapo unaweza sema, “Niko na haki ya kutosamehe.” Hivyo basi,

**KumhusishaMungu:** Kuna watu katika maisha yakoeti kwa sababu ya maneno yao ya kimwili au mitazamo yao wanakuweka kwa utumwa wa imani zako za uongo au wanaleta mtazamo wa kutosamehe ndani yako? Mtafute Mungu akupe mapenzi ya nguvu ya “kiroho” usije ukachukulia maneno au mitazamo ya mwingine ya kimwili.

Kwa kifupi, ni muhimu kuelewa kutakuwa na upinzani wa wazi na uliofichika kutoka nje na na ndani pia. Nataka kumaliza hili somo kwa kujadili kilenichoita “Mstari.” Namini kwamba huu mfano utakusaidia kufahamu vyema njia ya Mungu ya kuleta mabadiliko.

### **“MSTARI”**

“Neno la Mungu ni hai na lina nguvu; ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili. Hukata kabisa mpaka mahali ambapo moyo na roho...” Waebrania 4: 12

Katika Waebrania 4:12, tunakumbushwa ya kwamba moyo na roho ziko tofauti. Tukiwa tumeelewa hali zote mbili, tazama mfano tutakaotumia katika mafunzo yanayoendelea uitwao “**Mstari.**”Kwa mfano ulio hapa chini, juu ya “mstari” ni kuishi kwa roho. Roho yako ni roho yako ya ubinadamu kwa muungano na Roho wa Mungu. Chini ya “mstari” ni kuishi kwa moyo wako.

### **ROHO**

**(Roho wa Mwanadamu kwa muungano na Roho wa Mungu)**

**JUU**

*MSTARI* \_\_\_\_\_

**CHINI**

**MOYO**

## **Mambo Mengine Mawili Tunayopaswa Kujua Kuhusu Moyo na Roho**

### **Yasiyoonekana Dhidi Ya Yanayoonekana**

2 Wakorintho 4:18 yasema: “Hivyo tunatazamia kwa makini si vitu vinavyoonekana. Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile visivyooonekana ni vya milele.”

Ufalme usioonekana ni ufalme ambao Mungu huishi na kutawala. Kama Wakristo, tunaishi kwa ufalme usioonekana wa muungano wetu na Mungu tunapotembea na uhuru naye. Ufalme unaoonekana ndipo uhai huchukua nafasi ndani ya mioyo yetu. Ni mahali pa hisia zetu tano.

**Kuweza kuishi kwa ufalme USIOONEKANA ni ukweli kwa Wakristo pekee.**

## **SIKU YA NNE**

### **Imani Dhidi Ya Uzoefu**

“Maana tunaishi kwa **imani**, na sio kwa **kuona**” 2 Wakorintho 5:7

Kuna tofauti mbili Zaidi tunahitaji kuangalia kuhusu ufalme unaoonekana na usioonekana. Pale na ambapo tunaishi kwa **imani** kataika 2 Wakorintho 5:7 ni ufalme usioonekana wa muungano wetu na Mungu. Ufalme unaoonekana katika mioyo yetu ni mahali pa mtazamo au uzoefu. Ni ndani ya moyo tunakohisi na kuyazoea maisha muda baada ya mwingine.

**Tamano la Mungu ni kwamba ufalme wa imani utakuwa wazi kabisa kwetu kuliko ufalme wa mazoea.**

Ni muhimu kutofautisha Maisha haya mawili kwa maana imani haihusu hisia na uzoefu. (Tutajifunza mengine mengi kwa undani kuhusu kanuni hii tunapoendelea na mafunzo.) Kumbuka imani lazima iwe na kifaa, na kifaa hiki kwa Mkristo ni Mungu. Tupate kuongeza kanuni hizi mbili kwa mchoro wetu wa mstari:

## **ROHO**

## (Roho wa binadamu kwa muungano na Mungu)

Ufalme Usioonekana – Imani

JUU

MSTARI

CHINI

NAFSI


Ufalme Unaoonekana – Uzoefu


**Swali:** Je, unafikiria ni kwa nini Mungu anataka ufalme usioonekana wa imani uwe uwazi mkuu Zaidi ya ufalme unaoonekana wa uzoefu?

**Mhusishe Mungu:** Unapoendelea na safari ya imani, muulize Mungu akuwezeshe kuufanya ufalme usioonekana kuwa wazi kabisa kwako kuliko ule ufalme wa mazoea.

### “Mstari na Utambulisho wetu

Tupate mlinganisho wa “mstari” kwa utambulisho wetu wa kweli ndani ya roho dhidi ya nafsi zetu. Tufanye hivyo kwa kuchukua michoro ya duara iliyo hapa chini na kuiweka kwa mchoro wa “mstari”.





Tuchukue picha hizi mbili hapa juu na tuziweke kwa mlinganisho wa “mstari” hapa chini. Ubinafsi wako wa kweli ndani ya roho ya binadamu uko juu ya mstari ilhali hali ya nafsi yako iko chini ya mstari.

**Ubinafsi wako wa kweli dhidi ya hali ya moyo wako**

	<u><b>ROHO</b></u>	
Upendo bila masharti	Utakatifu	Unyenyekevu
Salama	Kukubalika	Utulivu
Kusamehe	Shupavu	Kamili
Kuhurumiana	Kupambanua	Busara
Utosherevu	Kutoshereka	Ujasiri
Huru	Shukrani	Kukosa ubinafsi
Kufurahia	Ushindi	Nguvu
Kujitoa	Amani	Uzuri

---

**MOYO**

**Imani za Uongo**

*Hisia potovu au za kinyume zilizofunganishwa na imani za uongo*  
Uchaguzi wa kuishi kwaimani za uongo  
**Tabia Za Kimwili**

**SIKU YA TANO**

**Je, Mungu anataka Uishi Wapi?**

“Basi, ikiwa mmefufuka pamoja na Kristo, panieni mambo ya juu, kule Kristo aliko, ameketi upande wa kulia wa Mungu. Muwe na hamu ya mambo ya huko juu, na sio mambo ya hapaduniani.” Wakolosai 3:1, 2

Baada ya kuangalia picha tulizojifunza nazo, unafikiri Mungu anataka tuishi wapi? Je, ni juu ya “mstari” kutokana na utambulisho wetu wa kweli au ni chini ya “mstari” ndani ya mioyo yetu? Ni dhahiri kuwa Mungu anataka tuishi juu ya “mstari” kutoka kwa utambulisho wetu wa kweli. Ni Dhahiri kuwa Mungu anataka tuishi kwa ukweli kuliko kuendelea kuishi na uamini wa undanganyifu.

**Tamano la Mungu ni tuishi**

**JUU ya “mstari” kwa utambulisho wetu wa kweli.**

**Tutaishi Je Juu Ya “Mstari”?**


Tutaishi je juu ya “mstari” na tuyaweke mawazo yetu kwa mambo yaliyo juu? Tutapata uzoefu wa yote yaliyo ya kweli kwetu kwa utambulisho wetu? Jibu ni **imani**. Sio tu kwa muungano

wetu ni mahali pa imani, bali imani ndiyo hututoa kwa kuishi kutokana na nafsi zetu na kuishi kwa roho. 1 Yohana 5:4 yasema imani ndiyo ushindi:

“...hivi ndivyo **tunavyoushinda** ulimwengu: kwa **imani** yetu.” 1 Yohana 5:4

“Basi, pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Kwa maana kila mtu anayemwendea Mungu ni lazima aamini kwamba Mungu yuko, na kwamba huwatunza wale wanaomtafuta.” Waebrania 11:6

Picha inayofuata inatueleza vile imani hutupeleka kutoka kwa kuishi kwa moyo hadi kuishi kutokana na roho:



tuutumie ukweli huu ulioko kwa picha hapa chini. Sehemu ya mchakato wa Mungu ni kuanza kuchukua hatua za imani kuishi juu ya “mstari” kwa iutambulisho wetu.

### Imani Ndiyo Hukupeleka Hadi Kuishi Juu Ya Mstari

	<u>ROHO</u>	
Upendo bila masharti	Utakatifu	Unyenyekevu
Salama	Kukubalika	Utulivu
Kusamehe	Shupavu	Kamili
Kuhurumiana	Kupambanua	Busara
Utosherevu	Kutoshereka	Ujasiri
Huru	Shukrani	Kukosa ubinafsi
Kufurahia	Ushindi	Nguvu
Kujitoa	Amani	Uzuri
		↑ I M A N I
	<b>MOYO</b>	
	Imani za uongo	

**Hisia potovu au za kinyume zilizofunganishwa na imani za uwongo**

**Uchaguzi wa kuishi kwaimani za uongo**

## **Tabia Za Kimwili**

### **“Mstari na Mabadiliko ya Mungu kwa Moyo**

Kama tulivyojifunza hapo awali, Mungu anataka kubadili nyoyo zetu ili;

**Fikira** – zigeuzwe upya ndio kuamini ukweli wa utambulisho wetu.

**Hisia**- anza kujua tunachoamini kuhusu utambulisho wetu wa kweli

**Mapenzi** - kuchagua kuishikwa utambulisho wetu

**Tabia za Kikristo** – ndio mazao

Tazama picha inayofuata apate kujua mabadiliko ya moyo yanavyofanana kwa mlinganisho wa mstari:

**Kutembea Kwa Njia Ya Imani huruhusu Nguvu Za Mungu Kubadili Nyoyo Zetu**

### **ROHO**

**Upendo bila masharti**

**Salama**

**Kusamehe**

**Kuhurumiana**

**Utogetherve**

**Utakatifu**

**Kukubalika**

**Shupavu**

**Kupambanua**

**Kutoshereka**

**Unyenyekevu**

**Utulivu**

**Kamili**

**Busara**


**Ujasiri**



Huru  
Kufurahia  
Kujitoa

Shukrani  
Ushindi  
Amani

Kukosa  
Nguvu  
Uzuri



---

MOYO

**Kufanya upya mawazo yetu kwa ukweli**  
*Mawazo na hisia potovu na zenye kinyume  
zinazoishi pamojana ukweli*

**Kuchagua Kuishi Kwa Ukweli**  
**TABIA ZA KIKRISTO**

**Kwa kumalizia**

Natumai huu ulinganisho wa mstari unakusaidia kuona vyema tofauti kati ya hali moyo na roho wa binadamu.

**Somo la Sita**

**Kuwa Na Uzoefu Wa Mtazamo Wa Kikristo Kwa Moyo**

**Ukweli Wa Mwisho Kuhusu Utambulisho Wetu**

**SIKU YA KWANZA**

**Lengo La Mwisho La Mungu Kwa Moyo Wako Ni Lipi?**

Neno la mwisho la Mungu moyoni mwako linapatikana katika Wafilipi 2:5, 2 Wakorintho 3:18, na Wagalatia 4:19;

“Muwe na msimamo ule ule aliokuwa nao Kristo Yesu.” Wafilipi 2:5

“Basi sisi sote ambao nyuso zetu hazikufunikwa, tunaona kama katika kioo, utukufu wa Bwana; tunabadilishwa tufanane Zaidi na huo mfano wake kwa utukufu mwingi Zaidi. Hiyo ni kazi yake roho wa Bwana.” 2Wakorintho 3:18

“Watoto wangu, mimi nataabika tena kwa ajili yenu mpaka hapo hali yake Kristo itakapoundwa ndani yenu.” Wagalatia 4:19

Mistari hii tatu inatueleza nini?

**Lengo la mwisho la Mungu ni kwa ajili ya tabia za kutambulika kwako kwa roho ya ubinadamu kujidhihirisha kwao walio na mtazamo wa Kikristo moyoni mwako.**

Kuhusu kutambulika kwako, mageuzi ni mchakato ambapo tabia za utambulisho hujidhihirisha kama mtazamo wa Kikristo ndani ya moyo wako. Nini mtazamo wa Kikristo?

**Mtazamo wa Kikristo ni jambo la jaribio la kweli ndani ya moyo wako**

**Kwa utambulisho wa roho wa binadamu**

**Mfano:** Tabia tatu zangu za utambulisho ndani ya roho ni kwamba mimi ni mtosherevu, salama, na mwenye kusamehe. Jinsi Mungu anavyobadilisha moyo wangu, nitaanza kufikiria, kuhisi na kuchagua kuwa mtu wa kutosheka, salama na mwenye kusamehe.

Matunda ya Roho katika Wagalatia 5:22, 23 ni mifano ya utambulisho wako kwa roho wako ya kwamba yatakuja kujidhihirisha kama wenye mtazamo wa Kikristo kwamoyo:

“Lakini matokeo ya kuongozwa na roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhiri, uaminifu, upole na kiasi...”

Tunaona ukweli uo huo katika Wakolosai 3:12-14:

“Nyinyi ni watu wa Mungu; yeye aliwapenda na kuwateua. Kwa hiyo basi, vaeni moyo wa huruma, wema, unyenyekevu, upole na uvumilivu. Vumilianeni nakusameheana iwapo mmoja wenu analo jambo lolote dhidi ya mwenzake. Mnapaswa kusameheana kama Bwana alivyowasamehe nyinyi. Zaidi ya hayo yote, zingatieni upendo, kwani upendo huunganisha kila kitu katika umoja ulio kamili.” Wakolosai 3:12-14

Ifuatayo ni orodha ya mojawapo ya tabia zako za utambulisho wako. Mapenzi ya Mungu ni kubadilisha moyo wako ili tabia hizi ziwe za Kikristo.

Mapenzi bila masharti	Kustahiki	Unyenyekevu
Salama	Kukubalika	Utulivu
Kusamehe	Karimu	Shupavu
Huruma	Kupambanua	Busara
Kutosha	Kushukuru	Mjasiri wa Kristo
Kujitoa	Utakatifu	Kutokuwa na ubinafsi


Huru  
Kufurahia

Ushindi  
Amani

Nguvu  
Wema

**Zoezi;** Ni zipi tabia tatu za utambulisho wako waroho ungependa kuzoea kama tabia za kikristo moyoni mwako?

Wakumbuka picha ya tabia za utambulisho kwa kristo kwa roho wako?



Sasa, tazama picha inayoonyesha utambulisho wako ndani ya roho wako ukijidhihirisha kama mtazamo wa Kikristo moyoni:



**Tofauti Kati Ya Mtazamo Wa Binadamu Na Ule Wa Kikristo**

**Mtazamo wa binadamu** – ni mtazamo unaoweza kubadilishwa na mawazo, hisia, mwili, nguvu za dhambi, hali, uhusiano, shetani, am dunia

**Mtazamo Wa Kikristo** – huu ni mtazamo unaosalia bilakubadilishwa na mawazo, hisia, mwili, nguvu za dhambi, hali, uhusiano, shetani, au hata dunia

**Mifano ya kuishi kwa Mtazamo wa Kikristo:**

1. Waweza poteza kazi yako, lakini hiyo hali hainyakui mtazamo wako wa Kikristo ya amani na ujasiri
2. Unaweza kuwa umekataliwana mtu, lakini kukataliwa kule hakunyakui mtazamo wa Kikristo wa kujikubali ndani yako
3. Waweza kuwa umejeruhiwa, lakini unawasamehea kwa vile unavyoishi na Maisha ya Kikristo ya kusameheana.
4. Hali zingine au mtu Fulani aweza fanya ujihisi duni, lakini hiyo haikunyanganyi mtazamo wa Kikristo wa utoshelevu

## **Mungu Anataka Kilicho Cha Haki Kwa Roho Yako Kiwe Cha Haki Kwa Moyo Wako**

Kando na kufanya upya mawazo yako, kuponya hisia zako, na kubadilisha mapenzi yako, utaanza kuzoea tabia ya utambulisho wa moyo wako. Mchoro unaofuata onaonyesha ukweli huu:

### **ROHO**

**Upendo bila masharti**

**Salama**

**Kusamehe**

**Kuhurumiana**

**Utosherevu**

**Huru**

**Kufurahia**

**Kujitoa**

**Utakatifu**

**Kukubalika**

**Shupavu**

**Kupambanua**

**Kutoshereka**

**Shukrani**

**Ushindi**

**Amani**

**Unyenyekevu**

**Utulivu**

**Kamili**

**Busara**

**Ujasiri**

**Kukosa ubinafsi**

**Nguvu**

**Uzuri**

---

### **MOYO**

#### **Pata uzoefu wa Utambulisho Wako wa Kweli**

Njia nyingine ya kuelezea haya ni kwa njia ya picha ifuatayo:

**Mabadiliko yaonyesha kuwa ambacho ni ukweli katika  
Roho ni ukweli katika Moyo**

### **ROHO**

**Upendo bila masharti**

**Salama**

**Kusamehe**

**Kuhurumiana**

**Utosherevu**

**Utakatifu**

**Kukubalika**

**Shupavu**

**Kupambanua**

**Kutoshereka**

**Unyenyekevu**

**Utulivu**

**Kamili**

**Busara**

**Ujasiri**

Huru  
Kufurahia  
Kujitoa

Shukrani  
Ushindi  
Amani

Kukosa ubinafsi  
Nguvu  
Uzuri

---

### MOYO

Upendo bila masharti  
Salama  
Kusamehe  
Kuhurumiana  
Utosherevu  
Huru  
Kufurahia  
Kujitoa

Utakatifu  
Kukubalika  
Shupavu  
Kupambanua  
Kutoshereka  
Shukrani  
Ushindi  
Amani

Unyenyekevu  
Utulivu  
Kamili  
Busara  
Ujasiri  
Kukosa ubinafsi  
Nguvu  
Uzuri

## SIKU YA PILI

### Mchakato wa Mungu Wa Kubadili Moyo

Tupate kutazama kwa undani zaidi kuhusu mchakato wa Mungu wa kubadili moyo wako. Tuseme unaamini uongo kuwa huko salama, hujatoshereka, na uko mwoga. Unachukua hatua hatua za imani, na unapoendelea, utapata kujua unapata uzoefu wa usalama wa Kristo, utoshelevu, na ushujaa. Kila hatua ya imani unayochukua itaongezea uzoefu wa kuwa na uhakika wa usalama wako, utosherevu, na kutokuwa na uwoga ndani ya Kristo. Picha ifuatayo inaonyesha mchakato wa Mungu moyoni:


### **Mchakato Wa Mabadiliko**

Salama  
Utoshelevu  
Shupavu


**ROHO**  
**MOYO**

---

SIO SALAMA  
DUNI  
WOGA



Salama  
Toshelevu  
Shupavu



**SALAMA**  
**Toshelevu**  
**SHUPAVU**

Kubadilishwa kwa moyo ni mchakato wa hatua kwa hatua ambapo hatimaye, utapata uzoefu moyoni kwa kilicho cha kweli kwa utambulisho wako.

## **Mtazamo Wa Kweli Katika Kutembea Kwako Kwa Imani Kwa Kutumia Mstari**

Ingawaje hutaki kurudi kwa imani zako za uongo katika safari ya imani, utajipata umerudi kwa hizo imani duni jambo na ambalo litasababisha tabia za kimwili. Mbona? Kwanza, hiyo ni mahali pako pa mazoea. Kwa hii, namaanisha kuwa, kuishi kwa imani ka uongo ni jambo umezoeana nalo.


Kwa kuongezea, unapoanza kutembea kwa imani, una “imani dhaifu” ama Yesu anachokiita “imani ndogo”. Imani yako dhaifu ni matokeo ya kiwango cha kutoamini Mungu ni nani na anavyoweza na atakavyofanya. Pamoja na imani yako dhaifu ni uamini wenye nguvu wa uongo na kuandamana kwa mwili. Kuamini kwako kwa uongo na mwili kutaleta mtego mkuu kwako mwanzoni, lakini unapoendelea kuzoea imani yako, ukweli utakuwa na nguvu zaidi kuliko nguvu za uongo wa uamini na mwili.

Tupate kuangalia ukweli huu tukitumia mlinganisho wa “mstari”. Utaona kwa upande wa kushoto wa picha, ya kwamba mwanzoni mwa safari yako ya imani, utatumia muda zaidi chini ya mstari ukiishi kwa imani za uongo na tabia za kimwili. Hata hivyo, unapoendelea na njia yako ya imani, utajipata ukitumia muda zaidi juu ya “mstari” ukiishi kwa utambulisho wa kweli.

# Ukweli kuhusu mtazamo wa kutembea kwa imani

## Roho

Unatumia muda mwingi kuishi katika utambulisho wako wa kweli .



**UNATUMIA MUDA MCHACHE KUISHI KATIKA IMANI za  
na tabia za kimwili**

## Moyo

### **KUMBUKA:**

**Ukweli nikwamba utageukia maisha ya kibinafsi au ya kimwili kama chanzo chako wakati mwingi, lakini kumbuka kwamba wakati mwingine, unaweza tubu na kurudi kwa Mungu kama chanzo chako.**

Hata kama utarudi kwa mwili mara mingi, hii haikufanyi mwenye kushindwa na sio sababu yako kujilaumu. Sababu? Warumi 8:37 yasema kuwa wewe sio wa kufeli machoni mwa Mungu ila tuko zaidi ya washindi ndani ya Kristo. Haufai kujilaumu unapofeli kwa sababu Warumi 8:1 yatueleza:

“Kwa hivyo, sasa **hakuna hukumu** kwa wale walio katika **Kristo.**”

Minajiri u ndani ya Kristo, Mungu hakulaumu tena, na huhitaji tena kujilaumu. (Natamai hii ni habari njema kwako kuona Wakristo wengi hutumia wakati mwingi wakijilaumu.) Ukifeli, unakiri makossa yako kwa Mungu na kugeukia kumtumainia yeye. La mno hapa ni:

**Hata ukirudi nyuma kwenye mwili wakati mwingi,  
La muhimu ni kutosita kumtafuta Mungu kwa imani.**



**Kumhusisha Mungu:** Unapoendelea na safari ya imani, muombe Mungu akushwishi kwamba hata ukirudi nyuma kwa mwili, wewe sio wa kushindwa. Kiri dhambi zako na umrejee yeye kwa kutubu na uendeleze safari. Usipoteze muda katika kujilaumu.

## **UKWELI WA MWISHO KUHUSU MCHAKATO WA MABADILIKO WA MUNGU**

### **1. # Mwanzoni mwa safari yako ya imani, utahitaji kuwa kwa ngazi za kimataifa kuhusu mchakato wa Mungu wa kudadili**

Kwa kuwa imani yako za uongo zinaweza zimewekwa kwako zamani, ni muhimu sana kuwa na urefu wa safari yako ya imani. Kwa hii, namaanisha ni vyema kumtafuta Mungu akutengenezee upya fikra zako na kukufanya huru. Pia, kwa kuwa upinzani una nguvu zaidi mwanzoni, ni muhimu kutafuta nguvu za Mungu kwa kiasi kikuu kuvunja na kuangusha upinzani.

### **2. # Majira ya Mungu ya kubadili yaweza kosa kulingana na ratiba yako**

“Kila kitu kina majira yake, kila jambo duniani lina wakati wake.” Mhubiri 3:1



Unapoendelea na safari hii ya kubadilishwa, tamanio lako litakuwa kwa Mungu kuyafanya upya mawazo yako na kugeuza uamini wa uongo haraka. Hata hivyo, utakuja kujua ya kwamba ratiba ya Mungu na yako hazifanani. Kwangu mimi, Mungu daima hufanya kazi polepole kuliko ninavyotaka. Hata hivyo, lazima tujue vyema kwamba Mungu anafahamu yote na kwamba ana ratiba kamili. Sababu nyingine ya majira ya Mungu ni kuwa anakufunza uviumilivu unapongoja akubadilishe. Jambo la muhimu Mungu analokufunza katika kungoja ni kuwa na inani. Tutajifunza kwa namna ipi nyingine ila kwa kupata fulsa za kungoja Mungu? Mtu Fulani alieleza imani kama: “Unaweza amini kwa muda upi bila kupata badiliko maishani?”

**Kumhusisha Mungu:** Ikiwa una changamoto na majira ya Mungu kuhusu mabadiliko, mtafute yeye awe uvumilivu wako unapoendelea na safari ya kubadilishwa.

### **3. # Mabadiliko ya Mungu maishani Mwako ni Yasiyo Ya Kawaida**

“Mawazo yangu si kama mawazo yenu, “asema Bwana. “wala njia zangu si kama njia zenu.” Isaiya 55:8

Kama matokeo ya Mungu kukupa ufunuo wa ukweli wake kama ulivyowasilishwa kwa mafunzo haya, unaweza kuwa unaanza safari ya kimataifa ya ushirika na Mungu kuyafanya upya mawazo yako kwa utambulisho wako wa kweli na Kristo. Naamini kuwa mojawapo ya mambo muhimu unayohitaji kuelewa unapoanza safari ya kubadilishwa ni kuelewa kwamba ni mchakato usio wa kawaida.

Mungu anaenda kubadili kwa njia ya ajabu unavyofikiri, hisi, chagua, na kutenda. Ni jambo la kushangaza ya kwamba, sisi, kwa undani wetu, hatukuweza (na hatuwezi) fanya hayo mageuzi. Tunataabika na haya kwa maana sote tunataka kujua jinsi Mungu atatubadilisha. Hii ndiyo sababu kutembea kwetu ni kutembea kwa imani. Mungu anatuuliza tumtumainie yeye katika mchakato wake wa kutubadilisha kwa njia ya kiajabu maishani.

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu daima akukumbushe kuwa mchakato wake sio wa kawaida na kuwa hauhitaji kujua jinsi Mungu anavyokuweka huru kutokana na imani zako za uongo.

## **SIKU YA TATU**

### **4. # Unaweza Kosa Kujua Nguvu Za Mungu Zikikubadilisha**

Baada ya miaka kadhaa ya kufunza na kupeana ushauri, kuna ukweli mkuu ambaonaamini ya kwamba kila Mkristo anahitaji kuelewa kuhusu kutembea kwa imani:

***Unapochukua hatua ya imani, waweza kosa  
Kujua ama kufahamu nguvu za Mungu zikifanya kazi ndani yako.***

Tupate kutazama Waebrania 11:1 tupate kujua zaidi kuhusu kuhisi, uzoefu na imani

“Kuwa na imani ni kuwa na hakika ya mambo tunayotumainia; kusadiki kabisa mambo tusiyoyaona.”

Mambo mawili muhimu kwa kifungu hiki ni uhakika na kutiwa hatiani. Hakuna mahali popote kwa maelezo haya tunaona kwa imani maneno “kuhisi” ama “uzoefu” kwa nini hii ni shida kwa wakristo wengi? kama binadamu, tunahisi na kuzoea maisha kupitia moja au zaidi ya ya akili zetu tano kila mda. Kwa kuwa hisia na uzoefu ni viungo muhimu maishani mwetu ni lahisi kuitimisha kuwa tunaposhukua hatua ya imani, tunahisi na kufahamu kazi ya Mungu. Tafadhali usiskie nikisema kuwa hisia na uzoefu haziwezi

kuongoza safari yetu ya imani. Hata hivyo, unaweza kosa kuwa unahisi ama kufahamu nguvu za Mungu zikimiminika ndani yako na anapobadilisha maisha yako. Yafuatayo ni ukweli unao umuhimu kuelewa:

**UKWELI MUHIMU:**

**Kwa sehemu kuu, imani ni “KUAMINI” kando na Hisia au mazoea yetu.**

**Kumhusisha Mungu:** Muombe Mungu akupe hakikisho ya kwamba yuafanya kazi ndani yako hat kama haupati kuiona hiyo kazi. Muombe Mungu kukuwezesha kuona ufalme wa imani ukiwa halisi kama ufalme unaoonekana.

**5. # Kwa nini mabadiliko kwa nyaja zingine yaweza kuja kwa haraka kuliko zingine**

Imani zingine zako za uongo zaweza kuwa zimekolea kulikozingine. Kwa mfano, waweza kuwa na imani ya uongo ya kutokuwa salama na amabayo haijakolea kama uamini wa uongo wa ukosefu. Hivyo basi, utapata uhuru kutokana na kutokuwa salama kabla ya kupata utoshelevu. Kwa hivyo, jua ya kwamba inavyokuchukua muda mrefu kupata uhuru wa kutoka kwa imani moja ya uongo dhidi ya nyingine ni ishara kwamba baadhi ya imani zingine zako zina nguvu zaidi na zitachukua muda mwingi kuzivunja.

Kwa ajiri ya nguvu za imani zako za uongo katika maisha yako, utapatana na kufeli katika mwendo wa kukombolewa kutokana na imani hizo. Hili ni jambo la kutarajiwa kufanyika. Hivyo basi, usimkubalie adui au mawazo yako kukukemea unapofeli. Kiri makosa yako kwa Mungu na uendelee kuchukua hatua nyingine ya imani.

**6. # Unapoanza Kubadilishwa, Ujasiri Wako Kwa Mungu Utakua**

Sitakuja kusahau wakati nilipoanza kupata uhuru kutoka kwa imani yangu ya uongo ya kutotosheleka na wasiwasi. Kujiamini kwangu ndani ya uwezo wa Mungu kukaanza kukua. Sikua napata kutosheleka kwake na amani. Vile tabia yangu ilianza kwenda sambamba na ukweli na sikuwa tena mateka wa hasira na mtazamo wenye shaka, kujiamini kwangu ndani ya Mungu kukakua hata zaidi. Hivyo basi, ukitembea kwa umbali kwa imani, utaweza kupata kubadilishwa na utapata kujiamini kwako kwa uwezo wa Mungu ukikua.

**Je, Nitajuaje Wakati Nimepata Badiliko?**

Kwa kuwa mchakato wa kubadilika ni la kuongezeka polepole, nitajuaje badiliko linafanyika? Katika Warumi 15:8, Paulo anatumia kwamba Mungu atatuhakikishia ahadi zake:

“Maana nawaambieni Kristo aliwatumikia Wayahudi apate kuonyesha uaminifu wa Mungu, na zile ahadi Mungu alizowapa babu zetu zipate kutimia.”

Tunajua ya kuwa, kwa imani, Mungu anafanya kazi ndani yetu. Hata hivyo, Mungu anataka kukupa hakikisho kwako kwa akili, wasia, hisia, na tabia vilevile. Basi, nimenakili njia kadhaa ambazo Mungu anaweza tumia kukuhakikishia kazi yake maishani mwako.

1. **Unaanza kuwaza mawazo ya kweli badala ya mawazo ya uongo kukuhusu**
2. **Utajipata ukiamini ukweli wa Mungu kukuhusu badala ya kuamini uongo**
3. **Hisia zako zitaanza kwenda sambamba na ukweli wa Mungu kuhusu utambulisho wako.**
4. **Utaanza kufanya maamuzi yaliyo na msingi wa ukweli unaofikiria sasa na kuhisi. Hii itazaa ndani yako kutamania zaidi kuja kwa Mungu ndio akufanyie upya mawazo yako kwaukweli.**
5. **Unaanza kupata badiliko kwa tabia zako unapoamini ukweli wa utambulisho wako**
6. **Utaanza kuchagua kuishi maisha ya mtazamo wa Kikristo badala ya mtazamo wa kimwili**

Hiyo nibaadhi tu ya mifano ya jinsi Mungu atakupa hakikisho la kukubadilishia imani zako za uongo na ukweli wake. Kutambua kazi zake ni kuwa na ufahamu au ushujaa. Daima kuwa mtazamo wa jinsi Mungu atahakikisha kazi yake kwa maisha yako. Kumbuka kuwa atabadilisha kila mmoja wetu kwa njia ya kipekee. Hivyo basi, hamna fomula ya jinsi Mungu atafanya kazi kwa kila mmoja.

**Unapomhusisha Mungu kwa imani, muombe akuhakikishie mabadiliko yake ndani**

## **Inavyokaa Katika Maisha Yako Ya Kila Siku Kuishi Kwa Utambulisho Wako Wa Kweli**

### **SIKU YA NNE**

#### **Ndoa**

Ni hoja zipi ulizonazo kwa uhusiano wako wa ndoa?

1. **Utambulisho**
2. **Mapenzi yasiyo na masharti**
3. **Kukubalika**
4. **Kusameheana**
5. **Dhamani**
6. **Kutokuwako kwa ubinafsi**
7. **Usalama**

## **Utambulisho**

Tabia iliyoko kwa ndoa ni kutathmini vibaya wenzetu kwa misingi ya tabia zao za kimwili. Lakini, kama mwenzako kwa ndoa ni mkristo, ni viumbe wapya tu kama wewe.

**Kuishi kwa utambulisho wako wa kweli:** I namaanisha kwamba unaweza tazama nyuma kwa mwenzako kwa ndoa na uone tabia zake za kimwili (sisemi kuzikubali) na uone vile walivyo viumbe wapya ndani ya Kristo. Kumbuka tu kama wewe, tabia zake haziamui utambulisho wao.

**Swali:** Inaweza badikaje vile unavyomuona mpenzi wako ukimuona kama kiumbe kipya ndani ya Kristo badala ya kumulika tu tabia zake za kimwili?

## **Upendo usio na masharti**

Kama binadamu, sote tunataka kupendwa kwa upendo usio na masharti. Hata hivyo, kama binadamu, hatuwezi kumpenda mwingine bila masharti. Kutakuwepo na masharti kwa kumpenda mwingine.

**Kuishi kwa utambulisho wako wa kweli:** Ukweli ni kuwa katika utambulisho wako wa kweli, umependwa bila ya masharti na Kristo aliye mpenzi bila masharti. Basi, kwa kuwa hilo hitaji limeshughulikiwa na Kristo, waweza omba Kristo ampende mpenzi wako kupitia kwako na upendo usio na masharti.

**Swali:** unafikiri ndoayako ingekuwaje kama ungapenda mpenzi wako na upendo usio na masharti?

## **Kukubalika**

Ninapofanya uanafunzi katika ndoa, Napata kuwa tatizo kuu ni kukataliwa. Tunakuja kwa ndoa namahitaji na matarajio. Wakati hayo mahitaji na matarajio hayashughulikiwi, mtindo ni kuwakataa wapenzi wetu. Kama wewe ndiwe mwathiriwa wa ile kukataliwa, pia nawe unajibu

na kumkataa mwenzako. Hivi ndivyo mzunguko wa kukataliwa huenda. Isiporekebishwa, itakuja kulete ile ndoa chini.

**Kuishi kwa utambulisho wako wa kweli:** hauhitaji tena kumiliki kukataliwa na mpenzi wako kama unaishi kwa kujikubali ndani ya Kristo. Kwa maneno mengine, unakuwa **hauwezi katalika**

**Swali:** Je, unafikiri ndoa yako yaweza badilikaje ukiacha kumiliki kukataliwa na mpenzi wako?

## **Msamaha**

Katika ndoa, kama mke na mme tutakoseana. Kama wewe ndiye mwenye kukosewa, uko na chaguo. Unaweza ukamsamehe mpenzi wako, ama unaweza pata mtazamo kuwa unamdai mwenzako (iliyo kutosamehe). Kama huo ndio mtazamo wako, unaweza ishia kukupelekea kwa hasira, machungu, na kutosamehe zaidi.

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Ukweli ni kwamba hauna sababu yoyote ya kutomsamehe mpenzi wako kwani unamsamehe mtu aliye ndani ya Kristo (Wakorosai 3:13). Kumbuka kuwa Kristo alitusamehe sote dhambi zetu na maovu.

**Swali:** Inawezaje kubadili ndoa yako kama ungekuwa wa kwanza kuomba msamaha au kusamehe wakati unapokosewa?

## **Dhamani**

Tunataka sote kudhamaniwa na kuonekana wa dhamana, hasa katika uhusiano wa ndoa. Hata hivyo, tunaonekana kuyaweka matarajio vile hiyo dhamani inafaa kuonyeshwa na wapenzi wetu. Pale na ambapo yale matarajio hayafikiwi, tunaonekana kuhisi kutodhaminiwa.

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Ukweli ni kwamba dhamani yako ya kweli yaweza patikana tu ndani ya Kristo (Zaburi 139:14). Dhamani yako kwa Kristo haina uzani.

**Swali:** Inaweza badilisha ndoa yako vipi kama ungekuwa unapata dhamani yako yote ndani ya Kristo badala ya mpenzi wako?

## **Kutojiweza**

Jambo la muhimu sana kwa ndoa kamilifu ni isiyo na ubinafsi na iliyona mtazamo wa kujitoa. Shida ni kuwa kwa mwili, tuko wabinafsi sana na wasiojitoa.

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Ukweli ni kuwa unapoishi nje ya utambulisho wako wa kweli, utakuwa mbinafsi kiasili (Wafilipi 2:4) na kujitoa (Yohana 15:13).

**Swali:** Ni sehemu zipi katika ndoa yako uliko mbinafsi na asiyejitoa? Inaweza badilisha ndoa yako kiviipi kama ungeendelea kwa kujitoa na bila ubinafsi?

## **Usalama**

Kama mke na mume, tunataka kuhisi tukiwa salama kwa ndoa zetu, salama kwa kuaminiana, na salama kwa upendo wetu n.k. Kunafanyika nini wakati usalama huo umetiwa mashakani?

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** usalamandani ya Kristo ni muhimu kwa ndoa kwa maana kama binadamu, tunaweza afikiana na huo usalama. Wakati hayo yanapofanyika, tunafaa kukumbuka ya kwamba usalama wa kweli na wa hakika hutokana na utambulisho na Kristo. Wakati usalama wabinadamu unapofeli, lazima tutegemee usalama ndani ya Kristo.

## **Mahali pa kazi**

**Ni masuala kama yepi unayokabiliana nayo kwa mahali pa kazi?**

**Zawezakuwa:**

4. Mkazo kazini?
5. Kiwango cha kuridhika au kutoridhika uliyo nayo na kazi yako?
6. Mtazamo wako kwa bosu au wafanyikazi wenzako?

**Ni mahitaji kama yepi unayoweza kuwa ukitafuta kwa mahali pa kazi kuhusiana:**

- Utambulisho wako?
- Dhamani, dhamana au sifa?
- Kukubalika kwako?
- Usalama wako?

Tupate kuona namna ya kuishi kwa utambulisho wako utaadhiri vyema mahali pako pa kazi.

## **Mkazo wa kazi**

Mkazo utakuwa sehemu ya kazi zetu mahali petu pa kazi. La mno ni, “Utachukulia kumiliki mkazo?” Jibu ni LA!

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Katika Kristo, uko na nguvu zake zote. Hivyo basi, una nguvu za kusema LA kwa mkazo. Hauhitaji tena kuwa mmiliki wa mkazo kwa mahali pako pa kazi.

**Swali:** Unafikiri nini kinachoweza kubadilika kwa mtazamo wako katika mahali pako pa kazi kama ungeacha kumiliki mkazo?

## **Kiwango cha kuridhika au kutoridhika ambayo uko nayo kazini mwako**

Sote tuko na viwango vya kuridhika au kutoridhika na kazi zetu kulingana na ni sehemu gani katika kazi inayojadiliwa. Swali ni, “Nini huamua kuridhika kwako?”

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** ndani ya Kristo, kuridhika kwako hakutegemei kazi yako ila ni kwa furaha inayotiririka kutoka kwa utambulisho wako kwa Kristo (Wagaratia 5:22,23).

**Swali:** Inaweza badilikaje jinsi unavyofanana kazini kama furaha ya Kikristo ingeamua kuridhika kwako kwa kazi yako badala ya hali ya kazi?

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:**ukiwaunaishi katoka katika unakubalika kwa utambulisho wako wa kweli (Warumi 15:7), hauhitaji tena kuchukua umiliki wa kukataliwa kule kwa wafanyakazi wenzako au mdosi.

Swali: Inaweza leta uzuri upi kwa mtazamo wako kwa wenzako kazini na pia mdosi wako ukiacha kumiliki tena kukataliwa na wao?

## **Ulinzi**

Tunapendezwa na maneno “usalama wa kikazi”. Hata vile, tunajua ya kuwa usalama huo unaweza enda na usiku mmoja. Unaweza hisi vipi kupata kesho asubuhi umepoteza kazi yako?

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Ukweli ni kwamba usalama wa hakika unapatikana kwa Kristo (Zaburi 139:5). Kama unaishi kwa usalama wa Kristo katika utambulisho wako wa kweli, kupoteza kazi yako haitapokonya usalama wako.

## **SIKU YA TANO**

### **Hali tofauti**

Hali mbaya zaweza sababisha kuhisi:

- Woga
- Kupoteza kujiamini
- Kushindwa
- Kutotoseleka
- Myonge



## **Woga**

Hali mbaya kama hali duni ya kiafya yaweza leta woga

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:**Ukweli ni kuwa katika utambulisho wako wa kweli, wewe sio wa kuogopa (Zaburi 56:4) kwani hauna chochote cha kuogopa. Mungu amejua kuhusu hali yako kwa kuishi milele na ana jibu. Ikiwa una ugonjwa ulio katika kiwango cha mwisho, hamna haja ya kuogopa kwa sababu ya mwisho wa safari yako baada ya kifo. Hauna cha kuogopa kwa kuwa Mungu ndiye mlinzi wako.

## **Kukosa kujiamini**

Sote tuko na kiwango cha kujiamini. Wakristo wanaochukulia maisha kwa uzuri wana kujiamini sana kuliko wengine. Hata vile, hali kama kupoteza kazi zetu zzaweza kunyakua kujiamini kwetu.

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Kama viumbe wapya, kujiamini kwetu ni katika Kristo (Zaburi 71:5). Kupitia imani yake, hatuhitaji tene kuenenda kwa kujiamini kwetu kwa kimwili. Hakuna kinachoweza kunyakua imani yetu katika Kristo.

**Swali:** Umezata kufikiria kuhusu upana wa Mungu katika maisha yetu ya kuharibu kujiamini kwetu ndio tukose chaguo lingine ila kutembea kwa imani ya Kristo?

## **Kushindwa**

Kuzoea kwa dhambi inaweza tuacha tukihisi tumeshindwa.

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:**Ukweli ni kuwa sisi tu washindi katika Kristo (1 Wakorintho 15:57). Hatufai kuhisi kushindwa kwani tuna ushindikatika Kristo. Kuhusu dhambi inayatuweza, tunaweza chagua kutembea kwa imani katika ushindi tulio nao ndani ya Kristo, au tuchague kututa tamaa. Kukata tamaa inamaanisha ya kuwa hisia za kushindwa zitaendelea ndani yako.

**Swali:** Je, unataka kuchukua hatua tosha za imani hadi upate ushindi ulio nao katika Kristo? Kama sio hivyo, unatarajia nini?

## **Hali duni**

Hisia zetu za hali duni zaweza onyeshwa kwa njia mingi kama vile kukosa kazi, kuhisi kana kwamba hatupati kipimo cha kiwango tulio weka kwetu wenyewe au kwa wengine, ama kuweza kupata kipimo cha kiwango wengine wametuweka.

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Taarifa muhimu ni kuwa utoshelevu wako unaweza tu kushughulikiwa ndani ya Kristo. Kila kitu maishani mwako ina uwezo wa

kukunyanganya kutosheleka kwa ubinadamu. Hakuna hali ama mtu anafaa kunyakua kutosheleka kwako ndani ya Kristo.

**Swali:** Inaweza badili maisha yako kiviipi kama ungeacha kupeana kutosheleka kwako kwa kukutana na viwango vyako mwenyewe ama viwango vilivyowekwa na wengine kwako?

## **Myonge**

Hkuna agetaka kujiona mnyonge (hasa wanaume). Tunataka kuwa na nguvu za ndani za kibinadamu ambazo zinaweza kustahimili shida zozote. Hata hivyo, Mungu anatupenda kutosha kukubalia hali mbalimbali kuja ndio zianike unyonge wetu wa kiutu.

**Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli:** Nguvu zetu za kweli zaweza tokana tu kwa Kristo (Waefeso 6:10). Tunapoishi katika nguvu za Kristo, hamna kinachoweza kunyakua hizo nguvu kutoka kwetu. Ndio Paulo akasema kuwa, "...kwa radhi naudhaifu, ndipo ninapokuwa na nguvu" (2 Wakorintho 12:10).

## **Ulezi**

### **Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli kama mzazi inamaanisha:**

1. Unapoishi kwa utambulisho wako wa kweli, una uvumilivu wote wa Kristo unapatikana kwako. (Na watoto wako, utapata yote unayoweza kupata)
2. Kujua utambulisho wako wa kweli utakuwezesha kuwafunza watoto wako kuhusu utambulisho wako ndani ya Kristo. Ingekuwa vyema sana kama wangejua mapema wao ni nani ndani ya Kristo.
3. Unapotembea kwa utambulisho wako mpya, watoto wako watakuiga
4. Hauhitaji tena kujaribu kupata kukubalika kwa watoto wako kwa kujua kwamba umekubalika na Kristo.
5. Utaweza kuwapenda watoto wako bila masharti bila kujali mitazamo au tabia zao za kimwili.
6. Unaweza kuadhibu tabia zao mbaya bila kushambulia utambulisho wao. Kwa mfano: Wakati mtoto wako anakosea, unaweza sema, "Tabia yako ni mbaya" badala ya kuchambulia utambulisho wake kwa kusema "Wewe ni mbaya"

Mahusiano mengine

### **Kuishi kwa utambulisho wetu wa kweli na wengine inamaanisha:**

1. Kwa kuwa wewe ni mwenye kusamehe ndani ya Kristo, unaweza msamehe yeyote iwe unahisi hivyo ama la.
2. Kwa kuwa umekamilika ndani ya Kristo, hauhitaji kuwategemea wengine kukufanya kuimalika.
3. Kutembea kwa utambulisho wako mpya utakuruhusu kuwapenda wale uliowaona kutopendeka

4. Kwa kuwa umetoshereka kikamilifu, hauhitaji kuchukua umiliki wa kukataliwa na wengine

Kumbuka una chaguo

Inapofika ni kutembea kwako kwa imani kwa kubalishwa kutembea katika utambulisho wako wa kweli, una chaguo mbili zifuatazo:

**Chaguo la kwanza: Kuendelea kuishi katika imani yako ya uwongo**

**Matokeo: Taabu mingi, tabia mingi za kimwili, na hakuna badiliko**


**Chaguo la pili: Kuendelea kuenenda kwa imani**

**Matokeo: Kufanywa upya kwa mawazo yako, uhuru kutoka kwa imani zako za uwongo, na kubadilishwa kutoka kwa tabia zako za kimwili kwa tabia za Kikristo.**

Mchoro ufuatao unaonyesha chaguo zako mbili:

**Kuendelea kuamini imani za uwongo kukuhusu = taabu mingi, tabia za kimwili na kutobadilika**

**Kuishi kwa utambulisho wa kweli = kufanyiwa upya kwa mawazo, nakupata tabia za Kikristo**



**Je, utachukua chaguo lipi?**

**Ukweli ni kuwa una chaguo moja tu!**

Chaguo la hakika ulilo nalo tu ni kuja kwa Mungu kwa imani na kutumainia katika uwezo wake kubadilisha imani yako ya uwongo. Mungu anajua mchakato huu wote. Ni yeye tu anayeweza kubadili upya mawazo yako kwa ukweli. Anajua vyema vile imani zako potovu zilivyo, lakini ana ufahamu wa vile inaweza badilishwa kwa kuwa ni yeye tu


anayeweza kukutoa kutoka kuamini uongo kwenda kwa ukweli. Hata vile, Mungu hukupa uhuru wa kufanya uamuzi.

**La muhimu kukumbuka kutomchagua Mungu ni kuchagua Ninachoita  
“mambo tu ya bure”**

Hivyo basi, nakuhimiza utembeke kwa njia za imani katika upya wako na Kristo. Unapofanya vile, pazia la uongo litapasuliwa mara mbili, na nyuma ya lile pazia, utaona uwazi wa ulivyo. Unaposhirikiana na Mungu kwa imani, Warumi 6:4 itakuja kuwa mazoea ya maisha yako:

**“Tulipobatizwa tuliungana na kifo chake, tukazikwa pamoja naye, ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka wafu kwa kitendo kitukufu cha Baba, sisi pia tuweze **kuishi maisha mapya**” Warumi 6:4**

### **Nitaenda wapi toka hapa?+**



Umemaliza kukisoma Kitabu cha Pili kati ya mafatano manne ya uanafunzi yanayoitwa “*Living A Transformed Live In Christ*”. Kitabu cha tatu cha mfuatano huu kinaitwa “*Being Transformed*”. Kama ungependa mafunzo haya, ningependa utembelee tovuti yetu ya huduma ambayo ni [www.christislifeministries.com](http://www.christislifeministries.com) na uangalie chini ya sehemu ya “Store”. Utapata mfuatano uitwao “*Living A Transformed Life In Christ*”. Utaona chini ya kifungu mtaala uitwao **Being Transformed**. Unaweza kuzinunua kwa mtandao au ututumie ujumbe kwa anuani zilizoko hapa chini. Ama unaweza pakua nakala haya bure na utoe nakala nyingi unavyopendezwa.

**Kubadilishwa itahusisha yafuatayo:**

- **Hali ya moyo wakati wa kupata wokovu**
- **Mchakato wa Mungu wa kuyafanya upya mawazo yako kwa ukweli**
- **Vita tunazozipata katika akili zetu**
- **Vita vya kiroho**
- **Mchakato wa Mungu wa kuponya vidonda na hisia zilizoharibiwa**
- **Mchakato wa Mungu wa kupeleka matamania yetu kutoka kwa kutopenda kwa kupenda**

Hivyo basi, ni matumaini yangu utaamua kuyapitia mafunzo ya Kubadilishwa kwa njia ya maombi. Kama ungetaka kuongea nami, anuani zangu ziko hapa chini. Ningetiwa moyo sana kusikia vile haya mafunzo yamegeuza maisha yako.

**Huduma za Kristo ni Uzima**

**Tovuti : [www.christislifeministries.com](http://www.christislifeministries.com)**

**Barua pepe: [bill@christislifeministries.com](mailto:bill@christislifeministries.com)**